# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA ADHABU, NAM. 6 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA ADHABU, KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kubakiza baadhi ya Sheria.
3. Sheria ya jumla ya tafsiri na ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### ENEO LA MATUMIZI YA SHERIA


4. Mipaka ya Mamlaka za Mahakama.
5. Sehemu ya makosa yanapotendwa ndani ya mamlaka na sehemu ya makosa yanapotendwa nje ya mamlaka.


### SEHEMU YA TATU
### MISINGI YA JUMLA KUHUSU UWAJIBIKAJI WA KIJINAI


6. Kutokujua sheria.
7. Kudai haki kwa nia njema.
8. Nia au dhamira.
9. Dhana isiyo ya kweli.
10. Kuchukuliwa kuwa na akili timamu.
11. Ugonjwa wa akili.
12. Ulevi.
13. Umri mdogo.
14. Maafisa wa Mahakama.

15. Kushurutishwa.
16. Haki ya kujilinda.
17. Matumizi ya nguvu katika kujilinda.
18. Pale haki ya kujilinda inapotumika na kusababisha kifo.
19. Kutumia nguvu katika kukamata.
20. Shurutisho kutoka kwa mume.
21. Mtu kutokuadhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile.

## SEHEMU YA NNE
## WASHIRIKI KWENYE MAKOSA

22. Wakosaji wakuu.
23. Makosa yanayotendwa na wakosaji walioshirikiana katika kutekeleza kusudio moja.
24. Kumshauri mwingine kutenda kosa.

## SEHEMU YA TANO
## ADHABU

25. Aina mbali mbali za adhabu.
26. Adhabu ya jumla.

## SEHEMU YA SITA
## UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA SERIKALI

27. Uhaini.
28. Kuingia Zanzibar kwa nia ya kupanga dhidi ya Mapinduzi.
29. Kuchochea uvamizi
30. Kuficha uhaini.
31. Makosa yanayohusiana na uhaini.
32. Ukomo wa kuendesha kesi ya uhaini.
33. Kuchochea uasi.
34. Kuwasaidia Wanajeshi au Maafisa wa Polisi katika vitendo vya uasi.
35. Kuwashawishi Wanajeshi au Maofisa wa Polisi kutoroka.
36. Kusaidia kwa kujua mateka wa vita kutoroka.
37. Kuruhusu kwa uzembe mateka wa vita kutoroka.
38. Tafsiri ya kitendo cha dhahiri.

39. Viapo visivyo halali ili kutenda makosa makubwa.
40. Viapo vyengine visivyo halali ili kutenda makosa.
41. Kwa kiasi gani kulazimishwa kunakuwa utetezi.
42. Mafunzo ya kijeshi yasiyo halali.
43. Kuchapisha taarifa za uongo.
44. Kuchochea kufanya ghasia.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA NCHI ZA NJE NA UTULIVU WA NJE

45. Kukashifu.
46. Uandikishaji wa wanajeshi wa Kigeni.
47. Uharamia.

## SEHEMU YA NANE
## MIKUSANYIKO ISIYO HALALI, MAANDAMANO, GHASIA NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA UTULIVU WA JAMII

48. Maana ya jumuiya na jumuiya isiyo halali.
49. Kuwa mwanachama au kuongoza jumuiya isiyo halali.
50. Masharti yanayohusiana na uendeshaji wa mashtaka chini ya kifungu cha 49.
51. Uwezo wa kuingia.
52 Kutangazwa jumuiya isiyo halali.
53. Kuchukua mali.
54. Maana ya mkusanyiko usio halali na ghasia.
55. Adhabu ya mkusanyiko usio halali.
56. Adhabu ya kushiriki katika ghasia.
57. Kutoa tangazo kwa wafanya ghasia kutawanyika.
58. Kutawanyika kwa wafanya ghasia baada ya tangazo kutolewa.
59. Ghasia baada ya tangazo.
60. Kuzuia au kupinga utoaji wa tangazo.
61. Wafanya ghasia kubomoa majengo.
62. Wafanya ghasia kuharibu majengo.
63. Kuingilia kwa ghasia gari au chombo cha baharini.

64. Kutembea na silaha hadharani na kumiliki silaha bila halali.
65. Kuingia kwa nguvu.
66. Kuzuia kwa nguvu
67. Kupigana hadharani.
68. Kuchochea mapigano ya watu wawili
69. Kutishia kwa kutumia nguvu.
70. Kusumbua na kuzonga.
71. Kutisha.
72. Mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo.
73. Silaha za hatari katika mikutano ya hadhara na kitendo cha uvunjifu wa amani.
74. Kuwa na silaha za hatari bila ya mamlaka ya kisheria.

## SEHEMU YA TISA
## MAKOSA YANAYOHUSU USIMAMIZI WA HAKI

75. Ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.
76. Maelezo ya uongo ya wakalimani.
77. Adhabu ya kutoa ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.
78. Ushahidi wa shtaka la kutoa ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.
79. Kutunga ushahidi.
80. Kiapo cha uongo.
81. Kudanganya mashahidi.
82. Kuharibu ushahidi.
83. Njama za kuzuia haki na kuingilia mashahidi.
84. Kufifilisha makosa
85. Kufifilisha mashtaka.
86. Matangazo kwa mali iliyoibiwa.
87. Kudharau Mahakama.

## SEHEMU YA KUMI
## KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAZUIA WATUMISHI WA MAHAKAMA

88. Kuokoa.
89. Kutoroka kwenye kizuizi halali.
90. Kusaidia wafungwa kutoroka.

91. Kutoroka kutoka kifungoni au kizuizini kwa makusudi au kwa uzembe wa mtumishi wa umma.

92. Uondoshaji wa mali iliyokamatwa kihalali.

93. Kuwazuia maafisa wa Mahakama.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA MCHANGANYIKO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA

94. Udanganyifu na uvunjaji uaminifu kwa watumishi wa umma.

95. Kuupuuza wajibu wa kikazi.

96. Kusababisha hasara kwa Serikali au Taasisi za Umma.

97. Kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa umma.

98. Kutokutii wajibu wa kisheria.

99. Kutokutii amri halali.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI

100. Kukashifu dini yoyote.

101. Kufanya ghasia kwenye mikusanyiko ya dini.

102. Kuingia sehemu ya makaburi bila halali.

103. Kuzuia mazishi ya mwili wa mtu aliyekufa.

104. Kuandika au kutamka maneno kwa nia ya kuumiza imani ya dini.

105. Kukashifu dini.

106. Kuhamasisha uadui baina ya makundi tofauti.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MAKOSA DHIDI YA MAADILI

107. Tafsiri ya kuingilia.

108. Kubaka.

109. Adhabu ya kubaka.

110. Adhabu ya kubaka kwa kundi.

111. Kujaribu kubaka.

112. Kutorosha mwanamke.

113. Kutorosha watoto wa kike na kiume

114. Shambulio la aibu.
115. Kunajisi mtoto wa kiume.
116. Kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili.
117. Kuwezesha ukahaba
118. Kuwezesha ngono haramu.
119. Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kiume kunajisiwa.
120. Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kike kuingiliwa.
121. Kumzuia mwanamke, mtoto wa kike au mtoto wa kiume katika danguro au penginepo
122. Uwezo wa kumtafuta mtu aliyezuiwa.
123. Kosa la ukahaba.
124. Mtu mwanamme anayeishi kwa kipato cha ukahaba.
125. Mtu mwanamke anayeishi kwa kipato cha ukahaba au kusaidia ukahaba.
126. Jengo linalotiliwa shaka na uwezo wa kupekua.
127. Danguro.
128. Njama ya kubaka.
129. Kujaribu kuwezesha kutoa mimba.
130. Kutoa mimba kwa mwanamke au mtoto wa kike.
131. Kutoa dawa au kifaa cha kuwezesha kutoa mimba.
132. Kujua umri wa mwanamke au mtoto wa kike si muhimu.
133. Makosa ya kuingilia kinyume na maumbile.
134. Kujaribu kutenda kosa la kuingilia kinyume cha maumbile.
135. Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume.
136. Matendo ya usagaji.
137. Matendo ya aibu kubwa baina ya watu.
138. Utumiaji wa watoto kingono.
139. Udhalilishaji mkubwa wa kingono.
140. Muungano wa watu wa jinsia moja.
141. Usumbufu wa kingono.
142. Uzinifu.
143. Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu.
144. Idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.
145. Kuweka wazi utambulisho wa muathirika.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NDOA NA MAHUSIANO YA KIFAMILIA

146. Ndoa ya hadaa.
147. Kufunga ndoa kinyume na Sheria.
148. Sherehe ya ndoa iliyofanyika kihadaa bila ya ndoa halali.
149. Ukatili kwa watoto.
150. Kutelekeza mtoto au mtu mwenye ulemavu.
151. Kupuuza kutoa chakula kwa mtoto au mtu mwenye ulemavu.
152. Mwajiri kutompatia mwanafunzi au mwajiriwa wake mahitaji.
153. Usafirishaji wa binaadamu.
154. Kuiba mtoto.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## MAUDHI NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA UTULIVU

155. Maudhi kwa jamii.
156. Nyumba ya kamari.
157. Mashine za kamari.
158. Nyumba ya kuweka dau.
159. Bahati nasibu.
160. Maana ya mtunza jengo.
161. Kusafirisha machapisho machafu.
162. Matendo machafu.
163. Watu wavivu na wenye tabia mbaya.
164. Wakorofi na wazururaji.
165. Makosa dhidi ya sare za kijeshi.
166. Kitendo cha uzembe kinachoweza kueneza maambukizo.
167. Kuchafua maji.
168. Kuchafua hewa.
169. Biashara mbaya.
170. Kutotii amri ya karantini.
171. Adhabu ya maudhi kwa jamii.
172. Kuendelea kwa maudhi.
173. Kuchanganya chakula na kitu chengine.

174. Kuuza chakula chenye madhara.
175. Kuchanganya dawa.
176. Kuuza dawa zilizochanganywa.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## KUUA, KUUA BILA YA KUKUSUDIA NA KUUA MTOTO MCHANGA

177. Kuua bila ya kukusudia.
178. Adhabu ya kuua bila kukusudia.
179. Kuua kwa kukusudia.
180. Adhabu ya kuua kwa kukusudia.
181. Nia ovu.
182. Kuua kwa kukasirishwa.
183. Maana ya kukasirishwa.
184. Maana ya kusababisha kifo.
185. Wakati mtoto anapochukuliwa kuwa mtu.
186. Ukomo wa muda wa kifo
187. Kuua mtoto mchanga.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## WAJIBU KUHUSIANA NA HIFADHI YA MAISHA NA AFYA

188. Jukumu la mtu anayemsimamia mtu mwengine.
189. Wajibu wa kiongozi wa familia.
190. Wajibu wa mwajiri.
191. Wajibu wa watu wanaofanya vitendo vya hatari au wenye dhamana ya vitu vya hatari.
192. Adhabu kwa kushindwa kutimiza wajibu.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUJIUA

193. Kujaribu bila halali kusababisha kifo.
194. Kusaidia baada ya kutendeka kosa la kuua kwa kukusudia.
195. Kutishia kwa maandishi kuua kwa kukusudia.

196. Kula njama ya kuua kwa makusudi.

197. Kusaidia kujiua.

198. Kujaribu kujiua.

199. Kuficha kuzaliwa kwa mtoto.

200. Kuharibu mtoto.

201. Kuficha mpango wa kutenda kosa.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA
## MAKOSA YA KUHATARISHA MAISHA AU AFYA

202. Kumzuia mtu kujihami ili kosa litendeke.

203. Kumpumbaza mtu kwa nia ya kutenda kosa.

204. Vitendo vinavyokusudia kusababisha madhara makubwa ya kimwili au kuzuia ukamataji.

205. Kumzuia mtu kujiokoa katika chombo.

206. Kwa makusudi kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa reli.

207. Kuhatarisha usalama wa chombo.

208. Madhara makubwa ya kimwili.

209. Kujaribu kujeruhi kwa kitu kinachoripuka.

210. Kuweka sumu kwa nia mbaya kwa lengo la kudhuru.

211. Kujeruhi na matendo yanayofanana na hayo.

212. Kushindwa kutoa mahitaji ya muhimu.

213. Wajibu kwa wanaofanya upasuaji wa kitabibu.

214. Wajibu wa kijinai.

215. Idhini haitoathiri uwajibikaji wa kijinai.

## SEHEMU YA ISHIRINI
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SHUGHULI ZA MAKUNDI YA KIJINAI

216. Makosa yanayohusiana na makundi.

217. Adhabu.

218. Tafsiri ya mwanachama wa kundi la kihalifu

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
## JINAI KWA KUTOJALI NA KUPUUZA


219. Tendo la kuharakisha au la kizembe linalosababisha kifo.

220. Vitendo vya kuharakisha na vya kizembe.

221. Kuondosha matonsisi.

222. Uondoshaji wa viungo vya binaadamu.

223. Vitendo vyengine vya uzembe vinavyosababisha madhara.

224. Ushughulikiaji vitu vya sumu kwa uzembe.

225. Kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa njia ya reli.

226. Kuonesha taa za uongo, alama au boya.

227. Kusafirisha mtu kwa njia ya maji kwa malipo katika chombo kisichokuwa salama au kilichojaza sana.

228. Hatari au kizuwizi kwenye njia ya umma au njia ya usafiri.


## SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
## MASHAMBULIO


229. Shambulio la kawaida.

230. Shambulio linalosababisha madhara ya mwili.

231. Mashambulio kwa watu wanaolinda vyombo.

232. Shambulio lenye adhabu ya kifungo cha miaka mitano.


## SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU
## MAKOSA DHIDI YA UHURU WA MTU


233. Tafsiri ya kuteka nyara kutoka Zanzibar.

234. Tafsiri ya kuteka nyara kutoka kwa mlezi halali.

235. Adhabu ya kuteka nyara.

236. Tafsiri ya kutorosha.

237. Kuteka nyara au kutorosha kwa ajili ya kuua kwa kukusudia.

238. Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumfungia mtu.

239. Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumsababishia mtu madhara makubwa au kumfanya mtumwa.

240. Kuficha mtu aliyetekwa au kutoroshwa kinyume na sheria.

241. Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kumuibia.

242. Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kudai fedha.
243. Kuzuia bila halali.
244. Kuweka kizuizini bila halali.
245. Adhabu ya kuzuia bila halali.
246. Adhabu ya kuweka kizuizini bila halali.
247. Kumnunua au kumuuza mtu yeyote kama mtumwa.
248. Mazoea ya kujihusisha na watumwa.
249. Kumlazimisha mtu kufanya kazi.

**SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE**
**WIZI**

250. Vitu vinavyoweza kuibiwa.
251. Tafsiri ya wizi.
252. Kesi maalum.
253. Fedha inayozuiliwa kwa maelekezo.
254. Fedha zinazopokelewa na wakala kutokana na mauzo.
255. Fedha inayopokelewa kwa niaba ya mwengine.
256. Wizi wa watu wenye maslahi katika kitu kilichoibiwa.
257. Mume na mke.
258. Adhabu ya jumla ya wizi.
259. Kuiba wasia, kitu kilichotumwa kwa njia ya posta au mnyama.
260. Kuiba kutoka maungoni au kuiba bidhaa zinazosafirishwa.
261. Kuibia Serikali.
262. Wizi wa makarani na watumishi.
263. Wizi wa wakurugenzi au maafisa wa makampuni.
264. Wizi wa mawakala.
265. Wizi wa wapangaji au wageni.
266. Kuiba baada ya kutiwa hatiani awali.
267. Wizi wa karafuu.
268. Wizi wa mazao.
269. Kutaifisha jengo ambalo mbao za wizi na miti imetumika katika ujenzi.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO
## MAKOSA YANAYOFANANA NA WIZI


270. Kuficha madaftari ya kumbukumbu.

271. Kuficha wasia.

272. Kuficha nyaraka.

273. Kuua mnyama kwa nia ya kumuiba.

274. Kuhamisha kwa nia ya kuiba.

275. Kuhaulisha kwa udanganyifu bidhaa zilizowekwa rehani.

276. Udanganyifu unaohusiana na madini katika migodi.

277. Kuchukua umeme kwa udanganyifu.

278. Kuchukua au kubadilisha kusikokuwa wizi.


## SEHEMU YA ISHIRINI NA SITA
## UNYANG'ANYI NA KUPORA KWA NGUVU


279. Tafsiri na adhabu ya unyang'anyi.

280. Unyang'anyi wa kutumia silaha.

281. Adhabu ya kujaribu kufanya unyang'anyi na kujaribu kufanya unyang'anyi wa kutumia silaha.

282. Shambulio kwa nia ya kuiba.

283. Kudai mali kwa vitisho vya maandishi.

284. Kujaribu kuchukua kwa vitisho.

285. Kuwezesha utekelezaji wa nyaraka kwa vitisho.

286. Kudai mali kwa kutishia kwa nia ya kuiba.

287. Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu.

288. Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu ya mtu aliyekufa.

289. Kuvunja uaminifu kijinai.


## SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA
## UVUNJAJI WA NYUMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO


290. Tafsiri ya kuvunja na kuingia.

291. Uvunjaji nyumba mchana na uvunjaji nyumba usiku.

292. Kuingia katika nyumba ya makaazi kwa nia ya kutenda kosa.
293. Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia kwa nia ya kutenda kosa.
294. Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia na kutenda kosa.
295. Watu kukutwa na silaha kwa nia ya kutenda kosa.
296. Kuingia kijinai.
297. Kutaifisha.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NANE
## UDANGANYIFU

298. Tafsiri ya udanganyifu.
299. Kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu.
300. Kujipatia utekelezaji wa dhamana kwa njia ya udanganyifu.
301. Kuhadaa.
302. Kujipatia mkopo kwa njia ya udanganyifu.
303. Kula njama ya kudanganya.
304. Udanganyifu katika kuuza au kuweka rehani mali.
305. Kujifanya kupiga ramli.
306. Kujipatia usajili kwa udanganyifu.
307. Tamko la uwongo ili kupata hati ya kusafiria.
308. Kujifanya Afisa wa umma.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TISA
## KUPOKEA MALI ILIYOIBWA AU ILIYOPATIKANA ISIVYO HALALI NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

309. Kupokea mali iliyoibiwa au iliyopatikana isivyo halali.
310. Watu wanaotuhumiwa kuwa na, au kusafirisha mali ya wizi.
311. Kupatikana na mali ya wizi.
312. Kuficha bidhaa.
313. Kukutwa na mali iliyoibiwa nje ya Zanzibar.

## SEHEMU YA THELATHINI
## UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WALIO KATIKA NAFASI ZA DHAMANA NA HESABU ZA UWONGO

314. Wadhamini kuharibu au kubadilisha mali za muamana kwa udanganyifu.
315. Ubadhirifu na udanganyifu wa Wakurugenzi na Maafisa wa Mashirika.
316. Maelezo ya uongo ya maafisa wa kampuni.
317. Hesabu za uongo.
318. Hesabu za uongo kwa Afisa wa umma.

## SEHEMU YA THELATHINI NA MOJA
## MAKOSA YANAYOSABABISHA UHARIBIFU WA MALI

319. Uchomaji wa mali kwa makusudi.
320. Kujaribu kuchoma mali.
321. Kuchoma moto mazao na mimea.
322. Kujaribu kuchoma moto mazao.
323. Kupeleka chombo mrama.
324. Kujaribu kupeleka mrama chombo.
325. Kujeruhi wanyama.
326. Adhabu ya kuharibu mali kwa makusudi.
327. Kujaribu kuharibu mali kwa miripuko.
328. Kusambaza maradhi ya kuambukiza kwa wanyama.
329. Kuondosha alama za mipaka kwa nia ya kudanganya.
330. Kuharibu kwa makusudi alama za upimaji na alama za mipaka.
331. Adhabu kwa kuharibu ujenzi wa reli au barabara.
332. Vitisho vya kuchoma au kuharibu.

## SEHEMU YA THELATHINI NA MBILI
## KUGHUSHI, UTENGENEZAJI WA SARAFU, UTENGENEZAJI FEDHA BANDIA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

333. Tafsiri ya kughushi.
334. Nyaraka.
335. Kutengeneza waraka wa uongo.

336. Nia ya kudanganya
337. Adhabu ya jumla ya kughushi.
338. Kughushi kunakoadhibiwa kwa kifungo cha maisha.
339. Kughushi hati ya Mahakama au waraka rasmi.
340. Kughushi na makosa mengine yanayohusiana na stempu.
341. Kutengeneza au kumiliki karatasi au zana za kughushi.
342. Kuwasilisha nyaraka za uongo.
343. Kuwasilisha nyaraka zilizofutwa au zilizomaliza muda.
344. Kuwezesha utekelezaji wa waraka kwa njia ya udanganyifu.
345. Kufuta mistari katika hundi.
346. Kutengeneza nyaraka bila mamlaka.
347. Kudai mali kwa nyaraka za wasia zilizoghushiwa.
348. Kununua noti zilizoghushiwa.
349. Kughushi hati za fedha zinazolipwa chini ya mamlaka ya umma.
350. Kughushi daftari la Kumbukumbu.
351. Kupeleka cheti cha uongo cha ndoa kwa mrajis.
352. Maelezo ya uongo kwa ajili ya daftari la uandikishaji wa vizazi, vifo au ndoa.
353. Kutaifisha.

## SEHEMU YA THELATHINI NA TATU
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SARAFU NA NOTI

354. Tafsiri.
355. Kughushi sarafu.
356. Matayarisho ya kutengeneza sarafu bandia.
357. Kupunguza sarafu.
358. Kumiliki vipande vya sarafu zilizokatwa.
359. Kutoa sarafu bandia.
360. Kurudia kutoa sarafu bandia.
361. Kuwasilisha chuma au sarafu isiyotumika kama sarafu kwa wakati huo
362. Kuingiza ndani ya nchi au kusafirisha nje ya nchi sarafu bandia.
363. Kutaifisha.
364. Kubadilisha noti ya kibenki na kuyayusha sarafu.
365. Utoaji wa noti usio halali.

## SEHEMU YA THELATHINI NA NNE
## STEMPU BANDIA


366. Kumiliki muhuri wa moto kwa madhumuni ya Kutengeneza stempu.

367. Karatasi na muhuri wa moto kwa ajili ya kutengeneza stempu za posta.


## SEHEMU YA THELATHINI NA TANO
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KOMPYUTA


368. Matumizi.

369. Makosa dhidi ya mali ya ubunifu.

370. Makosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta.

371. Kuharibu vifaa vya kompyuta.

372. Kuingilia taarifa.

373. Kuingilia mfumo wa kompyuta.

374. Kuingilia kati taarifa kinyume na sheria.

375. Vifaa visivyo halali.

376. Kosa dhidi ya watumiaji wa kompyuta.

377. Udanganyifu na kitendo kinachohusiana na kompyuta za Serikali.

378. Tafsiri ya maneno ndani ya Sehemu hii.


## SEHEMU YA THELATHINI NA SITA
## KUGHUSHI ALAMA ZA BIASHARA


379. Tafsiri ya alama ya biashara.

380. Kughushi alama za biashara.


## SEHEMU YA THELATHINI NA SABA
## KUJIFANYA MTU MWENGINE


381. Kujifanya mtu mwengine kwa ujumla.

382. Kwa udanganyifu anatoa maelezo ya kukiri dhima.

383. Kujifanya mtu aliyeandikwa katika cheti.

384. Kuazimisha, waraka au cheti kwa kujifanya mtu mwengine.

385. Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye uthibitisho wa tabia.

386. Kuazimisha uthibitisho kwa ajili ya kujifanya mtu mwengine.

**SEHEMU YA THELATHINI NA NANE**
**KUJARIBU**

387. Tafsiri ya kujaribu.
388. Kujaribu kutenda makosa.
389. Adhabu kwa kujaribu kutenda baadhi ya makosa.
390. Kushawishi au kuchochea wengine kutenda kosa ndani ya Zanzibar au kwengine.
391. Kupuuza kuzuia kosa.

**SEHEMU YA THELATHINI NA TISA**
**KULA NJAMA**

392. Kula njama ya kutenda kosa.
393. Njama nyenginezo.

**SEHEMU YA AROBAINI**
**WASHIRIKI WA UHALIFU BAADA YA KUTENDEKA KOSA**

394. Tafsiri ya kushiriki uhalifu baada ya kutendeka kosa.
395. Adhabu ya mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka.
396. Adhabu ya kumshawishi au kumchochea mtu mwengine kutenda kosa.
397. Kufuta na masharti ya mpito.

**JADWELI**

SHERIA NAMBA 6 YA 2018

NIMESAINI

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

16 Machi, 2018

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA ADHABU, NAM. 6 YA 2004 NA KUTUNGA SHERIA MPYA YA ADHABU, KUWEKA MASHARTI BORA ZAIDI PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Adhabu, 2018 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.

Kubakiza baadhi ya Sheria.

**2.**-(1) Hakuna jambo lolote katika sheria hii litakaloathiri:

(a) kuwajibika, kushtakiwa, au adhabu kwa mtu kwa kosa dhidi ya sheria nyingine yoyote inayotumika Zanzibar isiyokuwa na Sheria hii;

(b) kuwajibika kwa mtu yeyote kwa kushtakiwa au kuadhibiwa kwa kosa lolote chini ya masharti ya sheria yoyote inayotumika Zanzibar kuhusiana na mamlaka ya Mahakama inayohusiana na vitendo vilivyofanyika nje ya mamlaka ya kawaida ya Mahakama hizo;

(c) uwezo wa Mahakama yoyote kumpa adhabu mtu kwa kuidharau Mahakama;

(d) kuwajibika, kushtakiwa, au kuadhibiwa kwa mtu chini ya adhabu yoyote iliyopitishwa au itakayopitishwa kuhusiana na kitendo chochote kilichofanyika au kuanza kufanyika kabla ya kufutwa Sheria Namba 6 ya 2004;

(e) uwezo wa Rais wa Zanzibar kutoa msamaha au kupunguza adhabu au kufuta adhabu yote au sehemu ya adhabu au kuahirisha utimizaji wa hukumu yoyote iliyokwishatolewa au itakayotolewa; au

(f) sheria yoyote iliyoandikwa inayotumika kwa Idara maalum.

(2) Endapo mtu atatenda kosa ambalo linaadhibiwa chini ya Sheria hii na pia linaadhibiwa chini ya Sheria nyengine yoyote, mtu huyo hataadhibiwa kwa kosa hilo chini ya Sheria zote mbili kwa pamoja bali ataadhibiwa kwa Sheria moja wapo kati ya hizo.

Sheria ya jumla ya tafsiri na ufafanuzi.

**3.-(1)** Sheria hii itatafsiriwa kwa mujibu wa misingi ya tafsiri ya kisheria kama ilivyoelezwa na Mahakama zinazoendeshwa kwa kufuata Sheria za Nchi za Jumuiya ya Madola, na maneno yanayotumika katika Sheria hii yatachukuliwa kuwa yana maana inayotumika kwa mujibu wa Mahakama za Nchi za Jumuiya ya Madola na yatatafsiriwa ipasavyo, endapo tu yanalingana na mazingira halisi yaliyopo, na isipokuwa tu kama tafsiri itaelezwa vyenginevyo.

(2) Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"madhara ya mwili" maana yake ni maumivu au madhara yoyote yanayoathiri afya au hali ya mtu husika;

"mtoto wa kiume" maana yake ni mtu mwanamme mwenye umri chini ya miaka 18;

" madhara ya hatari" maana yake ni madhara yanayohatarisha maisha;

"nyumba ya kuishi" inajumuisha jengo lolote au kitu chochote kinachofanana na jengo au sehemu ya jengo au kitu kinachofanana na jengo ambalo likitumiwa na mmiliki au mtu anayetumia kwa ajili ya makazi yake mwenyewe binafsi, familia yake, watumishi wake au yeyote kati ya hao na haijalishi hata kama baadhi ya wakati halitumiki; jengo au kitu kilichokaribu ya jengo, au kilichokaribu na kitu kilichofanana na jengo kinachotumiwa sambamba na nyumba ya kuishi kitachukuliwa ni sehemu ya nyumba ya kuishi iwapo kutakuwa na mawasiliano kati ya jengo hilo au kitu kinachofanana na jengo na nyumba ya kuishi, ama moja

kwa moja au kwa njia iliyofunikwa au iliyozungushwa uzio inayoruhusu kutoka sehemu moja kwenda nyingine;

"mtoto wa kike" maana yake ni mtu mwanamke mwenye umri chini ya miaka 18;

"madhara makubwa" maana yake ni madhara ambayo yanasababisha ulemavu au madhara ya hatari, au madhara yanayodhuru afya kwa kiwango kikubwa au madhara ya kudumu ambayo yanayoweza kudhuru afya kwa namna hiyo, au madhara yanayosababisha ulemavu wa kudumu, au madhara makubwa au ya kudumu katika sehemu yoyote ya nje au ndani ya mwili, kiungo au viungo vya hisia;

"utovu mkubwa wa nidhamu" maana yake ni kitendo cha uasharati kisichokuwa cha kuingilia kingono na kinaweza kujumuisha utoaji wa mbegu za uzazi kwa kutumia mkono na kugusa au tabia isiyo ya kiungwana bila ya kugusa;

"madhara" maana yake ni madhara ya mwili, ugonjwa au ulemavu uwe wa kudumu au wa muda;

"hospitali" maana yake ni maeneo ya hospitali na yanajumuisha maeneo ya taasisi yoyote kwa ajili ya mapokezi na matibabu ya watu au matibabu ya watu yanayohitaji uangalizi wa kitabibu au huduma ya kuuguzwa;

"ngono haramu" maana yake ni maingiliano ya kingono baina ya watu ambao hawajaoana;

"shauri la kiMahakama" litajumuisha shauri lolote lililopo au lililopelekwa mbele ya Mahakama, baraza, tume ya uchunguzi, au mtu yeyote ambaye mbele yake ushahidi unaweza kuchukuliwa kwa kiapo;

“kwa kujua" likitumika pamoja na neno linalomaanisha uwasilishaji au utumiaji, litakuwa na maana ya kuonesha hali ya kufahamu tabia ya kitu hicho kilichotamkwa au kilichotumiwa;

"serikali za mitaa" maana yake ni serikali za mitaa zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria;

"kilema" maana yake ni uharibifu au ulemavu wa kudumu wa sehemu yoyote ya nje au ndani ya mwili, kiungo au viungo vya hisia;

"mwanamme" maana yake ni mtu mwanamme mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi;

"fedha" inajumuisha hati za kibenki, sarafu, hundi na hati ya idhini ya fedha, hundi na amri nyingine, idhini au maombi ya malipo ya fedha;

"usiku" au "wakati wa usiku" maana yake ni kipindi kati ya saa kumi na mbili na nusu jioni na saa kumi na mbili asubuhi;

"kosa" maana yake ni kufanya kitendo au kujaribu kufanya kitendo au kutokufanya kitendo, kinyume na sheria;

"silaha ya hatari" maana yake ni kitu kilichotengenezwa au kinachoweza kutumika kujeruhi, au kinachokusudiwa kutumika kwa matumizi hayo kwa mtu mwenyewe, au mtu mwengine;

"mtu" na "mmiliki" na maneno yanayofanana na hayo yanapotumika kuhusiana na mali yatajumuisha pia mashirika ya aina zote na jumuiya nyengine yoyote ya watu inayoweza kumiliki mali, na pia pale inapotumika hivyo itahusisha Serikali ya Zanzibar;

"mtu aliyeajiriwa kwenye utumishi wa umma" maana yake ni mtu yeyote anayefanya kazi katika mojawapo ya ofisi zifuatazo au ambaye anafanya shughuli za ofisi hizo, awe kama msaidizi au vinginevyo, yaani:

(a) ofisi yoyote ya umma ikijumuisha ofisi ya Rais wa Zanzibar, ofisi ambayo mamlaka ya uteuzi wa mtu au kumuondoa yapo kwa Rais, au yapo kwa Tume au yapo kwa mamlaka nyengine ya uteuzi;

(b) ofisi yoyote ambayo, mtu ameteuliwa au kuchaguliwa kwa mujibu wa sheria yoyote;

(c) ofisi yoyote ya umma, ambayo mamlaka ya uteuzi wa mtu au kumuondoa yapo kwa mtu au watu wenye dhamana ya ofisi ya aina yoyote iliyotajwa katika aya ya (a) au (b) za tafsiri hii;

(d) ofisi yoyote ya msuluhishi au muamuzi katika shauri au jambo lolote lililopelekwa kwa ajili ya usuluhishi kwa amri au uamuzi wa Mahakama, au kwa mujibu wa sheria yoyote; na pia itamaanisha watu wafuatao:

(i) mjumbe wa tume ya uchunguzi aliyeteuliwa chini au kwa mujibu wa sheria yoyote;

(ii) mtu yeyote aliyeajiriwa kutekeleza amri ya Mahakama;

(iii) watendaji wa Idara Maalum;

(iv) watendaji wanaofanya kazi katika idara yoyote ya Serikali;

(v) mtu anayekaimu kama kiongozi wa dini yoyote ambaye anatimiza wajibu wake katika kutangaza nia ya ndoa, au kufungisha ndoa, au kuweka kumbukumbu za usajili au utoaji wa cheti cha ndoa, kuzaliwa, ubatizo, kifo au mazishi;

(vi) mtendaji anaefanya kazi katika serikali za mitaa;

"kumiliki" "kuwa katika umiliki wa kitu" au "kumiliki kitu" kunajumuisha:

(a) sio tu kitu kuwa nacho yeye mwenyewe, bali pia kujua kuwa anamiliki kitu hicho au kujua kitu kinachohusika kipo kwa mtu mwengine, au kujua kitu hicho kipo sehemu nyengine yoyote inayomilikiwa au kukaliwa na yeye mwenyewe au vinginevyo kwa matumizi au manufaa yake yeye mwenyewe au ya mtu mwengine yeyote;

(b) iwapo kuna watu wawili au zaidi, na mmoja au zaidi ya mmoja kati yao kwa ufahamu na ridhaa ya wenzake anahodhi au kumiliki au wanahodhi au kumiliki, itachukuliwa kuwa kinahodhiwa au kumilikiwa na kila mmoja na wote kwa pamoja;

"mali" itajumuisha kila kitu chenye uhai au kisicho na uhai ambacho kinaweza kumilikiwa;

"umma" inamaanisha sio tu watu wote waliomo Zanzibar, lakini pia watu wanaoishi au wanaotumia sehemu yoyote husika, au idadi yoyote ya watu hao, na pia inajumuisha watu wengine ambao hawatambuliki kama watakavyoathiriwa na mwenendo unaohusika ambapo neno hilo linatumika;

"njia ya umma" unajumuisha njia kuu yoyote, mtaa, daraja, au njia nyengine ambayo kwa mujibu wa sheria inaruhusiwa kutumiwa na watu;

"sehemu ya umma" au "majengo ya umma" inajumuisha njia yoyote ya umma, jengo la umma, soko, eneo la wazi, mahali au chombo cha usafiri ambacho, kwa wakati huo watu wana haki au wanaruhusiwa kuingia bila ya sharti au kwa sharti la kulipa, na jengo lolote

au mahali ambapo kwa wakati huo hutumika kwa ajili ya mikutano ya hadhara au ya mikutano ya kidini; au mikusanyiko au kwenye Mahakama ya wazi;

"hadharani" pale linapotumika katika vitendo vilivyofanywa lina maana kuwa:

(a) kwamba vinatendwa mahali popote hadharani ambapo vinaweza kuonekana na mtu yeyote endapo mtu huyo yupo au hayupo hadharani; au

(b) kwamba vimefanywa mahali popote ambapo si hadharani lakini kuna uwezekano wa kuonekana na mtu yeyote aliyopo hadharani;

"udhalilishaji wa kingono" maana yake ni matendo yanayofanywa au maneno yanayosemwa yasiyo halali yanayoashiria ngono kuhusiana na mtu yeyote kwa ajili ya kujistarehesha au kwa lengo lolote lisilo halali;

"maingiliano ya kingono" ama kwa maumbile au kinyume na maumbile, kwa madhumuni ya kuthibitisha kosa la kingono, yatachukuliwa kuwa yamekamilika kwa kuingilia tu na sio kwa kukamilika kwa tendo la kuingilia na kutoa mbegu;

"kosa la kingono" maana yake ni kosa lolote lililoainishwa katika Sehemu ya Kumi na Tatu na vifungu 146, 147 na 148 vya Sheria hii;

"Idara Maalum" maana yake ni Idara Maalum iliyoanzishwa chini ya Katiba ya Zanzibar, 1984;

"wanandoa" maana yake ni mume au mke wa mtu;

"stempu inayotumika kwa madhumuni ya mapato ya umma" inajumuisha alama yoyote au stempu ya kitu kinachoonesha kutuma, kitu kilichoainishwa katika Sheria ya Posta, na hulipwa kwa mujibu wa vitu vinavyotumwa, na inajumuisha pia stempu zinazogandishwa na stempu zinazochapwa, muhuri wa moto au vyenginevyo vinavyoonesha katika bahasha, vifungashio, kadi za posta au kitu kingine na kitu kilichoainishwa katika Sheria ya Posta; na inajumuisha pia stempu zinazobandikwa kwenye hati au nyaraka nyengine zinazoonesha malipo ya kodi;

"uwasilishaji" inajumuisha kutumia au kujihusisha na, na kujaribu kutumia au kujihusisha na, na kujaribu kushawishi mtu yeyote kutumia, kujihusisha na au kufanya kulingana na kitu au jambo husika;

"dhamana yenye thamani" inajumuisha nyaraka yoyote ile ambayo ni mali ya mtu yeyote, na ambayo ni ushahidi wa umiliki wa mali yoyote au haki ya mtu yeyote kudai au kupokea mali yoyote na inajumuisha amri ya malipo ya fedha au hundi inayotolewa chini ya masharti ya Sheria ya Posta;

"chombo" inajumuisha meli, boti na kila aina ya chombo kinachotumika kusafiria majini, na inajumuisha chombo cha usafiri wa anga;

"mwanamke" maana yake ni mtu mwanamke mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi;

"Taasisi ya Wanawake au Watoto" maana yake ni Taasisi inayopokea na kutoa uangalizi wa wanawake au watoto, kwa namna yoyote ilivyoelezwa;

"jeraha" maana yake ni kuchanika au kutoboka ambako kumegawana au kumeweka mpenyo kunatoboa sehemu yoyote ya nje ya mwili, na sehemu yoyote ya nje ya mwili kwa madhumuni ya ufafanuzi huu ni ile ambayo inaweza kuguswa bila ya kuigawa, kuchanwa au kutobolewa ngozi nyengine;

"Sheria iliyoandikwa" maana yake ni Sheria ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na inajumuisha Amri, Taratibu, Kanuni na sheria ndogo zinazoandaliwa na kupitishwa chini ya mamlaka ya sheria yoyote.

## SEHEMU YA PILI
## ENEO LA MATUMIZI YA SHERIA

Mipaka ya Mamlaka za Mahakama.

**4.** Mamlaka ya Mahakama za Zanzibar kwa madhumuni ya Sheria hii ni sehemu yoyote ndani ya Zanzibar na sehemu yake ya bahari na makosa yatakayotendwa kwenye bahari kuu katika vyombo vilivyosajiliwa Zanzibar.

Sehemu ya makosa yanapote-ndwa ndani ya mamlaka na sehemu ya makosa yanapotendwa nje ya mamlaka.

**5.** Endapo kitendo ambacho, kimefanyika chote ndani ya mamlaka ya Mahakama, kitakuwa ni kosa dhidi ya Sheria hii, na endapo sehemu ya kitendo hicho kimefanyika nje ya mipaka ya mamlaka, mtu ambae amefanya sehemu ya kitendo hicho ndani ya mamlaka ya Mahakama anaweza kushtakiwa na kuhukumiwa chini ya Sheria hii kama vile amekifanya kitendo hicho chote ndani ya mamlaka ya Mahakama.

## SEHEMU YA TATU
## MISINGI YA JUMLA KUHUSU UWAJIBIKAJI WA KIJINAI

Kutokujua sheria.

**6.** Kutokujua sheria hakuwezi kuwa ni sababu ya kusamehewa kwa kutenda au kutokutenda kitendo ambacho kinaweza kuwa ni kosa, isipokuwa kama kujua sheria kwa mkosaji itaelezwa wazi kuwa ni kiini cha kosa.

Kudai haki kwa nia njema.

**7.** Mtu hatawajibika kwa kosa la kijinai linalohusika na mali iwapo kitendo kilichofanywa au kilichoachwa kufanywa na mtu huyo kuhusiana na mali kilifanywa kwa kudai haki kwa nia njema na bila ya nia ya kuiba.

Nia au dhamira.

**8.**-(1) Bila ya kuathiri masharti yaliyotajwa katika Sheria hii kuhusiana na vitendo vilivyofanywa au kuachwa kufanywa kwa uzembe, mtu hatawajibika kwa kosa la kijinai kwa kufanya au kuacha kufanya kitendo ambacho kimetokea bila ya idhini yake, au kwa tukio lililotokea kwa bahati mbaya.

(2) Isipokuwa pale ambapo nia ya kusababisha tukio fulani imeelezwa kuwa ni kiini kinachopelekea kufanyika kwa kosa, kwa kosa zima au sehemu ya kosa, kwa kutenda au kutotenda, matokeo yaliyokusudiwa kutokea kwa kutenda au kutokutenda hayatahesabiwa.

(3) Isipokuwa kama imetamkwa vyenginevyo, dhamira ambayo mtu imemshawishi kutenda au kuacha kutenda kitendo, au imemfanya kukusudia, haitamtoa katika kuhusika kwake kwenye makosa ya kijinai.

Dhana isiyo ya kweli.

**9.**-(1) Mtu ambaye anaetenda au kuacha kutenda kitendo kwa nia njema na kwa sababu za msingi, lakini kwa kukosea akaamini kuwepo kwa hali yoyote ya vitu, hatawajibika kwa kiwango kikubwa zaidi kwa kosa la kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda iwapo hali halisi ya vitu alivyoviamini kuwepo vingekuwa kama alivyoamini.

(2) Kutumika kwa msingi huu kunaweza kuondolewa kwa maelezo au masharti ya wazi au yasiyowazi kwenye sheria inayohusiana na jambo husika.

Kuchukuliwa kuwa na akili timamu.

**10.** Mtu atachukuliwa kuwa ana akili timamu, na atachukuliwa kuwa ana akili timamu wakati wowote linapokuja suala la akili timamu wa tukio la jinai, mpaka pale itakapothibitishwa vyenginevyo.

Ugonjwa wa akili.

**11.**-(1) Mtu hatawajibika kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda iwapo wakati wa kutenda kitendo hicho au kuacha kutenda alikuwa katika hali ya ugonjwa wowote unaoathiri akili yake:

(a) kwa kutoweza kujua kitu anachokitenda;

(b) kwa kutoweza kutambua kwamba hapaswi kutenda au kuacha kutenda jambo husika; au

(c) kwa kutokuwa na uwezo wa kuzuia kutenda au kuacha kutenda.

(2) Mtu atachukuliwa kuwa ametenda kosa la jinai kwa kutenda au kuacha kutenda kitendo ingawaje akili yake itakuwa imeathiriwa na ugonjwa, kama ugonjwa huo haukumletea mojawapo ya madhara yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kwa kutenda huko au kuacha kutenda.

Ulevi.

**12.**-(1) Isipokuwa kama ilivyoelezwa katika kifungu hiki, kulewa hakutachukuliwa kuwa ni utetezi katika kosa lolote la jinai.

(2) Kulewa kutakubaliwa kuwa utetezi kwa shitaka lolote la jinai, iwapo tu kwa sababu ya kulewa huko, mtu anayeshtakiwa wakati wa kutenda au kuacha kutenda kosa analoshtakiwa alikuwa hatambui kutenda huko au kuacha kutenda ni kosa au alikuwa hatambui atendalo na:

(a) hali ya kulewa huko ilisababishwa bila ya hiari yake kwa kitendo cha ubaya au uzembe wa mtu mwengine; au

(b) kwa sababu ya kulewa, mtu aliyeshitakiwa alikuwa ana matatizo ya akili, ya muda mfupi au vyenginevyo, wakati wa kutenda huko au kuacha kutenda.

(3) Endapo utetezi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki utathibitika, na kama kesi itaangukia chini ya aya ya (a) ya kifungu kidogo hicho, mshtakiwa ataachiwa huru, na kama kesi itaangukia kwenye aya ya (b) ya kifungu kidogo hicho, masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai kuhusu ugonjwa wa akili yatatumika.

(4) Kulewa kutatiliwa maanani kwa madhumuni ya kuamua iwapo mtu aliyeshtakiwa alifanya kosa kwa makusudi maalum au vinginevyo, ambapo kama yasingekuwepo makusudi hayo asingelichukuliwa kuwa ni mkosa.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "ulevi" utachukuliwa kujumuisha hali iliyosababishwa na dawa za kulevya, dawa, au dawa zinazoathiri akili.

Umri mdogo.

**13.**-(1) Mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na mbili anachukuliwa kuwa hawezi kuwajibika kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda.

(2) Mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nne hatawajibika kijinai kwa kutenda au kuacha kutenda, isipokuwa kama itathibitishwa kwamba wakati wa kutenda au kuacha kutenda kitendo hicho alikuwa na uwezo wa kujua kwamba hapaswi kukitenda au kuacha kukitenda.

(3) Mwanamme mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nne atachukuliwa kuwa hawezi kufanya tendo la kujamiiana.

Maafisa wa Mahakama.

**14.** Isipokuwa kama itaelezewa kwenye Sheria hii, Afisa wa Mahakama hatowajibika kijinai kwa jambo lolote alilofanya au aliloacha kulifanya wakati wa utekelezaji wa kazi zake za kimahakama, ijapokuwa jambo alilolifanya liko nje ya mamlaka yake ya kimahakama au ijapokuwa analazimika kufanya kitendo ambacho hakukifanya.

Kushurutishwa.

**15.** Mtu hatawajibika kijinai kwa kosa endapo kosa hilo limefanywa na wakosaji wawili au zaidi, na iwapo kitendo hicho kimetendwa au kimeachwa kutendwa kwa sababu tu kwa kipindi chote ambacho kitendo kimetendeka au kimeachwa kutendwa mtu huyo amelazimishwa kukitenda au kuacha kukitenda kwa vitisho kutoka kwa mkosaji mwengine au wakosaji wengine kwa kutishia kumuua papo hapo au kumdhuru madhara makubwa ya kimwili iwapo atakataa, lakini vitisho vya kumdhuru hapo baadaye havitachukuliwa kuwa ni utetezi wa kosa lolote.

Haki ya kujilinda.

**16.**-(1) Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii, kila mtu anayo haki ya:

(a) kujilinda yeye mwenyewe binafsi au kumlinda mtu mwengine dhidi ya kitendo chochote kisicho halali au shambulio au utumiaji nguvu dhidi ya mwili; au

(b) kulinda mali yake au mali yoyote iliyo chini ya umiliki wake kihalali, himaya yake, au chini ya uangalizi wake au mali ya mtu mwengine yeyote dhidi ya kuchukuliwa isivyo halali au kuharibiwa au kuvamiwa

(2) Katika kifungu hiki, neno "mali ya mtu mwingine yeyote" itajumuisha mali yoyote inayomilikiwa na Serikali au Shirika la Umma au ya mwajiri au mali inayomilikiwa kwa pamoja na jumuiya ya watu kama chama cha ushirika au kijiji.

Matumizi ya nguvu katika kujilinda.

**17.**-(1) Katika kutumia haki ya kujilinda mwenyewe au kumlinda mtu mwengine au kulinda mali, mtu atatakiwa tu kutumia nguvu za kiasi zinazohitajika katika ulinzi huo.

(2) Mtu atawajibika kijinai kwa kosa lolote linalotokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda au katika kumlinda mtu mwengine au katika kulinda mali.

(3) Mtu yeyote atakayesababisha kifo cha mtu mwengine kutokana na matumizi ya nguvu kupita kiasi katika kujilinda, atakuwa ametenda kosa la kuua bila kukusudia.

Pale haki ya kujilinda inapotumika na kusababisha kifo.

**18.**-(1) Haki ya kujilinda au kumlinda mtu mwengine au kulinda mali itatumika kwa mtu yeyote ambaye, katika kutumia haki hiyo, atasababisha kifo au madhara makubwa kwa mtu mwengine na mtu atakayefanya hivyo na amefanya kwa nia njema huku akiamini alikuwa na sababu ya msingi kwamba kitendo chake kilistahili ili kuokoa maisha yake, kiungo chochote cha mwili wake au kuokoa maisha au kiungo chake au maisha au kiungo cha mtu mwengine au mali, katika hali ambayo:

(a) kitendo halali kilikuwa katika hali ambayo kingeweza kusababisha hofu ya kifo chake mwenyewe au kifo cha mtu mwengine ambacho kingeweza kuwa ni matokeo ya kitendo hicho;

(b) kitendo halali kilikuwa katika hali ambayo kingeweza kusababisha hofu ya madhara makubwa kwenye mwili wake au mwili wa mtu mwengine madhara makubwa ambayo yangeweza kuwa ni matokeo ya kitendo hicho;

(c) kitendo ambacho ni kinyume cha sheria kinachofanyika kwa nia ya kubaka au kunajisi au kwa kosa la kuingilia kinyume na maumbile;

(d) kitendo ambacho ni kinyume cha sheria kinachofanyika kwa nia ya kuteka nyara au kutorosha; au

(e) kitendo ambacho ni kinyume cha sheria kwa kuvunja na kuingia usiku katika jengo la makaazi kwa madhumuni ya kutenda kosa, unyang'anyi, kuchoma moto au kosa lolote la jinai, lenye kuhatarisha maisha au mali.

(2) Iwapo, katika kutumia haki ya kujilinda kwa mujibu wa Sheria hii, mtu anayetumia haki hii yupo katika mazingira ambayo hawezi kujilinda kikamilifu bila ya kuhatarisha au kuleta madhara kwa mtu asiye na hatia au mali, haki yake ya kujilinda haitaathiriwa na hatari inayoweza kutokea.

Kutumia nguvu katika kukamata.

**19.** Iwapo mtu yeyote anashtakiwa kwa kosa la jinai linalotokana na kumkamata au kujaribu kumkamata mtu, ambaye kwa kutumia nguvu anapinga kukamatwa au anajaribu kuepuka kukamatwa, Mahakama katika kutafakari iwapo njia zilizotumiwa zilikuwa zinafaa au kiasi cha nguvu kilichotumiwa ili kumkamata mtu huyo kilikuwa kinafaa, itazingatia uzito wa kosa ambalo limefanywa au lilikuwa linafanywa na mtu huyo na mazingira ambayo kosa hilo lilifanywa au lilikuwa linafanywa na mtu huyo.

Shurutisho kutoka kwa mume.

**20.** Mwanamke aliyeolewa hawezi kuepuka kuwajibika kijinai kwa kutenda kosa au kuacha kutenda kwa sababu tu kutenda huko au kuacha kutenda kumefanyika mbele ya mume wake; lakini kwenye shtaka dhidi ya mke kwa kosa lolote lisilokuwa la uhaini au la mauaji, itakuwa ni utetezi mzuri kuthibitisha kwamba kosa hilo lilifanywa mbele ya mume wake na kwa kushurutishwa na mume wake.

Mtu kutoku-adhibiwa mara mbili kwa kosa lilelile.

**21.** Mtu hatoadhibiwa mara mbili, ama chini ya masharti ya Sheria hii au chini ya masharti ya sheria nyingine yoyote ile, kwa kosa lile lile, isipokuwa katika kesi inayohusu kutenda au kuacha kutenda kitendo ambacho kimesababisha kifo cha mtu mwengine, anaweza kutiwa hatiani kwa kusababisha kifo hicho, bila ya kujali kwamba tayari alishatiwa hatiani kwa kosa jengine lililofanywa kwa kutenda au kuacha kutenda huko.

## SEHEMU YA NNE
## WASHIRIKI KWENYE MAKOSA

Wakosaji wakuu.

**22.** Pale ambapo kosa limetendeka, kila mmoja kati ya watu wafuatao atachukuliwa kwamba ameshiriki katika kutenda kosa hilo na atakuwa ni mkosa, na anaweza kushtakiwa kwa kutenda kosa hilo, yaani:

(a) mtu ambaye anafanya kitendo au ambaye ameacha kufanya kitendo ambacho kinapelekea kufanya kosa;

(b) mtu ambaye anafanya kitendo au anaacha kufanya kitendo kwa madhumuni ya kumuwezesha au kumsaidia mtu mwengine kutenda kosa;

(c) mtu ambaye anamsaidia au anamshawishi mtu mwengine kutenda kosa;

(d) mtu ambaye anamshauri au anamshirikisha mtu mwengine yeyote kutenda kosa.

Makosa yanayotendwa na wakosaji walioshi-rikiana katika kutekeleza kusudio moja.

**23.** Pale watu wawili au zaidi wanakuwa na nia moja ya kutekeleza kusudio lisilo halali kwa pamoja, na katika kutekeleza kusudio hilo, kosa linatendeka kwa namna ambayo kutendeka kwa kosa hilo kulikuwa ni matokeo ya kutekelezwa kwa kusudio hilo, kila mmoja wao atachukuliwa kuwa ametenda kosa hilo.

Kumshauri mwengine kutenda kosa.

**24.**-(1) Pale mtu anamshauri mtu mwengine kutenda kosa, na mtu aliyeshauriwa akatenda kosa baada ya ushauri huo, haijalishi kama kosa alilolitenda ni sawa na lile

aliloshauriwa au ni tofauti, au kosa hilo amelitenda katika namna aliyoshauriwa au katika namna tofauti, vyovyote itakavyokuwa almuradi mambo yanayotengeneza kosa lililotendwa ni matokeo halisi ya utekelezaji wa ushauri uliotolewa.

(2) Katika hali yoyote iliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu aliyetoa ushauri atachukuliwa kwamba amemshauri mtu mwengine kutenda kosa ambalo amelitenda.

## SEHEMU YA TANO
## ADHABU

Aina mbali mbali za adhabu.

**25.** Adhabu zifuatazo zinaweza kutolewa na Mahakama:

(a) kifo;

(b) kifungo;

(c) kuitumikia jamii;

(d) faini;

(e) kunyang'anywa mali;

(f) kulipa gharama;

(g) kulipa fidia;

(h) kuweka dhamana kwa ajili ya kutunza amani na kuwa na tabia njema, au kwa kuhudhuria kupewa hukumu;

(i) uangalizi wa polisi;

(j) kuachiwa kwa masharti chini ya sheria inayohusu Uangalizi wa Wahalifu;

(k) kuifuta au kuisitisha leseni ya udereva chini ya Sheria ya Usalama Barabarani;

(l) amri inayotolewa chini ya Sheria ya Watoto; na

(m) adhabu nyengine yoyote inayotolewa na Sheria hii au sheria nyengine yoyote;

Adhabu ya jumla.

**26.**-(1) Pale katika Sheria hii hakuna adhabu iliyotamkwa kwa kosa lolote, kosa hilo litaadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka miwili au kulipa faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au vyote viwili kwa pamoja.

(2) Mahakama, badala ya adhabu iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, inaweza kutoa adhabu ya kuitumikia jamii kwa kipindi cha miezi sita au kwa kipindi chengine chochote kama Mahakama itakavyoamua.

## SEHEMU YA SITA
## UHAINI NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA SERIKALI

Uhaini.

**27.** Mtu ambae anapanga, anaanzisha, anazusha au anakusudia tendo lolote, jambo au dhana na kueleza, kutamka au kutangaza mpango, kuanzisha, kuzusha au kukusudia huko kwa kuchapisha chapisho lolote au maandishi au kwa tendo lolote la dhahiri au kwa kutenda tendo lolote ambalo, linakusudia kuleta au kusababisha kuondosha au kuleta mabadiliko ya Serikali ya Zanzibar kinyume na utaratibu wa Katiba ya Zanzibar, atakuwa ni mkosa wa kosa la uhaini na atapewa adhabu ya kifo.

Kuingia Zanzibar kwa nia ya kupanga dhidi ya Mapinduzi.

**28.** Mtu anaeingia Zanzibar kwa nia ya kupanga harakati za kupinga Mapinduzi dhidi ya Serikali au kwa nia ya kuchochea wengine kupanga harakati hizo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifo.

Kuchochea uvamizi.

**29.** Mtu anaemchochea mgeni kuivamia sehemu yoyote au sehemu yote ya eneo la Zanzibar kwa nguvu za kijeshi, atakuwa ni mkosa wa kosa la uhaini na atapewa adhabu ya kifo.

Kuficha uhaini.

**30.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anaficha uhaini baada ya kutokea; au

(b) anafahamu kuwa mtu yeyote ana nia ya kutenda kosa la uhaini au kufanya uhaini na hakutoa taarifa kwa njia yoyote kwa Rais wa Zanzibar, Waziri wa Serikali ya Zanzibar, Wakuu wa Idara Maalum, Afisa Tawala, Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Hakimu, au Afisa dhamana wa kituo cha polisi, au hakufanya jitihada za kuzuia kufanyika kwa kosa,

atakuwa ni mkosa wa kosa la kuficha uhaini na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Makosa yanayohusiana na uhaini.

**31.** Mtu yeyote ambae ametia nia ya kufanya moja kati ya makusudio yafuatayo, yaani:

(a) kumuondoa mtu kwa nguvu za kijeshi kutoka kwenye Ofisi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi au kuvamia kwa nguvu za kijeshi Ofisi na Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa lengo la kuwazuia wajumbe wa Baraza hilo kutekeleza mamlaka

na majukumu yao, au kuvamia vyombo vya habari **vya Serikali** au kuwakamata mateka maafisa wa Mahakama au watumishi wa umma kwa lengo la kuzorotesha na kuzuia utekelezaji wa kazi na majukumu ya Serikali yaliyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar.

(b) kuanzisha vita dhidi ya Serikali ya Zanzibar ndani ya sehemu yoyote ya Zanzibar, au ndani ya nchi yoyote kwa dhamira ya kumlazimisha au kumzuia kwa kumlazimisha Rais wa Zanzibar au mhimili wowote mwengine au Idara ya Serikali ya Zanzibar kubadilisha hatua, sera, maamuzi au ushauri, au kwa dhamira ya kushinikiza kwa nguvu au kuzuia, au kwa dhamira ya kutishia au kuogopesha Baraza la kutunga sheria au mamlaka ya kutunga sheria ya Zanzibar;

(c) kumchochea mgeni yoyote kufanya uvamizi wa kijeshi katika sehemu yoyote au eneo lote la Zanzibar;

(d) kumnyima Rais wa Zanzibar mamlaka ya juu katika Zanzibar; au

(e) kuanzisha vita dhidi ya Zanzibar,

na kuionesha nia hiyo kwa kitendo cha dhahiri, au kwa kuchapisha chapisho lolote au maandishi, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Ukomo wa kuendesha kesi ya uhaini.

**32.**-(1) Mtu hataweza kushtakiwa kwa kosa la uhaini au kwa makosa yaliyoainishwa kwenye vifungu vya 30 na 31, isipokuwa kwa shtaka lililoanzishwa ndani ya miaka miwili baada ya kosa kutendeka.

(2) Wala mtu hataweza kushtakiwa kwa uhaini, au kwa kosa lolote miongoni mwa makosa hayo, na kutiwa hatiani, isipokuwa endapo atakiri mwenyewe au kwa ushahidi wa mashahidi wawili katika mahakama ya wazi wa angalau tendo moja la dhahiri la aina ya uhaini au la kosa analotuhumiwa nalo, au kwa ushahidi wa shahidi mmoja wa tendo moja la dhahiri, na shahidi mmoja mwengine kwa tendo jengine la dhahiri la aina hiyo hiyo ya uhaini au kosa analotuhumiwa nalo.

(3) Kifungu hiki hakitatumika kwa kesi ambazo tendo la dhahiri la uhaini linalotuhumiwa ni la kumuua Rais wa Zanzibar au jaribio la moja kwa moja la kuhatarisha maisha au kumdhuru Rais wa Zanzibar yeye mwenyewe.

Kuchochea uasi.

**33.** Mtu yeyote ambaye, kwa kushauriwa anajaribu kutimiza moja kati ya makusudio yafuatayo, yaani:

(a) kumshawishi afisa yeyote wa Jeshi, Idara Maalumu au Askari Polisi aache wajibu na utii wake juu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; au

(b) kuwachochea watu wengine wowote wa aina hiyo kutenda kitendo cha uasi au kutenda kitendo chochote cha usaliti au kitendo cha uasi; au

(c) kuwachochea watu wengine wowote wa aina hiyo kufanya au kujitahidi kufanya mkusanyiko wa uasi,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuwasaidia Wanajeshi au Maafisa wa Polisi katika vitendo vya uasi.

**34.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamsaidia, anamshawishi au anashiriki katika tendo lolote la uasi; au

(b) anashawishi uchochezi au kutokutii amri yoyote halali iliyotolewa na afisa wa ngazi ya juu, au afisa wa ngazi ya chini, au askari wa kawaida wa Jeshi la Ulinzi, Polisi au Idara Maalum,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Kuwashawishi Wanajeshi au Maofisa wa Polisi kutoroka.

**35.** Mtu yeyote ambaye kwa njia yoyote ile, moja kwa moja au vyenginevyo:

(a) anamuwezesha au anamshawishi au anajaribu kumuwezesha au kumshawishi atoroke; au

(b) anamsaidia, anamshawishi au ni mshiriki katika kumtorosha; au

(c) kutokana na kuamini kwamba ni mtoro, anamficha au anasaidia katika kujificha,

afisa yeyote wa ngazi ya chini au askari wa kawaida wa Jeshi la Ulinzi, au Polisi, au Idara Maalum, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini hakitozidi miaka kumi.

Kusaidia kwa kujua mateka wa vita kutoroka.

**36.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua na kufahamu anamsaidia adui wa kigeni wa watu na Serikali ya Zanzibar, ambaye ni mateka wa kivita ndani ya Zanzibar, ikiwa mateka husika yupo ndani ya kizuizi cha gereza au mahali pengine, au yupo huru kutokana na msamaha, kutoroka kutoka gerezani au kizuizini, au ikiwa yupo huru kwa msamaha kutoroka kutoka Zanzibar, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuruhusu kwa uzembe mateka wa vita kutoroka.

**37.** Mtu ambaye kwa uzembe na bila halali anaruhusu kutoroka kwa mtu aliyetajwa kwenye kifungu cha 36 cha Sheria hii, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Tafsiri ya kitendo cha dhahiri.

**38.** Kwa kosa lolote kati ya yaliyotajwa katika Sehemu hii, pale ambapo kubainika kwa kitendo cha dhahiri cha nia ya kutekeleza kusudio lolote ni kiini cha kosa, kitendo chochote cha kula njama na mtu mwengine ili kutekeleza kusudio hilo, na kila kitendo kinachofanywa katika kufikia kusudio hilo kinachofanywa na mtu yoyote miongoni mwa waliokula njama, kitachukuliwa kuwa ni kitendo cha dhahiri kinachobainisha nia.

Viapo visivyo halali ili kutenda makosa makubwa.

**39.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anasimamia, au anakuwepo na anakubali kusimamia kiapo chochote, au kujihusisha katika suala lenye sura ya kiapo, kinachombana anayekula kiapo kutenda kosa lenye adhabu ya kifo; au

(b) anakula kiapo au anajihusisha katika suala lenye sura ya kiapo, bila kulazimishwa kufanya hivyo,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Viapo vyengine visivyo halali ili kutenda makosa.

**40.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anasimamia, au anakuwepo na anakubali kusimamia kiapo chochote, au kujihusisha katika suala lenye sura ya kiapo, kinachombana anayekula kiapo kutenda moja kati ya haya yafuatayo:

(i) kujihusisha na vitendo vyovyote vya uasi au uchochezi;

(ii) kutenda kosa lolote ambalo adhabu yake sio kifo;

(iii) kuvuruga amani ya jamii;

(iv) kuwa mwanachama wa ushirika, jumuiya au shirikisho linaloundwa kwa lengo la kufanya jambo lolote lililotajwa katika aya ndogo ya (i) hadi aya ya (iii) ya aya hii;

(v) kutii amri au maelekezo kutoka katika kamati yoyote au kikundi cha watu ambacho hakikuanzishwa kihalali, au kutoka kwa kiongozi au kamanda au mtu mwengine yeyote asiye na mamlaka ya kisheria kuhusu jambo husika;

(vi) kutokutoa taarifa au ushahidi dhidi ya mwana ushirika, mwanachama wa shirikisho au mtu mwengine yeyote; au

(vii) kutokuonesha au kutokubainisha ushirika wowote usio halali, jumuiya au shirikisho, au kitendo chochote kisicho halali kilichofanywa au kitakachofanywa, au kiapo chochote kisicho

halali au suala lenye sura ya kiapo ambalo linaweza kuwa limesimamiwa au limewasilishwa au limetekelezwa na yeye mwenyewe au mtu mwengine yoyote, au maana ya kiapo hicho au suala lenye sura ya kiapo;

(b) anakula kiapo hicho au anajihusisha katika suala lenye sura ya kiapo, bila kulazimishwa kufanya hivyo,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kwa kiasi gani kulazimishwa kunakuwa utetezi.

**41.** Mtu ambaye anakula kiapo au anajihusisha na suala lenye sura ya kiapo kama ilivyotajwa katika kifungu cha 39 na 40 vya Sheria hii hawezi kutoa utetezi kuwa alilazimishwa kufanya hivyo, isipokuwa ndani ya siku kumi na nne baada ya kula kiapo, au, iwapo amezuiwa kwa nguvu au maradhi, ndani ya siku kumi na nne baada ya kumalizika kuzuiwa huko atatamka kwa taarifa ya kiapo mbele ya hakimu, au, iwapo yupo katika utumishi wa Jeshi la Ulinzi, Idara Maalumu au Jeshi la Polisi, ama kwa taarifa hiyo au kwa taarifa aliyoitoa kwa wakuu wake wa kazi, yote anayoyajua kuhusu jambo hilo ikijumuisha mtu au watu ambao wamemlisha kiapo na ambao walikuwepo na mahala na muda ambao kiapo au suala lenye sura ya kiapo limesimamiwa au limetekelezwa.

Mafunzo ya kijeshi yasiyo halali.

**42.**-(1) Mtu ambaye:

(a) bila ya ruhusa ya Rais wa Zanzibar anafundisha au anatoa mafunzo ya kijeshi kwa mtu mwingine yeyote kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kijeshi, mwenendo, au kazi za kivita; au

(b) anahudhuria kwenye mkutano wowote au mkusanyiko wa watu, uliofanywa bila ruhusa ya Rais wa Zanzibar, kwa lengo la kufundisha au kutoa mafunzo ya kijeshi kwa watu wengine wowote kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kijeshi, mwenendo au kazi za kivita;

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(2) Mtu yeyote ambaye, katika mkutano au mkusanyiko wowote uliofanywa bila ya ruhusa ya Rais wa Zanzibar, anafundishwa au anapewa mafunzo ya kijeshi kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kijeshi, mwenendo, au kazi za kivita, au anahudhuria kwenye mkutano wowote au mkusanyiko wa watu, uliofanywa kwa lengo la kufundishwa au kupewa mafunzo ya kijeshi, watu wengine wowote kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kijeshi, mwenendo au kazi za kivita, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kuchapisha taarifa za uongo.

**43.**-(1) Mtu yoyote ambaye anachapisha au anatoa taarifa za uongo, uvumi, au ripoti ambayo kikawaida inapelekea kusababisha hofu na mshituko kwa jamii au inavuruga amani ya jamii, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka miwili.

(2) Itakuwa ni utetezi kwa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kama mshtakiwa atathibitisha kwamba, kabla ya kuchapisha alichukua hatua za kuhakiki usahihi wa taarifa hiyo, uvumi au ripoti zilizomuongoza kuamini kwamba taarifa hiyo ni ya kweli.

Kuchochea kufanya ghasia.

**44.**-(1) Mtu yeyote ambaye, bila ya dharura ya kisheria, amechapa, amesambaza au katika mkusanyiko wowote ametoa kauli au maneno yanayoashiria au yanayomaanisha kwamba itakuwa ni lazima au itahitajika:

(a) kufanya kitendo kinachokusudiwa kuleta kifo au madhara ya kimwili kwa mtu au tabaka lolote au jamii ya watu;

(b) kufanya kitendo kinachokusudiwa kutokomeza au kuharibu mali,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka miwili.

(2) Mtu hatoshtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "mkusanyiko" maana yake ni mkusanyiko wa watu watatu au zaidi.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA YANAYOATHIRI MAHUSIANO NA NCHI ZA NJE NA UTULIVU WA NJE

Kukashifu.

**45.** Mtu yeyote ambaye, bila ya sababu au dharura ambayo inakubalika katika shauri la kumkashifu mtu binafsi, amesambaza kitu chochote kinachokusudiwa kusomwa, au alama yoyote au kiwakilishi chochote kinachoonekana, kwa kukusudia kushusha hadhi, kutukana au kumfanya achukiwe au adharauliwe kiongozi yeyote, balozi, au mgeni mwenye kuheshimika kwa nia ya kuvuruga amani na urafiki baina ya Zanzibar na nchi ambayo kiongozi, balozi, au mgeni mwenye kuheshimika anatoka, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Uandikishaji wa wanajeshi wa Kigeni.

**46.**-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa iwapo atatenda mojawapo ya matendo yafuatayo bila ya ruhusa ya Rais iliyowekwa muhuri wa Serikali, au iliyoainishwa na kanuni au maelekezo muafaka ya kiutawala, yaani:

(a) atakayetayarisha au kuwezesha msafara wowote wa askari wa majini au msafara wa kijeshi kwenda kushambulia tawala za dola yoyote iliyo rafiki au atakayeshughulika na maandalizi au uwezeshaji, au kusaidia katika hayo, au kuajiriwa katika cheo chochote katika msafara huo;

(b) akiwa ni raia wa Tanzania, anakubali au anafanya makubaliano ya kukubali kazi yoyote au kujihusisha na shughuli yoyote ya kijeshi au utumishi wa uaskari wa majini wa dola yoyote ya kigeni ambayo iko katika vita na dola yoyote rafiki, au, akiwa raia wa Tanzania au sio raia, anamshawishi mtu mwengine yoyote kukubali au kufanya makubaliano ya kukubali kazi yoyote au kujishughulisha na shughuli yoyote ya kijeshi au utumishi wa uaskari wa majini wa dola yoyote ya kigeni kama ilivyokwishaelezwa;

(c) akiwa ni raia wa Tanzania, anatoroka au anaingia katika chombo chochote kwa dhamira ya kutoroka Zanzibar, kwa nia ya kukubali kazi yoyote au kujihusisha na shughuli yoyote ya kijeshi au utumishi wa uaskari wa majini wa dola yoyote ya kigeni ambayo iko katika vita na dola yoyote rafiki, au akiwa raia wa Tanzania au sio raia, anamshawishi mtu mwengine yoyote kutoroka au kuingia katika chombo chochote kwa dhamira ya kutoroka Zanzibar kwa nia kama hiyo;

(d) akiwa ni nahodha au mmiliki wa chombo, iwapo anajua anamchukua katika chombo, au anajihusisha katika kumchukua katika chombo, au anae katika chombo hicho mtu yeyote ambaye hakuandikishwa kisheria; au

(e) akiwa, ana nia au anajua, au ana sababu za kuamini kwamba chombo hicho kitatumika katika jeshi au utumishi wa uaskari wa majini wa dola yoyote ya kigeni iliyo kwenye vita na dola yoyoye rafiki, anaunda, anaingia katika makubaliano ya kuunda, anawezesha kuundwa, anaweka vifaa, anatuma, au anawezesha au anaruhusu kutumwa chombo chochote au vitu au anatoa kazi kwa chombo chochote.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu anayeunda, anaewezesha kuundwa, au anaeweka vifaa katika chombo kwa namna mojawapo katika hizo zilizotajwa, kwa kutimiza mkataba uliofanywa kabla ya kuanza kwa vita hivyo kama ilivyoelezwa, hatapewa adhabu yoyote miongoni mwa adhabu zilizoainishwa katika kifungu hiki zinazohusiana na uundaji huo au uwekaji vifaa iwapo:

(a) baada ya Rais wa Zanzibar kutoa tangazo la kutofungamana na upande wowote katika vita, mtu huyo atatoa notisi mara moja kwa

Rais wa Zanzibar au Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar kwamba anaunda, anawezesha kuundwa, au anaweka vifaa katika chombo hicho, na atatoa maelezo mahsusi ya mkataba na mambo yoyote yanayohusiana nayo, au yaliyofanywa au yatakayofanywa chini ya mkataba kama itakavyohitajika na Rais wa Zanzibar au Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar; na

(b) mtu huyo anatoa dhamana na anachukua au kuruhusu kuchukuliwa hatua nyenginezo husika, kama zipo, kama Rais wa Zanzibar au Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Zanzibar atakavyoeleza kwa ajili ya kuhakikisha kwamba chombo hicho hakitapelekwa, hakitawasilishwa au hakitaondoshwa bila ya ruhusa ya Rais wa Zanzibar hadi pale vita hivyo vitakapomalizika.

Uharamia.

**47.-** (1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anatenda kitendo kisicho halali cha kutumia nguvu dhidi ya, au kuikamata meli au chombo kilichosajiliwa Zanzibar au mahala pengine popote au dhidi ya watu au mali iliyo ndani ya meli hiyo au chombo;

(b) anatenda kitendo kisicho halali cha kutumia nguvu dhidi ya, au kuikamata meli au chombo au dhidi ya mtu yeyote au mali iliyo ndani ya meli hiyo au chombo;

(c) kwa ridhaa yake anashiriki katika shughuli za meli, chombo au ndege kwa madhumuni ya kufanya kitendo kilichoainishwa katika aya ya (a) au (b); au

(d) kushawishi au kuwezesha kwa makusudi kitendo chochote kilichoelezwa katika aya ya (a) au (b) au (c),

atakuwa ni mkosa kwa kosa la "uharamia" na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(2) Mashtaka chini ya kifungu hiki hayataanzishwa bila idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

## SEHEMU YA NANE
## MIKUSANYIKO ISIYO HALALI, GHASIA NA MAKOSA MENGINE DHIDI YA UTULIVU WA JAMII

Maana ya jumuiya na jumuiya isiyo halali.

**48.**-(1) Jumuiya inajumuisha mjumuiko wa watu kumi au zaidi, inawezekana kuwa jumuiya inajulikana kwa jina au vinginevyo.

(2) Jumuiya isiyo halali ni:

(a) endapo itaundwa kwa moja kati ya makusudio yafuatayo:

(i) kuanzisha vita au kuhamasisha au kusaidia mtu kuanzisha vita dhidi ya Serikali au wakaazi wa sehemu yoyote ya Zanzibar;

(ii) kuua au kudhuru au kuchochea kuua au kudhuru mtu yeyote;

(iii) kuteketeza au kudhuru au kuchochea uteketezaji au madhara ya mali;

(iv) kuondosha au kuendeleza uondoshaji wa Serikali au watendaji wake;

(v) kufanya au kuchochea kufanyika kwa matendo ya kutumia nguvu au vitisho;

(vi) kuingilia, kupinga, au kuchochea kuingilia au kupinga utekelezaji wa sheria; au

(vii) kuvuruga au kuchochea katika kuvuruga amani na utulivu katika sehemu yoyote ya Zanzibar;

(b) endapo itatangazwa kwa amri ya Rais wa Zanzibar kwamba ni jumuiya hatari kwa Serikali.

Kuwa mwanachama au kuongoza jumuiya isiyo halali.

**49.**-(1) Mtu ambae anaongoza au anasaidia katika kuongoza jumuiya isiyo halali atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuwa mwanachama wa jumuiya isiyo halali na atapewa adhabu ya faini ya Shilingi Milioni Moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

Masharti yanayohusiana na uendeshaji wa mashtaka chini ya kifungu cha 49.

**50.**-(1) Uendeshaji mashtaka kwa kosa chini ya kifungu cha 49 cha Sheria hii, hautaanzishwa isipokuwa kwa ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

(2) Katika uendeshaji wa mashtaka chini ya kifungu cha 49 cha Sheria hii, haitokuwa lazima kuthibitisha kwamba jumuiya ilikuwa ina wajumbe kumi au zaidi, ila itatosha kuthibitisha kuwepo kwa mjumuiko wa watu, na jukumu litakuwa kwa anaeshtakiwa kuthibitisha kwamba idadi ya wajumbe wa mjumuiko huo haikufikia watu kumi.

(3) Mtu ambaye anahudhuria katika mkutano wa jumuiya isiyo halali atachukuliwa, hadi pale na isipokuwa itakapothibitika vyenginevyo, kuwa ni mwanachama wa jumuiya hiyo.

(4) Mtu ambae anamiliki au ana katika hifadhi yake au katika udhibiti wake nembo yoyote, mabango, silaha, vitabu, karatasi, nyaraka, au mali nyengine za jumuiya isiyo halali, au anavaa nembo yoyote, au anatambulika kwa alama yoyote ya jumuiya, atachukuliwa, isipokuwa kama itathibitika vyenginevyo, kuwa ni mwanachama wa jumuiya hiyo.

Uwezo wa kuingia.

**51.**-(1) Afisa anaeshughulikia amani, na afisa wa polisi aliyeidhinishwa kwa maandishi na afisa anayeshughulikia amani, anaweza kwa msaada au bila ya msaada kuingia katika nyumba au jengo lolote au mahala popote ambapo ana kila sababu ya kuamini kwamba kunafanyika mkutano wa jumuiya isiyo halali, au wa watu ambao ni wanachama wa jumuiya isiyo halali, na kukamata au kuwezesha kukamatwa kwa watu wote waliopo katika mkutano huo na kupekua nyumba, jengo au mahala, na kuchukua au kuwezesha kuchukuliwa nembo zote, mabango, silaha, vitabu, karatasi, nyaraka na mali nyengineyo ambayo anaweza kuwa na kila sababu ya kuamini kuwa ni mali ya jumuiya isiyo halali, au kwa njia yoyote inahusika na makusudio ya mkutano huo.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "afisa anayeshughulikia amani" maana yake ni hakimu yeyote au askari polisi si chini ya cheo cha msimamizi *(Superintendent).*

Kutangazwa jumuiya isiyo halali.

**52.**-(1) Endapo jumuiya inatangazwa kuwa si jumuiya halali kwa amri ya Rais wa Zanzibar, mambo yafuatayo yatahusika:

(a) mali za jumuiya zilizopo Zanzibar zitakuwa mikononi mwa afisa aliyeteuliwa na Rais wa Zanzibar;

(b) afisa aliyeteuliwa na Rais wa Zanzibar atashughulikia na kufunga shughuli za jumuiya na, baada ya kujiridhisha na kulipa madeni na dhima za jumuiya na gharama za ufungaji wa shughuli za jumuiya, iwapo kutakuwa na bakaa ya mali, atatayarisha na kuwasilisha kwa Rais wa Zanzibar mpango wa utaratibu wa matumizi ya bakaa ya mali;

(c) mpango wa utaratibu, utakapowasilishwa ili kupata idhini, unaweza kurekebishwa na Rais wa Zanzibar kama atakavyoona inafaa kulingana na mazingira husika;

(d) idhini ya Rais wa Zanzibar kwa mpango huo itatambuliwa kwa kupitia hati ya idhini iliyotiwa saini na Rais wa Zanzibar na, baada ya kufanyika hayo, bakaa ya mali, ambayo inahusika na mpango huo

itakuwa mikononi mwa afisa kwa mujibu wa masharti na madhumuni yatakayoelezwa;

(e) kwa madhumuni ya kufunga shughuli za jumuiya, afisa aliyeteuliwa na Rais wa Zanzibar atakuwa na uwezo wote ambao anao mtu aliyekabidhiwa rasmi kwa lengo la kuzitambua mali za mdaiwa na kuzikusanya.

(2) Rais wa Zanzibar anaweza, kwa madhumuni ya kuiwezesha jumuiya kufunga shughuli zake, kusimamisha kutumika kwa kifungu hiki kwa kipindi ambacho ataona inafaa.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayatatumika kwa mali iliyochukuliwa wakati wowote chini ya kifungu cha 51.

Kuchukua mali.

**53.** Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 52 cha Sheria hii, nembo, mabango, silaha, vitabu, karatasi, nyaraka na mali nyengineyo ya jumuiya isiyo halali itataifishwa na Serikali.

Maana ya mkusanyiko usio halali na ghasia.

**54.**-(1) Endapo watu watatu au zaidi wanakusanyika kwa nia ya kutaka kutenda kosa, au, wakiwa wamekusanyika kwa nia ya kutenda madhumuni fulani kwa pamoja, wakajiweka katika hali ambayo itawafanya watu walio jirani wawe na sababu ya kuogopa kwamba watu hao waliokusanyika watavunja amani, au kwa kukusanyika huko kutachochea, bila ya sababu ya maana, watu wengine wavunje amani, watakuwa ni mkusanyiko usio halali.

(2) Haijalishi kama mkusanyiko wa mwanzo ulikuwa halali, endapo baada ya kukusanyika, walijiweka kwa madhumuni ya pamoja kwa namna iliyokwisha tajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Wakati mkusanyiko usio halali unapoanza kutimiza madhumuni ya mkusanyiko kwa kuvunja amani na kujenga vitisho kwa jamii, mkusanyiko huo utaitwa ghasia na watu waliokusanyika watatambuliwa kuwa wamekusanyika kwa ajili ya ghasia.

Adhabu ya mkusanyiko usio halali.

**55.** Mtu yeyote ambaye anashiriki katika mkusanyiko usio halali atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Adhabu ya kushiriki katika ghasia.

**56.** Mtu yeyote ambaye anashiriki katika ghasia atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka miwili.

Kutoa tangazo kwa wafanya ghasia kutawanyika.

**57.** Afisa yeyote wa polisi wa ngazi ya juu au afisa yoyote wa ngazi ya juu wa jeshi la ulinzi ndani ya Zanzibar, atakayeona watu kumi na mbili au zaidi

wamekusanyika kwa ajili ya ghasia, au ana wasiwasi kuwa ghasia inataka kufanywa na watu kumi na mbili au zaidi anaowaona, anaweza kutoa au kuwezesha kutolewa tangazo kwa jina la Rais wa Zanzibar, kwa namna atakayoona inafaa, kuwaamrisha wafanya ghasia au watu hao waliokusanyika kutawanyika kwa amani.

Kutawanyika kwa wafanya ghasia baada ya tangazo kutolewa.

**58.** Iwapo muda utapita baada ya tangazo kutolewa, au baada ya kuzuiwa kwa nguvu tangazo hilo kutolewa, watu kumi na mbili au zaidi wanaendelea kukusanyika pamoja kufanya ghasia, mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kutoa tangazo, au afisa wa polisi yeyote, au mtu mwengine yeyote anayemsaidia mtu huyo au afisa huyo wa polisi, anaweza kufanya mambo yote muhimu kuwatawanya watu wanaoendelea kukusanyika, au kuwakamata wote au yeyote miongoni mwao, na iwapo mtu yeyote atakaidi, anaweza kutumia nguvu zote zitakazolazimu kwa kuendana na kuzuia ukaidi huo, na hatawajibika katika shauri lolote la jinai au madai lililohusu madhara au kifo cha mtu yeyote katika kutumia nguvu hizo.

Ghasia baada ya tangazo.

**59.** Iwapo tangazo limetolewa, kuwaamrisha watu waliojihusisha katika ghasia au waliokusanyika kwa ajili ya kufanya ghasia kutawanyika, mtu ambaye ndani ya muda au baada ya kupita muda wa tangazo hilo, anashiriki au anaendelea kushiriki katika ghasia au mkusanyiko, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja lakini kisichozidi miaka mitano.

Kuzuia au kupinga utoaji wa tangazo.

**60.** Mtu yeyote ambaye kwa kutumia nguvu anazuia au anaweka kizuizi cha utoaji wa tangazo kama ilivyo katika kifungu cha 57 cha Sheria hii, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi; na kama utoaji wa tangazo umezuiwa, mtu ambaye anajua kwamba utoaji wa tangazo umezuiwa, anashiriki au anaendelea kushiriki katika ghasia au mkusanyiko, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Wafanya ghasia kubomoa majengo.

**61.** Watu ambao, wamekusanyika kinyume cha sheria kufanya ghasia wanabomoa au wanaharibu, au wanaanza kubomoa au kuharibu jengo lolote, njia ya reli, mitambo au miundombinu ya majengo, watakuwa ni wakosa na kila mmoja wao atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Wafanya ghasia kuharibu majengo.

**62.** Watu ambao, wamekusanyika kinyume cha sheria kufanya ghasia wanaharibu kitu chochote kilivyotajwa katika kifungu cha 61 cha Sheria hii, watakuwa ni wakosa na kila mmoja wao atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka saba.

Kuingilia kwa ghasia gari au chombo cha baharini.

**63.** Watu ambao, wamekusanyika kufanya ghasia, kinyume na sheria na kwa kutumia nguvu wanazuia, wanachelewesha au wanaweka kizuizi upakiaji au ushushaji wa gari au chombo cha baharini, au kuzuia kuanza au upitaji wa gari, au upitaji au uongozaji wa chombo cha baharini, au kinyume na sheria na kwa kutumia nguvu kuingia katika

gari au chombo cha baharini kwa madhumuni ya kutenda hayo, watakuwa ni wakosa na kila mmoja wao atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kutembea na silaha hadharani na kumiliki silaha bila halali.

**64.**-(1) Mtu yeyote anayetembea na silaha hadharani kinyume na sheria kwa namna ambayo inasababisha hofu kwa mtu, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili na silaha hiyo itachukuliwa na Serikali.

(2) Mtu yeyote ambaye, bila halali ana katika milki yake au ananunua au anapata silaha yoyote ya moto au risasi kwa ajili ya silaha ya moto, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na nne.

Kuingia kwa nguvu.

**65.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa ajili ya kutaka kuhodhi, anaingia katika ardhi yoyote au makaazi kwa nguvu, ama nguvu hizo za mabavu zimetumika kwa mtu mwengine yeyote au kwa kutisha au kufungua kwa kuvunja nyumba yoyote au kwa kukusanyika idadi ya watu isiyo ya kawaida, atakuwa ni mkosa wa kosa la "kuingia kwa nguvu" na, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

(2) Haijalishi kwamba anastahiki au hastahiki kuingia katika ardhi, isipokuwa kwamba mtu anaeingia katika ardhi au makaazi yake mwenyewe, lakini yapo katika hifadhi ya mtumishi au mlinzi wake, hatakuwa ametenda kosa la kuingia kwa nguvu.

Kuzuia kwa nguvu.

**66.** Mtu yeyote ambaye, anaehodhi ardhi bila ya haki yoyote, anahodhi ardhi hiyo katika namna ambayo inaweza kuleta uvunjifu wa amani au kusababisha woga wa uvunjifu wa amani, dhidi ya mtu anaestahiki kisheria kuhodhi ardhi hiyo, atakuwa ni mkosa wa kosa la "kuzuia kwa nguvu" na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kupigana hadharani.

**67.** Mtu yeyote ambaye anashiriki katika kupigana hadharani atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi shilingi laki tano.

Kuchochea mapigano ya watu wawili.

**68.** Mtu yeyote ambaye anamchochea mtu mwengine kupigana, au anajaribu kumchochea mtu mwengine kupigana na mtu mwengine, au anajaribu kumchochea mtu amchochee mtu mwengine kupigana, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kutishia kwa kutumia nguvu.

**69.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa nia ya kumuogopesha au kumkasirisha mtu anatishia kuvunja au kuharibu nyumba ya kuishi; au

(b) kwa nia ya kumshitua mtu katika nyumba ya makaazi, anatoa silaha ya moto yenye risasi au anafanya kitendo chengine chochote cha uvunjifu wa amani,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Iwapo kosa limetendwa wakati wa usiku, mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kusumbua na kuzonga.

**70.**-(1) Mtu yeyote ambaye anasumbua au anazonga:

(a) nyumba yoyote au maeneo ya karibu ya nyumba hiyo, kwa madhumuni ya kuzuia mtu mwengine yeyote asifanye kitu chochote ambacho mtu huyo ana haki kisheria kufanya mahala hapo; au

(b) nyumba au mahala pengine ambapo mtu mwengine anafanya shughuli zake au yupo, au maeneo ya karibu ya nyumba au mahala hapo kwa madhumuni ya kumzuia mtu huyo mwengine asifanye au kumlazimisha kufanya kitendo chochote ambacho mtu huyo mwengine ana haki kisheria kufanya au kumlazimisha kufanya kitendo ambacho ana haki ya kutokufanya,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili.

(2) Masharti ya kifungu hiki hayatatumika kwa kusumbua au kuzonga ambako ni halali katika masharti ya sheria nyengine zozote zinazohusiana na vyama vya wafanyakazi au migogoro ya kazi.

(3) Mtu hatoshtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kutisha.

**71.**-(1) Mtu yeyote ambaye kimakosa na bila ya mamlaka ya kisheria anamtisha mtu mwengine yeyote kwa nia ya kumlazimisha mtu huyo:

(a) kumzuia kufanya kitendo chochote ambacho ni haki yake kukifanya; au

(b) kufanya kitendo chochote ambacho ana haki kisheria kuacha kukifanya,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

(2) Katika kifungu hiki:

neno "kutisha" maana yake ni kusababisha katika akili ya mtu hofu ya kupata madhara yeye mwenyewe au mtu mwengine wa familia yake au wategemezi wake au hofu ya kutumika nguvu au madhara kwa mtu au mali;

neno "madhara" linajumuisha madhara kwa mtu kuhusiana na biashara, kazi, ajira au njia nyengine ya kipato na linajumuisha pia kitendo chochote kinachoweza kushitakiwa.

(3) Mtu hawezi kushitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo.

**72.** Watu wawili au zaidi ambao wanakusanyika pamoja, kwa lengo la kuteremsha, kuchukua au kuficha bidhaa yoyote iliyolazimika kulipiwa ushuru wa forodha na inayowajibika kutaifishwa na Serikali chini ya sheria yoyote inayohusiana na ushuru wa forodha, watakuwa ni wakosa, na kila mmoja wao atapewa adhabu ya kulipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita.

Silaha za hatari katika mikutano ya hadhara na kitendo cha uvunjifu wa amani.

**73.**- (1) Mtu ambaye:

(a) wakati yupo katika mkutano wowote wa hadhara au katika maandamano ana silaha yoyote ya hatari, bila ya kuwa na mamlaka ya kisheria au ruhusa ya Kamishna wa Polisi; au

(b) katika sehemu yoyote ya hadhara au katika mkutano wowote wa hadhara anatumia maneno ya vitisho, kejeli au matusi au mwenendo wenye nia ya kuchochea uvunjifu wa amani au kwa mwenendo huo uvunjifu wa amani unaweza kutokea,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Hamsini Elfu au adhabu zote mbili.

(2) Kwa madhumuni ya aya ya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu hatochukuliwa kuwa ametenda kulingana na mamlaka ya kisheria isipokuwa awe ametenda kwa nafasi yake kama afisa wa polisi au kwa maelekezo ya Kamishna wa Polisi.

(3) Katika kifungu hiki:

(a) "mkutano wa hadhara" unajumuisha mkutano unaofanyika hadharani na mkutano mwengine wowote ambao jamii au baadhi ya watu katika

jamii wanaruhusiwa kuhudhuria, ama kwa malipo au vyenginevyo, na kwa madhumuni ya tafsiri hii "mkutano" maana yake ni mkutano unaofanywa kwa madhumuni ya kujadili mambo yenye maslahi ya umma au kwa madhumuni ya kutoa maoni kuhusiana na mambo hayo;

(b) "maandamano ya hadhara" maana yake ni maandamano yanayofanywa hadharani.

Kuwa na silaha za hatari bila ya mamlaka ya kisheria.

**74.**-(1) Mtu ambaye anaingiza nchini, anatengeneza, anauza, anatoa au anatangaza kwa ajili ya kuuza au anavaa au anachukua silaha yoyote ya hatari bila ya mamlaka ya kisheria atakuwa ni mkosa, na jukumu la kuthibitisha mamlaka hayo litakuwa juu yake.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "silaha ya hatari" maana yake ni kitu chochote kilichotengenezwa au kinachotumika kusababisha madhara kwa mtu au inakusudiwa na mtu aliyenacho kwa matumizi yake hayo na bila ya kuathiri ujumla wa hayo yaliyotajwa inajumuisha vitu vifuatavyo na sehemu ya vitu hivyo yaani singe yoyote, upanga, ala ya upanga, jambia, kisu, mshale, shoka, lakini haijumuishi vitu vifuatavyo:

(a) kisu cha kukunja ambacho kina sehemu ya kukatia isiyozidi urefu wa inchi nne ambapo kisu hicho cha kukunja hakijatengenezwa kuweza kubadilishwa kwa njia ya spiringi au vyenginevyo kuwa jambia au kisu kisichokuwa cha kukunja; au

(b) kitu ambacho kimsingi kimetengenezwa kwa ajili ya kutumika katika fani maalum, kazi ya mikono, au shughuli au kwa matumizi ya nyumbani na ambacho kinaingizwa nchini, kinatengenezwa au kuuzwa kwa matumizi hayo au ambacho kinavaliwa au kinachukuliwa na mtu ambae anatekeleza au anaendeleza fani hiyo, kazi ya mikono au shughuli ambayo kitu kilichovaliwa au kuchukuliwa na mtu huyo kimsingi kimetengenezwa kwa ajili hiyo; au ambacho kinavaliwa au kinachukuliwa kwa matumizi ya nyumbani tu; au

(c) kitu kinapovaliwa au kuchukuliwa na mtu ndani ya nyumba yake au eneo la nyumba yake au kwenye chombo chochote.

(3) Endapo mtu anatiwa hatiani kwa kosa chini ya masharti ya kifungu hiki au baada ya kushtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hicho shtaka hilo litaondoshwa chini ya masharti ya kifungu cha 327 cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Mahakama inaweza kutoa amri ya kutaifisha silaha hiyo hatari ambapo kwa silaha hiyo kosa lilitendeka na kutoa amri ya kuangamizwa au kuharibiwa.

## SEHEMU YA TISA
## MAKOSA YANAYOHUSU USIMAMIZI WA HAKI

Ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.

**75.**-(1) Mtu yeyote ambaye, katika kesi yoyote, au kwa ajili ya kuanzisha kesi yoyote, kwa kujua anatoa ushahidi wa uongo unaogusa jambo lolote ambalo ni muhimu kwa suala lolote linalohusika na kesi hiyo au linalokusudiwa kuibuliwa katika kesi hiyo, atakuwa ni mkosa wa kosa la "kutoa ushahidi wa uongo".

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:

(a) haijalishi ikiwa ushahidi umetolewa kwa kiapo au chini ya ruhusa nyengine yoyote iliyoruhusiwa na sheria;

(b) taratibu na desturi zinazotumika katika usimamizi wa kiapo au njia nyengine inayomlazimisha mtu mwenye kutoa ushahidi kusema ukweli hazitapewa uzito, endapo mwenye kula kiapo amekubali taratibu na desturi ambazo hasa zimetumika;

(c) haijalishi ikiwa ushahidi wa uongo umetolewa kwa mdomo au kwa maandishi;

(d) haijalishi ikiwa Mahakama au Baraza limeundwa kwa mujibu wa utaratibu, au limekaa katika mahala sahihi, au vyenginevyo, iwapo Mahakama au Baraza limefanya kazi hasa kama Mahakama au Baraza katika shauri ambalo ushahidi huo umetolewa;

(e) haijalishi ikiwa mtu mwenye kutoa ushahidi ana sifa za kutoa ushahidi au hana, au ikiwa ushahidi huo unakubalika katika shauri au haukubaliki.

(3) Mtu ambaye anamsaidia, anamhamasisha, anamshauri, anamuwezesha, au anamshawishi mtu mwengine atende kosa la utoaji wa ushahidi wa uongo atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "kushawishi kutoa ushahidi wa uongo".

Maelezo ya uongo ya wakalimani.

**76.** Endapo mkalimani rasmi wa Mahakama yoyote katika shauri lolote, au mtu yeyote ambaye ameapishwa kisheria kama mkalimani katika kesi, kwa makusudi anatoa maelezo muhimu katika kesi hiyo ambayo anajua kuwa ni uongo, au haamini kuwa ni ya kweli, atakuwa ni mkosa wa kosa la kutoa ushahidi wa uongo.

Adhabu ya kutoa ushahidi wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.

**77.** Mtu ambaye ametenda kosa la kutoa ushahidi wa uongo au la kushawishi kutoa ushahidi wa uongo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka saba.

Ushahidi wa shtaka la kutoa **ushahidi** wa uongo na kushawishi kutoa ushahidi wa uongo.

**78.** Mtu hatotiwa hatiani kwa kutenda kosa la kutoa ushahidi wa uongo au kushawishi kutoa ushahidi wa uongo kwa kutegemea ushahidi wa shahidi mmoja pekee kuhusu uongo wa maelezo yanayodaiwa kuwa ya uongo, isipokuwa utakapoungwa mkono kwa nyaraka.

Kutunga ushahidi.

**79.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kuipotosha Mahakama yoyote au Baraza lolote katika kesi yoyote:

(a) anatunga ushahidi kwa njia yoyote isiyokuwa ya kutoa ushahidi wa uongo au kushawishi kutoa ushahidi wa uongo; au

(b) kwa kujua anatumia ushahidi huo wa kutunga,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Kiapo cha uongo.

**80.** Mtu yeyote ambae anaapa uongo au anathibitisha uongo au anatoa tamko la uongo mbele ya mtu aliyeidhinishwa kusimamia kiapo au kupokea tamko kuhusiana na jambo lolote lenye maslahi ya umma katika hali ambayo kiapo hicho cha uongo au tamko hilo, endapo lingefanywa kwa uongo katika shauri Mahakamani lingehisabika kuwa ni kutoa ushahidi wa uongo, atakuwa ni mkosa.

Kudanganya mashahidi.

**81.** Mtu yeyote anayefanya udanganyifu wowote au hadaa, au kwa kujua anatoa au anaonesha maelezo ya uongo, kiashiria, alama au maandishi, kwa mtu aliyeitwa au atakayeitwa kuwa shahidi katika kesi, kwa nia ya kuathiri ushahidi wa mtu huyo kama shahidi, atakuwa ni mkosa.

Kuharibu ushahidi.

**82.** Mtu yeyote ambaye, kwa kujua kwamba kitabu chochote, nyaraka, au kitu cha namna yoyote, kinahitajika au kinaweza kuhitajika katika ushahidi kwenye kesi, kwa makusudi anakiondoa au anakiharibu au anakifanya kisiweze kusomeka au kisiweze kufahamika au kisiweze kutambulika, kwa nia ya kuzuia kitu hicho kisitumike katika ushahidi, atakuwa ni mkosa.

Njama za kuzuia haki na kuingilia mashahidi.

**83.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anakula njama na mtu mwengine yeyote kumtuhumu mtu yeyote kwa uongo kwa kosa lolote la jinai au kufanya jambo lolote kwa lengo la kuzuia, kukinga, kupotosha au kuharibu utekelezaji wa haki;

(b) kwa dhamira ya kuzuia utekelezaji wa haki, anamvunja moyo, anamzuia au anamkataza mtu yeyote anayewajibika kisheria

kuhudhuria na kutoa ushahidi kama shahidi Mahakamani kutokuhudhuria na kutoa ushahidi, au anajitahidi kufanya hivyo; au

(c) anazuia au anaingilia kwa njia nyengine yoyote au kwa kujua anazuia utoaji wa nyaraka za kisheria zinazohusika na kadhia za madai na jinai,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kufifilisha makosa.

**84.**-(1) Mtu yeyote ambaye anaomba, anapokea, au anachukua au anakubali au anajaribu kupokea au kuchukua mali au manufaa ya aina yoyote kwa maslahi yake au ya mtu mwengine kwa makubaliano yoyote au maelewano kwamba atafifilisha au aficha kosa, au atazuia, atakatisha au atacheleweshaa uendeshaji wa mashitaka wa kosa lolote au atazuia ushahidi wowote husika, atakuwa ni mkosa.

(2) Pale mtu anapotiwa hatiani kwa kosa lililopo chini ya kifungu hiki, Mahakama inaweza, kwa kuongezea au badala ya, adhabu yoyote inayoweza kutolewa, kuamrisha kutaifishwa na Serikali, mali ambayo imepatikana wakati wa kufanyika kosa hilo, au, iwapo mali hiyo haiwezi kutaifishwa au haiwezi kupatikana, Mahakama itatathmini thamani ya mali hiyo.

(3) Mali au thamani iliyotaifishwa itashughulikiwa kwa namna ambayo Rais wa Zanzibar anaweza kuelekeza.

(4) Malipo ya thamani yoyote iliyoamriwa na Mahakama kutaifishwa yanaweza kutekelezwa katika namna ile ile na kwa masharti yale yale kama faini.

Kufifilisha mashtaka.

**85.**-(1) Mtu yeyote ambaye, ameshapeleka mashtaka au kwa kisingizio cha kupeleka mashtaka, dhidi ya mtu mwengine chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote kwa dhamira ya kupata kutoka kwa mtu huyo mwengine malipo kwa kosa lolote lililofanywa au linalodaiwa kufanywa na mtu huyo mwengine, anafifilisha mashtaka hayo bila ya amri au idhini ya Mahakama ambayo mashtaka hayo yamepelekwa au yatapelekwa, atakuwa ni mkosa.

(2) Pale mtu anapotiwa hatiani kwa kosa lililopo chini ya kifungu hiki, Mahakama inaweza, kwa kuongezea au badala ya, adhabu yoyote inayoweza kutolewa, kuamrisha kutaifishwa na Serikali, mali ambayo imepatikana wakati wa kufanyika kosa hilo, au, iwapo mali hiyo haiwezi kutaifishwa au haiwezi kupatikana, Mahakama itatathmini thamani ya mali hiyo.

(3) Mali au thamani iliyotaifishwa itashughulikiwa kwa namna ambayo Rais wa Zanzibar anaweza kuelekeza.

(4) Malipo ya thamani yoyote iliyoamriwa na Mahakama kutaifishwa yanaweza kutekelezwa katika namna ile ile na kwa masharti yale yale kama faini.

Matangazo kwa mali iliyoibiwa.

**86.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anatangaza hadharani kutoa zawadi kwa kurejeshewa mali yoyote ambayo imeibiwa au imepotea, na katika kutoa tangazo hilo anatumia maneno yanayomaanisha kwamba hakutaulizwa swali lolote, au mtu atakaeleta mali hiyo hatokamatwa wala kudhuriwa;

(b) anatangaza hadharani kumrejeshea mtu ambaye amechukua au ametoa fedha kwa njia ya mkopo kwa mali yoyote iliyoibiwa au kupotea, fedha hizo zilizolipwa au zilizochukuliwa kwa njia ya mkopo, au kiasi chengine chochote cha fedha au zawadi kwa ajili ya kurejeshewa mali hiyo; au

(c) anachapisha au anasambaza tangazo hilo,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kudharau Mahakama.

**87.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) ndani ya jengo ambalo shauri lolote linasikilizwa, au ndani ya eneo la jengo hilo, anaonesha dharau kwa kuzungumza au kwa namna fulani kwenye shauri hilo linalosikilizwa, au kwa mtu ambaye mbele yake shauri hilo linasikilizwa;

(b) baada ya kuitwa kutoa ushahidi katika shauri, anashindwa kuhudhuria au, baada ya kuhudhuria, anakataa kula kiapo au kufanya uthibitisho, au baada ya kula kiapo au kufanya uthibitisho, anakataa bila ya sababu ya kisheria kujibu swali au kutoa waraka, au anabakia katika chumba ambacho shauri hilo linasikilizwa baada ya mashahidi kuamriwa kutoka katika chumba hicho;

(c) anasababisha kizuizi au ghasia wakati shauri linasikilizwa;

(d) wakati shauri linasubiri maamuzi, anatumia mazungumzo ya mdomo au maandishi kupotosha shauri hilo, au yanayoweza kuathiri mtu kwenye manufaa yake au dhidi ya wahusika wowote katika shauri hilo, au yatakayopelekea kushusha mamlaka ya mtu ambaye shauri hilo mbele yake linasikilizwa;

(e) anasambaza taarifa za ushahidi uliochukuliwa kwenye shauri lolote ambalo limeelekezwa kusikilizwa faragha;

(f) bila ya halali anajaribu kumuingilia au kumshawishi shahidi katika shauri ama kabla au baada ya kutoa ushahidi, kuhusiana na ushahidi huo;

(g) anamfukuza mtumishi kwa sababu ametoa ushahidi kwa niaba ya mhusika fulani katika shauri;

(h) anachukua tena ardhi kutoka kwa mtu ambaye punde tu alipewa umiliki kwa amri ya Mahakama;

(i) bila ya halali anamchukua tena mtoto kutoka kwa mtu ambaye alipewa uangalizi wa mtoto huyo kwa amri ya Mahakama;

(j) ana uwezo wa kulipa kiasi chochote kwa njia ya fidia au gharama au vyenginevyo katika mashauri ya madai au jinai yaliyoamuliwa alipe na Mahakama yoyote, bila halali anakataa au anapuuza baada ya kupewa notisi kufanya malipo hayo kwa mujibu wa amri yoyote ya kulipa ama kwa awamu au vyenginevyo; au

(k) anafanya kitendo chengine chochote cha kudharau kwa makusudi kwa shauri lolote, au kwa mtu yeyote ambaye shauri hilo linasikilizwa mbele yake,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu.

(2) Pale kosa lolote dhidi ya aya za (a), (b), (c), (d), au (k) za kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, limefanyika mbele ya Mahakama, Mahakama inaweza kuamuru mkosaji awekwe kizuizini, na wakati wowote kabla ya Mahakama haijaanza siku hiyo, inaweza kulishughulikia kosa hilo na kutoa adhabu kwa mkosaji ya faini isiyozidi shilingi laki moja au akishindwa kulipa, atapewa adhabu ya kifungo kisichozidi mwezi moja.

(3) Masharti ya kifungu hiki yatachukuliwa kuwa ni ziada, na si kwamba yanapunguza uwezo wa Mahakama Kuu kutoa adhabu kwa kosa la kuidharau Mahakama.

## SEHEMU YA KUMI
## KUOKOA, KUTOROKA NA KUWAZUIA WATUMISHI WA MAHAKAMA

Kuokoa

**88.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa kutumia nguvu, anamuokoa au anajaribu kumuokoa mtu mwengine yeyote kutoka kwenye kizuizi halali:

(a) ambaye amehukumiwa kifo au kifungo cha maisha au ameshtakiwa kwa kosa lenye adhabu ya kifo au kifungo cha maisha, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha;

(b) ambaye amefungwa kwa shtaka au kwa adhabu ya kosa lolote mbali ya hayo yaliyotajwa katika aya ya (a), atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba; au

(c) katika hali nyengine yoyote, atakuwa ni mkosa.

(2) Iwapo mtu aliyeokolewa yumo katika uangalizi wa mtu binafsi, mkosaji lazima ajue ukweli kwamba, mtu aliyeokolewa yupo katika ulinzi huo.

Kutoroka kwenye kizuizi halali.

**89.**-(1) Mtu yeyote ambaye, yupo kwenye kizuizi halali, anatoroka kutoka katika kizuizi hicho atakuwa ni mkosa na atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kinachowiana mara mbili ya ukubwa wa kipindi ambacho mtu huyo alikuwa anatumikia wakati alipokuwepo katika kizuizi halali.

(2) Adhabu inayohusiana na kosa la kutoroka kutoka kwenye kizuizi halali itaanza baada ya mtu huyo kukamilisha adhabu aliyokuwa anaitumikia mwanzo kabla ya kutoroka kutoka katika kizuizi halali.

(3) Mtu ambaye, yupo katika kizuizi halali kabla ya kutiwa hatiani, anatoroka kutoka kwenye kizuizi hicho, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kusaidia wafungwa kutoroka.

**90.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamsaidia mfungwa kutoroka au kujaribu kutoroka kutoka kwenye kifungo halali; au

(b) anapeleka kitu chochote au anasababisha kitu chochote kupelekwa ndani ya chuo cha mafunzo kwa nia ya kuwezesha mfungwa kutoroka,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Kutoroka kutoka kifungoni au kizuizini kwa makusudi au kwa uzembe wa mtumishi wa umma.

**91.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mtumishi wa umma anayewajibika kisheria kama mtumishi wa umma kumueka kizuizini mtu anayeshtakiwa au aliyetiwa hatiani kwa kosa lolote au amepelekwa kizuizini kisheria, kwa uzembe au kwa makusudi anamuwezesha mtu huyo kutoka kizuizini, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili.

Uondoshaji wa mali iliyokamatwa kihalali.

**92.** Mtu yeyote ambaye, pale mali inapokuwa imekamatwa au imechukuliwa kwa amri au mamlaka ya Mahakama yoyote, kwa kujua, na kwa nia ya kuzuia au kuharibu ukamataji huo au amri, anapokea, anaondoa, anabakisha, anaficha au anauza mali hiyo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kuwazuia maafisa wa Mahakama.

**93.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi anazuia, au kwa kujua anakinga au kwa njia yoyote anaingilia au anazuia kupokea yeye mwenyewe au mtu mwengine wito, notisi, amri, hati ya kukamata, kuweka kizuizini au kupekua au hati nyengine zinazotolewa na Mahakama ili zipokelewe na yeye mwenyewe au mtu mwengine, kama hali itakavyokuwa;

(b) kwa makusudi anazuia au kwa kujua anakinga au kwa njia yoyote anaingilia au anazuia utekelezaji wa wito, notisi, amri, hati ya kukamata, kuweka kizuizini au kupekua au hati nyengine zinazotolewa na Mahakama au mtu mwengine mwenye dhamana ya kisheria ya utekelezaji wa hati hizo;

(c) kwa makusudi anachelewesha utekelezaji wa wito, notisi, amri, hati ya kukamata, kuweka kizuizini au kupekua au hati nyengine zinazotolewa na Mahakama; au

(d) anatoroka kwa dhamira ya kuepuka asipewe wito wowote, notisi, amri, hati ya kukamata, kuweka kizuizini au kupekua au hati nyengine zinazotolewa na Mahakama,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA MCHANGANYIKO DHIDI YA MAMLAKA YA UMMA

Udanganyifu na uvunjaji uaminifu kwa watumishi wa umma.

**94.** Mtu yeyote aliyeajiriwa katika utumishi wa umma ambaye, katika kutekeleza majukumu ya ofisi yake, anafanya udanganyifu wowote au kuvunja uaminifu unaoathiri jamii, ama udanganyifu huo au uvunjaji wa uaminifu ungekuwa ni jinai au si jinai kama ungetendwa dhidi ya mtu binafsi, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kuupuuza wajibu wa kikazi.

**95.** Mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma ambaye, kwa makusudi anapuuza kutekeleza jukumu lolote ambalo anawajibika kwa mujibu wa sheria kulitekeleza, isipokuwa kwamba utekelezaji wa jukumu hilo hauandamani na hatari kubwa zaidi

kuliko ambayo mtu wa kawaida angeweza kutarajia kukabiliana nayo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kusababisha hasara kwa Serikali au Taasisi za Umma.

**96.**-(1) Mtu yeyote ambaye, akiwa muajiriwa, afisa au mfanyakazi wa taasisi ya umma, kwa makusudi ametenda au ameacha kutenda, au kwa uzembe wake au tabia mbaya au kwa sababu yoyote ameshindwa kuchukua hatua muafaka, anasababisha taasisi ya umma inayohusika kupata hasara yoyote ya kifedha au madhara ya mali inayomilikiwa au iliyo katika mikono ya taasisi ya umma, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kinachozidi miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi au atatozwa faini inayozidi shilingi milioni tatu lakini isiyozidi shilingi milioni kumi au adhabu zote mbili.

(2) Mahakama itatoa amri kwa Serikali kutaifisha mali ambayo ilipatikana kutokana na utendwaji wa kosa, au iwapo mali hiyo haiwezi kutaifishwa au haiwezi kupatikana, Mahakama itatathmini thamani ya mali hiyo.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "taasisi ya umma" maana yake na inajumuisha:

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(b) Shirika la Umma lililoanzishwa kwa sheria nyengine yoyote;

(c) Kampuni, ambayo hisa nyingi za mtaji wa shirika hilo zinamilikiwa na Serikali;

(d) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mashirika yake yaliyopo Zanzibar.

(4) Bila kujali ukweli kwamba taasisi ya umma imeshapokea malipo ya bima kuhusiana na hasara iliyopatikana au vyenginevyo imeshalipwa fidia kwa ajili ya hasara hiyo, taasisi hiyo ya umma bado itachukuliwa kwamba imepata hasara ya kifedha chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(5) Mtu anayeshtakiwa chini ya Sheria hii kwa wizi au kosa lolote na akaachiwa huru, anaweza kushtakiwa baadae na kupelekwa Mahakamani kwa kosa chini ya kifungu hiki kutokana na matendo hayo hayo au kutokutenda matendo hayo hayo ambayo yalikuwa msingi wa shtaka la awali.

(6) Baada ya kutiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki, Mahakama vile vile itaamuru mtu huyo kuilipa taasisi ya umma fidia ya kiwango kinachowiana na hasara halisi iliyopata taasisi ya umma husika.

(7) Amri hiyo ya fidia inayotolewa na Mahakama inaweza kusajiliwa na taasisi ya umma husika katika Mahakama yenye mamlaka ya jambo hilo kwa ajili ya kukaza hukumu bila ya kujali kiwango kinachohusika.

(8) Mashtaka chini ya kifungu hiki hayatoanzishwa bila ya ruhusa ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa umma.

**97.** Mtu yeyote ambaye anatoa kwa mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma taarifa yoyote ambayo anajua au anaamini kuwa ya uongo, anakusudia kwa taarifa hiyo kusababisha, au anajua kuwa taarifa hiyo ina uwezekano mkubwa kuwa atasababisha mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma:

(a) kufanya au kutokufanya kitu chochote ambacho mtu huyo aliyeajiriwa katika utumishi wa umma asingepaswa kufanya au kutokukifanya endapo ukweli halisi wa jambo kuhusiana na taarifa hiyo iliyotolewa angekuwa anaujua; au

(b) kutumia mamlaka halali ya mtu huyo aliyeajiriwa katika utumishi wa umma kumdhuru au kumuudhi mtu yeyote,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili.

Kutokutii wajibu wa kisheria.

**98.** Mtu yeyote ambaye, kwa makusudi hatii sheria yoyote kwa kufanya kitendo kilichokatazwa na sheria, au kwa kuacha kufanya kitendo chochote kinachotakiwa kufanywa, na ambacho kinahusu jamii au sehemu yoyote ya jamii, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au adhabu zote mbili, isipokuwa kama itaonekana kwenye sheria yoyote kwamba lengo la Baraza la Kutunga Sheria ni kutoa adhabu nyengine maalum kwa kutokutii huko.

Kutokutii amri za halali.

**99.** Mtu yeyote ambaye hatii amri yoyote, hati, au maelekezo yaliyotolewa ipasavyo, yaliyotolewa na Mahakama yoyote, afisa au mtu anayetekeleza jukumu lolote kwa nafasi yake na ameidhinishwa ipasavyo kwa nafasi hiyo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili, isipokuwa kama adhabu nyengine yoyote au namna yoyote ya shauri imeelezwa wazi kuhusiana na kutokutii huko.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA DINI

Kukashifu dini yoyote.

**100.** Mtu yeyote ambaye anavunja, anaharibu au anachafua mahala popote pa kuabudia kwa nia ya kukashifu dini yoyote ya watu au kwa kujua kwamba watu wa aina yoyote wanaweza kuchukulia kuvunja huko, kuharibu au kuchafua ni kashfa kwa dini yao, atakuwa ni mkosa.

Kufanya ghasia kwenye mikusanyiko ya dini.

**101.** Mtu yeyote ambaye kwa hiari yake anasababisha ghasia kwenye mkusanyiko halali ulioandaliwa kwa ajili ya ibada ya dini au sherehe ya dini, atakuwa ni mkosa.

Kuingia sehemu ya makaburi bila halali.

**102.** Mtu yeyote ambaye kwa madhumuni ya kuumiza hisia za mtu yeyote au kukashifu dini ya mtu, au kwa kujua kwamba hisia hizo za mtu zinaweza kuumizwa, au kwamba dini hiyo ya mtu inaweza kukashifiwa, anaingia bila halali katika sehemu ya ibada au katika sehemu ya kuzikia, au katika sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya kufanya taratibu za mazishi, au sehemu iliyoandaliwa kuhifadhia maiti, au anaikashifu maiti ya binaadamu, au anasababisha ghasia kwa watu waliokusanyika kwa ajili ya shughuli za mazishi, atakuwa ni mkosa.

Kuzuia mazishi ya mwili wa mtu aliyekufa.

**103.** Mtu yeyote ambaye bila halali anazuia mazishi ya mwili wa mtu yeyote, au bila ya mamlaka halali anafukua, anapasua, au anadhuru mwili wa mtu aliyekufa, au, akiwa ana wajibu wa kuwezesha mwili wa mtu aliyekufa kuzikwa, anashindwa kutekeleza wajibu huo, atakuwa ni mkosa.

Kuandika au kutamka maneno kwa nia ya kuumiza imani ya dini.

**104.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya makusudi ya kuumiza imani za dini ya mtu mwengine yeyote, anaandika neno lolote, au mtu ambaye, kwa nia kama hiyo, anatamka neno au anatoa sauti inayosikika na mtu mwengine yeyote au anafanya ishara au anaweka kitu kinachoonekana na mtu mwengine yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili.

Kukashifu dini.

**105.**-(1) Endapo watu wawili au zaidi wanakusanyika kwa nia ya kupanga dhidi ya Serikali na wanakusanyika hivyo kwa kisingizio cha kujishughulisha na utekelezaji wa ibada ya dini, watu hao ni wakosa kwa kosa la "kukashifu dini".

(2) Nia ya kupanga dhidi ya Serikali itachukuliwa iwapo mambo yafuatayo yatathibitishwa:

(a) kwamba watu wamekusanyika kisiri au katika mazingira yanayopelekea kuibua shaka; na

(b) kwamba pahala ambapo watu hao wamekusanyika sio msikiti, kanisa, hekalu, au mahala pengine pa ibada; na

(c) kwamba athari za maneno ya ibada yoyote yanayosomwa na hao waliokusanyika yanaweza kupelekea Serikali kuchukiwa, kukejeliwa au kudharauliwa au kuhamasisha hisia mbaya na uadui dhidi ya Serikali.

(3) Mtu ambaye anakashifu dini atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Kuhamasisha uadui baina ya makundi tofauti.

**106.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa maneno, ama yaliyotamkwa au kuandikwa, au kwa alama, au kwa kiwakilishi kinachoonekana au vyenginevyo, anahamasisha au anajaribu kuhamasisha, kwa sababu za dini, kabila, mahala pa kuzaliwa, makaazi, lugha au jamii au sababu nyengine yoyote, kutokuelewana au hisia za uadui, chuki au nia mbaya baina ya dini tofauti, kabila, lugha au makundi ya kikanda au ya kijamii;

(b) anatenda tendo lolote ambalo linaharibu utunzaji wa amani baina ya dini tofauti, kabila, lugha au makundi ya kikanda au ya kijamii na ambacho kinaharibu au kinaweza kuharibu utulivu wa jamii; au

(c) anapanga zoezi lolote, harakati, mafunzo au shughuli inayofanana na hayo kwa kukusudia kwamba ushiriki katika shughuli hiyo utatumia au utafundisha matumizi ya nguvu za kijinai au ghasia au kujua kwamba washiriki katika shughuli hiyo watatumia au watafundishwa kutumia nguvu za kijinai au ghasia, au anashiriki katika shughuli inayotarajia kutumia au kufunza utumiaji wa nguvu za kijinai au ghasia au kujua uwezekano kwamba washiriki katika shughuli hiyo watatumia au watafunzwa kutumia nguvu za kijinai au ghasia, dhidi ya dini yoyote, kabila, lugha au kundi la kikanda au kijamii na shughuli hiyo, kwa sababu yoyote ile imesababisha au itapelekea kusababisha hofu au mshituko au hisia za kutokuwepo amani miongoni mwa watu wa dini hiyo, kabila, lugha au kundi la kikanda au kijamii,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

(2) Mtu yeyote ambaye anatenda kosa lililoainishwa katika kifungu cha (1) cha Sheria hii, katika mahala pa ibada au kwenye mkusanyiko ulioandaliwa kwa ajili ya kutelekeleza ibada ya dini au sherehe za dini, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## MAKOSA DHIDI YA MAADILI

Tafsiri ya kuingilia.

**107.** Wakati wowote ambapo mtu anashtakiwa kwa kosa lililopo katika Sehemu hii inaweza kuwa ni lazima kuthibitisha kuingilia, haitakuwa lazima kuthibitisha utoaji hasa wa mbegu ili kukamilika kuingilia, lakini kuingilia kutachukuliwa kuwa kumekamilika kwa ushahidi wa kuingiza tu.

Kubaka.

**108.**-(1) Ni kosa kwa mtu mwanamme kumbaka mtoto wa kike au mwanamke.

(2) Mtu mwanamme anatenda kosa la kubaka ikiwa anamuingilia kingono mtoto wa kike au mwanamke katika mazingira yaliyopo katika moja ya maelezo yafuatayo:

(a) ambaye si mke wake, au mke wake ambaye ametenganishwa nae kisheria bila ridhaa yake wakati wa muingiliano wa kingono;

(b) kwa ridhaa yake pale ambapo ridhaa hiyo imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho, au kwa kumuogopesha au kumtishia kumuua au kumuumiza au akiwa kizuizini bila halali;

(c) kwa ridhaa yake pale ambapo ridhaa hiyo imepatikana wakati alipokuwa hana akili timamu au alipokuwa amelewa kutokana na kilevi au dawa zozote, jambo au kitu, alichopewa na mwanamme huyo au mtu mwengine;

(d) kwa ridhaa yake pale ambapo mtu mwanamme anajua kwamba yeye si mume wake, na kwamba, ridhaa hiyo inatolewa kwa sababu mtoto wa kike au mwanamke huyo alifanywa kuamini kuwa yeye ni mwanamme ambaye ni mumewe kihalali;

(e) kwa ridhaa yake au bila ya ridhaa yake pale anapokua chini ya umri wa miaka kumi na nane, isipokuwa kama mtoto wa kike huyo ni mke wake ambaye hajatenganishwa nae kisheria.

(3) Mtu yeyote:

(a) akiwa mtu mwenye dhamana, anachukua fursa ya dhamana yake rasmi na anambaka mtoto wa kike au mwanamke kwa kutumia mahusiano yake rasmi au bila halali anamzuia na anambaka mtoto wa kike au mwanamke;

(b) akiwa katika uongozi au mfanyakazi wa mahabusu au sehemu nyengine ya uangalizi, iliyoanzishwa kisheria, au akiwa katika

taasisi ya wanawake au watoto, anachukua fursa ya dhamana yake na anambaka mwanamke mahabusu aliyopo ndani ya mahabusu, pahala pa uangalizi au taasisi;

(c) akiwa kwenye uongozi au mfanyakazi wa hospitali, anachukua fursa ya dhamana yake na anambaka mtoto wa kike au mwanamke;

(d) akiwa mganga wa kienyeji, anachukua fursa ya dhamana yake na anambaka mtoto wa kike au mwanamke ambaye, kwa madhumuni ya matibabu, ni mteja wake;

(e) akiwa kiongozi wa dini anachukua fursa ya dhamana yake na anambaka mtoto wa kike au mwanamke.

(4) Kwa madhumuni ya kuthibitisha kosa la kubaka:

(a) kuingiza kunatosha kukamilisha tendo la kuingilia kingono linalofanya kiini cha kosa; na

(b) ushahidi wa kukataa kama vile majeraha yanayoonekana mwilini sio muhimu kuthibitisha kuwa kuingilia kingono kumetendeka bila ridhaa yake.

Adhabu ya kubaka.

**109.**-(1) Mtu yeyote ambaye anabaka, isipokuwa katika mazingira yanayoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atapewa adhabu ya kifungo cha maisha na katika hali nyengine yoyote atapewa kifungo kisichopungua miaka thalathini na faini, na zaidi ya adhabu hizo ataamriwa alipe fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama, kwa mtu ambaye aliyetendewa kosa hilo kwa madhara ya kimwili au kisaikolojia aliyosababishiwa mtu huyo.

(2) Endapo kosa limetendwa na mtoto wa kiume mwenye umri chini ya miaka kumi na nane:

(a) ikiwa mkosaji kwa mara ya kwanza, ataadhibiwa kwa kupelekwa kwa mwaka mmoja nyumba ya watoto, skuli zilizoidhinishwa au kutumikia jamii;

(b) ikiwa mkosaji kwa mara ya pili, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miezi kumi na mbili;

(c) ikiwa mkosaji kwa mara ya tatu na ni sugu, atapewa adhabu kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Adhabu ya kubaka kwa kundi.

**110.**-(1) Endapo kosa la kubaka limetendwa na mtu mmoja au zaidi kwa kundi, kila mtu katika kundi hilo aliyetenda au aliyesaidia kutendeka kwa kosa hilo atachukuliwa kwamba ametenda kosa la kubaka kwa kundi.

(2) Mtu ambaye ametiwa hatiani kwa kubaka kwa kundi, atapewa adhabu ya kifungo cha maisha, bila ya kujali ushiriki wake halisi katika kubaka, na bila kujali ni mwanamme au mwanamke.

Kujaribu kubaka.

**111.**-(1) Mtu yeyote ambaye anajaribu kubaka atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini.

(2) Mtu anajaribu kubaka iwapo, kwa nia ya kuwezesha kufanyika kwa ngono haramu na mtoto wa kike au mwanamke, anaonesha nia yake kwa:

(a) kumtishia mtoto wa kike huyo au mwanamke kwa nia ya kufanya ngono;

(b) akiwa ni mtu mwenye dhamana au ushawishi kwa mtoto wa kike au mwanamke, anatumia kitendo chochote cha kitisho dhidi yake kwa nia ya kufanya ngono;

(c) anafanya udanganyifu kwa nia ya kupata idhini yake;

(d) endapo mtoto wa kike au mwanamke ameolewa, anajifanya kuwa yeye ni mume wa mtoto wa kike au mwanamke, na mtoto wa kike au mwanamke huyo anawekwa katika mazingira ambayo, isipokuwa kwa kutokea kitu kisichotegemea utashi wa mtu huyo, mtoto wa kike au mwanamke bila ridhaa yake angeingiliwa.

(3) Endapo kosa limefanywa na mtoto wa kiume mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, atapewa adhabu ya miezi sita kwa kupelekwa kwenye nyumba ya watoto, skuli zilizoidhinishwa au kuitumikia jamii.

Kutorosha mwanamke.

**112.** Mtu yeyote ambaye kwa nia ya kumuoa au kumuingilia mwanamke wa umri wowote, au kuwezesha mwanamke kuolewa au kuingiliwa na mtu mwengine yeyote, anamchukua mwanamke huyo au anamzuia, bila ya ridhaa yake, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Kutorosha watoto wa kike na kiume.

**113.**-(1) Mtu yeyote ambaye, bila ya halali anamchukua:

(a) mtoto wa kike ambaye hajaolewa kutoka nje ya uangalizi au ulinzi wa baba yake au mama yake au mtu mwengine mwenye dhamana kisheria ya kumtunza au kumhifadhi, na bila ya ridhaa ya baba huyo, mama au mtu mwengine;

(b) mtoto wa kiume kutoka nje ya uangalizi au ulinzi wa baba yake au mama yake au mtu mwengine mwenye dhamana kisheria ya kumtunza au kumhifadhi, na bila ya ridhaa ya baba huyo, mama au mtu mwengine,

atakuwa ni mkosa, na atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi.

(2) Haitokuwa utetezi kwa kosa lolote chini ya kifungu hiki iwapo itaonekana kwenye Mahakama ambayo mbele yake shtaka litapelekwa kwamba mtu anayeshtakiwa alikuwa na sababu ya msingi ya kuamini na kwa kweli aliamini kwamba muathirika alikuwa ana umri zaidi ya miaka kumi na nane.

Shambulio la aibu.

**114.**-(1) Mtu yeyote ambaye bila ya halali na bila ya heshima anamshambulia mwanamke, au mtoto wa kike atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano na atatozwa fidia itakayoamuliwa na Mahakama.

(2) Haitokuwa utetezi chini ya Sheria hii kwa shtaka la shambulio la aibu kwa mtoto wa kike, kuthibitisha kwamba mtoto wa kike alikubali kufanyiwa shambulio hilo.

(3) Mtu yeyote ambaye kwa nia ya kukashifu heshima ya mwanamke au mtoto wa kike, anatamka neno lolote, anatoa sauti yoyote au ishara au anaonesha kitu chochote akikusudia kwamba neno hilo au sauti hiyo isikike, au kwamba ishara hiyo au kitu hicho kionekane, na mwanamke huyo, au mtoto wa kike huyo au anaingilia faragha ya mwanamke huyo, mtoto wa kike, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na atatozwa fidia itakayoamuliwa na Mahakama.

Kunajisi mtoto wa kiume.

**115.**-(1) Mtu yeyote ambaye anamuingilia mtoto yeyote wa kiume atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(2) Mtu yeyote ambaye anajaribu kumuingilia mtoto yeyote wa kiume atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini.

Kunajisi mtu mwenye ulemavu wa akili.

**116.**-(1) Mtu yeyote ambaye, anajua kwamba mwanamke, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume ana ulemavu wa akili, bila ya halali anamuingilia katika mazingira ambayo hayahesabiki kuwa ni kubaka, lakini mazingira ambayo yatathibitisha kwamba mkosaji alijua wakati wa kutenda kosa kwamba mwanamke huyo, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume alikuwa mwenye ulemavu wa akili, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(2) Mtu yeyote ambaye, anajua kwamba mwanamke, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume ana ulemavu wa akili, bila ya halali anajaribu kumuingilia katika mazingira ambayo hayahesabiki kuwa ni kubaka, lakini mazingira ambayo yatathibitisha kwamba mkosaji alijua wakati wa kutenda kosa kwamba mwanamke huyo, mwanamme, mtoto wa kike au mtoto wa kiume alikuwa mwenye ulemavu wa akili, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini.

Kuwezesha ukahaba.

**117.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamuwezesha, au anajaribu kumuwezesha, mtu wa umri wowote, ama kwa ridhaa au bila ya ridhaa ya mtu huyo, kuwa kahaba ndani au nje ya Zanzibar;

(b) anamuwezesha, au anajaribu kumuwezesha, mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, aondoke Zanzibar, ama kwa ridhaa au bila ya ridhaa ya mtu huyo, kwa dhamira ya kuwezesha ngono haramu na mtu aliye nje ya Zanzibar, au anamuondosha au anajaribu kumuondosha Zanzibar mtu huyo, ama kwa ridhaa au bila ya ridhaa ya mtu huyo, kwa ajili hiyo;

(c) anamuwezesha, au anajaribu kumuwezesha, mtu mwenye umri wowote, kuondoka Zanzibar, ama kwa ridhaa au bila ya ridhaa ya mtu huyo, kwa nia kwamba, mtu huyo aishi, au awe anakwenda mara kwa mara kwenye danguro popote lilipo, au anamuondoa au anajaribu kumuondoa kutoka Zanzibar, mtu huyo, ama kwa ridhaa au bila ridhaa ya mtu huyo, kwa ajili hiyo;

(d) anamleta, au anajaribu kumleta Zanzibar, mtu mwenye umri wowote kwa dhamira ya kufanya ngono haramu na mtu mwengine yeyote ndani au nje ya Zanzibar;

(e) anamuwezesha, au anajaribu kumuwezesha, mtu mwenye umri wowote, ama kwa ridhaa, au bila ya ridhaa ya mtu huyo, aondoke mahala pake pa kawaida pa kuishi ndani ya Zanzibar, mahala hapo pakiwa sio danguro, kwa nia kwamba, mtu huyo kwa dhamira ya ukahaba awe anaishi au anakwenda mara kwa mara, kwenye danguro ndani au nje ya Zanzibar; au

(f) anamzuia mtu yeyote bila ya ridhaa ya mtu huyo katika danguro au mahala popote kwa dhamira ya kufanya ngono haramu au udhalilishaji wa kingono kwa mtu huyo,

atakuwa anatenda kosa la uwezeshaji ukahaba na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi au

atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au adhabu zote.

Kuwezesha ngono haramu.

**118.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa vitisho au kutishia, anamuwezesha au anajaribu kumuwezesha mtoto wa kike, mtoto wa kiume au mwanamke kufanya ngono haramu ndani au nje ya Zanzibar;

(b) kwa kujisingizia au kwa kusema uongo, anamuwezesha au anajaribu kumuwezesha mtoto wa kike, mtoto wa kiume au mwanamke kufanya ngono haramu ndani au nje ya Zanzibar; au

(c) anamnusisha, anampa, au anamuwezesha mtoto wa kike, mtoto wa kiume au mwanamke kutumia dawa yoyote au kitu chochote kwa nia ya kumpoteza fahamu au kupungukiwa nguvu ili kumuwezesha mwanamme kufanya ngono haramu kwa mwanamke huyo, mtoto wa kike au mtoto wa kiume,

atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja lakini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi au adhabu zote mbili.

Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kiume kunajisiwa.

**119.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mmiliki au mkaazi katika jengo anashughulikia au anafanya au anasaidia katika uangalizi au udhibiti wa jengo hilo, anamshawishi au kwa kujua anaruhusu mtoto wa kiume kukaa au kuwepo ndani ya jengo hilo kwa madhumuni ya kuingiliwa na mwanamme bila halali, ama kuingiliwa huko kunakusudiwa kuwe na mwanamme maalum au mwanamme yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi.

Mwenye nyumba kuruhusu mtoto wa kike kuingiliwa.

**120.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mmiliki au mkaazi katika jengo anashughulikia au anafanya au anasaidia katika uangalizi au udhibiti wa jengo hilo, anamshawishi au kwa kujua anaruhusu mtoto wa kike kukaa au kuwepo ndani ya jengo hilo kwa madhumuni ya kuingiliwa na mwanamme bila halali, ama kuingiliwa huko kunakusudiwa kuwe na mwanamme maalum au mwanamme yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi.

Kumzuia mwanamke, mtoto wa kike au mtoto wa kiume katika danguro au penginepo.

**121.**-(1) Mtu yeyote ambaye anamzuia mwanamke au mtoto wa kike au mtoto wa kiume bila ridhaa yake:

(a) ndani au katika jengo lolote kwa nia kwamba mwanamke, mtoto wa kike au mtoto wa kiume aingiliwe na mwanamme bila halali, ama mwanamme yeyote maalum au mwanamme yeyote; au

(b) katika danguro lolote,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

(2) Pale mwanamke, mtoto wa kike au mtoto wa kiume yumo katika jengo lolote kwa lengo la kuwa na mahusiano ya kingono bila halali, au yumo katika danguro lolote, mtu atachukuliwa amemzuia mwanamke huyo, mtoto wa kike au mtoto wa kiume ndani au katika jengo hilo au katika danguro hilo, ikiwa, kwa nia ya kumlazimisha au kumshawishi kubakia ndani au katika jengo hilo au danguro hilo, mtu huyo anazizuwia nguo zake za kuvaa mwanamke huyo, mtoto wa kike au mtoto wa kiume au mali zake nyengine, au pale nguo zake za kuvaa aliazimwa au vyenginevyo alipewa mwanamke huyo, mtoto wa kike, au mtoto wa kiume au kwa maelekezo ya mtu huyo, mtu huyo anamtisha mwanamke huyo, mtoto wa kike au mtoto wa kiume kwa mashtaka ya sheria kama atakimbia nazo nguo hizo za kuvaa alizoazimwa au alizopewa.

(3) Hatua za kisheria, ama za madai au jinai, hazitochukuliwa dhidi ya mwanamke huyo, au mtoto wa kike au mtoto wa kiume kwa kuzichukua au kukutwa nazo nguo hizo za kuvaa pale ambapo ilikuwa ni lazima kumuwezesha kuondoka katika jengo au danguro.

Uwezo wa kumtafuta mtu aliyezuiwa.

**122.**-(1) Iwapo hakimu ataona, kwa taarifa iliyotolewa kwake kwa kiapo na mzazi, jamaa au mlezi wa mwanamke, mtoto wa kiume au mtoto wa kike au mtu mwengine ambaye, kwa maoni ya hakimu, anatenda kwa nia njema kwa maslahi ya mwanamke, mtoto wa kiume au mtoto wa kike, kwamba kuna sababu ya msingi kutia shaka kwamba mwanamke huyo, mtoto wa kiume, au mtoto wa kike amezuiwa bila halali kwa malengo yaliyo kinyume na maadili na mtu katika sehemu yoyote ndani ya eneo la mamlaka ya hakimu huyo, hakimu huyo, anaweza kutoa hati, kumuidhinisha mtu aliyetajwa kwenye hati hiyo amtafute, na pale atakapompata, amchukue na amhifadhi kwenye sehemu salama mwanamke huyo, mtoto wa kiume au mtoto wa kike mpaka atakapoletwa mbele ya hakimu; na hakimu aliyepelekewa mwanamke huyo, mtoto wa kiume au mtoto wa kike atawezesha apelekwe kwa wazazi au walezi, au vyenginevyo atashughulikia kama mazingira yatakavyoruhusu na yatakavyohitaji.

(2) Hakimu anayetoa hati hiyo anaweza, kwa hati hiyo au hati nyengine yoyote, kuwezesha mtu anaetuhumiwa kumzuia bila ya halali mwanamke huyo, mtoto wa kiume au mtoto wa kike akamatwe na aletwe mbele ya hakimu na mashauri yataanzishwa kwa ajili ya kumuadhibu mtu huyo kwa mujibu wa sheria.

(3) Mwanamke, mtoto wa kiume au mtoto wa kike atachukuliwa kuwa amezuiliwa bila ya halali kwa malengo yaliyo kinyume na maadili ikiwa amezuiwa bila halali na kwa madhumuni ya kuingiliwa na mwanamme, ama mwanamme maalum au mwanamme mwengine yeyote.

(4) Mtu yeyote aliyeidhinishwa kwa hati chini ya kifungu hiki kumtafuta mwanamke, mtoto wa kiume au mtoto wa kike aliyezuiliwa kama ilivyoelezwa anaweza kuingia, hata kama itahitajika nguvu, katika nyumba, jengo au sehemu nyengine iliyotajwa kwenye hati, na anaweza kumtoa mwanamke huyo, mtoto wa kiume au mtoto wa kike kutoka humo.

Kosa la ukahaba.

**123.** Mtu yeyote ambaye kwa malipo anatoa mwili wake kuingiliwa kingono, anatenda kosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mtu mwanamme anayeishi kwa kipato cha ukahaba.

**124.**-(1) Mtu mwanamme ambaye:

(a) kwa kujua, anaishi kwa kipato chake chote au sehemu ya kipato chake kutokana na ukahaba; au

(b) hadharani, bila ya kuchoka anashawishi au analazimisha mambo yaliyo kinyume na maadili,

atakuwa ni mkosa.

(2) Pale mtu mwanamme inapothibitika anaishi na au kwa kawaida anaandamana na kahaba au inapothibitika anadhibiti, anaelekeza au anashawishi harakati za kahaba kwa namna ambayo inaonesha kwamba anasaidia, anashawishi au analazimisha ukahaba wake na mtu mwengine yeyote, au kwa ujumla, isipokuwa pale atakapoiridhisha mahakama kinyume na hivyo, vyenginevyo atachukuliwa kwamba anajua kuwa anaishi kwa kipato cha ukahaba.

Mtu mwanamke anayeishi kwa kipato cha ukahaba.

**125.** Mwanamke ambaye kwa kujua anaishi kwa kipato chake chote au sehemu ya kipato chake kutokana na ukahaba au amethibitika kuwa, kwa madhumuni ya kupata kipato, anadhibiti, anaelekeza au anashawishi harakati za kahaba kwa namna ambayo inaonesha kwamba anasaidia, anashawishi au analazimisha ukahaba wake na mtu fulani au na mtu yeyote, atakuwa ni mkosa.

Jengo linalotiliwa shaka na uwezo wa kupekua.

**126.** Iwapo hakimu ataona, kwa taarifa iliyotolewa kwake kwa kiapo kwamba kuna sababu ya msingi kutia shaka kwamba nyumba, sehemu ya nyumba au jengo inatumiwa na mwanamke au mtoto wa kike kwa madhumuni ya ukahaba, na kwamba mtu anayeishi humo au anayehudhuria katika nyumba hiyo mara kwa mara anaishi kwa kujua kipato chake chote au sehemu ya kipato chake ni cha ukahaba, au anadhibiti, anaelekeza au anashawishi harakati za kahaba, hakimu anaweza kutoa hati kumuidhinisha afisa wa polisi kuingia na kupekua nyumba hiyo na kumkamata mtu huyo.

Danguro.

**127.** Mtu yeyote ambaye:

(a) ameweka, anaendesha au anasaidia katika uendeshaji wa danguro;

(b) akiwa mpangaji, mkodishwaji au mkaazi, au mtu mwenye dhamana ya jengo, kwa kujua anaruhusu jengo hilo au sehemu ya jengo hilo kutumika kama danguro; au

(c) akiwa mkodishaji au mmiliki wa jengo, au wakala wa mkodishaji huyo au mmiliki huyo, anakodisha jengo hilo au sehemu ya jengo hilo kwa kujua kwamba jengo hilo au baadhi ya sehemu ya jengo hilo zinatumika au zitatumika kama danguro au kwa makusudi anashiriki katika kuendelea kutumia jengo hilo kama danguro,

atakuwa ni mkosa.

Njama ya kubaka.

**128.** Mtu yeyote anayekula njama na mtu mwengine kumshawishi mwanamke au mtoto wa kike, kwa njia za udanganyifu au kwa njia za ulaghai, kumruhusu mwanaume yeyote kumuingilia bila halali mwanamke huyo au mtoto huyo wa kike atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kujaribu kuwezesha kutoa mimba.

**129.** Mtu yeyote ambaye kwa nia ya kuwezesha kuharibika kwa mimba ya mwanamke au mtoto wa kike, ama mwanamke au mtoto wa kike huyo ana mtoto au hana mtoto, bila ya halali anampa au anasababisha mwanamke huyo au mtoto wa kike kula sumu au kitu chengine chenye madhara, au anatumia nguvu ya aina yoyote, au anatumia njia nyengine yoyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi na nne.

Kutoa mimba kwa mwanamke au mtoto wa kike.

**130.** Mwanamke au mtoto wa kike ambaye kwa nia ya kuwezesha kuharibika mimba yake bila ya halali anakula mwenyewe sumu au kitu chengine chenye madhara, au anatumia nguvu ya aina yoyote au anatumia njia nyengine yoyote, au anaruhusu kitu chochote hicho kuliwa au njia nyengine yoyote kutumika, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Kutoa dawa au kifaa cha kuwezesha kutoa mimba.

**131.** Mtu yeyote ambaye bila halali anampa au anamuwezesha mtu kitu chochote, huku akijua kwamba kinakusudiwa kutumika bila halali kuwezesha kuharibu mimba ya mwanamke au mtoto wa kike, ama ana mtoto au hana mtoto, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kujua umri wa mwanamke au mtoto wa kike si muhimu.

**132.** Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo, haitatiliwa maanani katika kesi ya kosa lolote lililofanywa kuhusiana na mwanamke au mtoto wa kike chini ya umri ulioainishwa, kwamba mshtakiwa hakujua kuwa mwanamke au mtoto wa kike alikuwa chini ya umri huo, au aliamini kuwa hakuwa chini ya umri huo.

Makosa ya kuingilia kinyume na maumbile.

**133.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamuingilia mtu kinyume na maumbile;

(b) anamuingilia mnyama au anaingiliwa na mnyama; au

(c) anamruhusu mtu mwanamme kumuingilia mwanamme au mwanamke kinyume na maumbile,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka thelathini.

Kujaribu kutenda kosa la kuingilia kinyume cha maumbile.

**134.** Mtu yeyote ambaye anajaribu kutenda kosa la kuingilia kinyume cha maumbile atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Shambulio la aibu kwa mtoto wa kiume.

**135.** Mtu yeyote ambaye bila ya halali na bila ya heshima anamshambulia mtoto wa kiume, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano.

Matendo ya usagaji.

**136.** Mwanamke au mtoto wa kike ambaye anatenda tendo la usagaji na mwanamke mwengine au mtoto wa kike mwengine, ama mfanyaji au mfanywaji, atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi.

Matendo ya aibu kubwa baina ya watu.

**137.**-(1) Mtu yeyote ambaye, hadharani au kwenye faragha, anatenda, au anashiriki kutenda, au anamuwezesha au anajaribu kumuwezesha mtu kutenda kitendo chochote cha aibu kubwa na mtu mwengine, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tatu lakini isiyozidi shilingi milioni tano.

(2) Endapo kosa hilo limetendwa na mtu mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi kwa mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi, na pia ataamriwa kulipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa mtu huyo aliyetendewa kosa kwa madhara ya mwili na kiakili aliyosababishiwa.

Utumiaji wa watoto kingono.

**138.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa kujua anamruhusu mtoto kubakia katika jengo lolote, kwa madhumuni ya kuwezesha mtoto huyo kutumiwa kingono au kushiriki katika aina yoyote ya shughuli ya kingono au katika maonesho yoyote machafu yasiyofaa au onesho;

(b) anatenda kama muwezeshaji wa mtoto kwa madhumuni ya kufanya maingiliano ya kingono au kwa aina ya udhalilishaji wa kingono au maonesho yasiyofaa au onesho;

(c) anamshawishi mtu kuwa mteja wa mtoto kwa ajili ya kufanya maingiliano ya kingono au kwa aina ya udhalilishaji wa kingono au maonesho yasiyofaa au onesho, kwa njia za kuchapisha au vyombo vyengine vya matangazo, matangazo ya mdomo au njia nyengine zinazofanana na hizo;

(d) anatumia fursa ya ushawishi wake, au uhusiano wake na mtoto, kuwezesha mtoto huyo kufanya maingiliano ya kingono au aina ya udhalilishaji wa kingono au maonesho yasiyofaa au onesho;

(e) anatishia, au anatumia nguvu dhidi ya mtoto, kumuwezesha mtoto huyo kufanya maingiliano ya kingono au aina ya udhalilishaji wa kingono au maonesho yasiyofaa au onesho; au

(f) anampa au anaahidi kumpa malipo, vitu au maslahi mengine mtoto au wazazi wake kwa nia ya kumuwezesha mtoto huyo kufanya maingiliano ya kingono au aina ya udhalilishaji wa kingono au maonesho yasiyofaa au onesho,

atakuwa ni mkosa wa kosa la utumiaji watoto kingono na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka ishirini.

Udhalilishaji mkubwa wa kingono.

**139.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa kujifurahisha kingono, anatenda tendo, kwa kutumia sehemu zake za siri au sehemu nyengine ya mwili wa binaadamu au kifaa kwenye tundu au sehemu ya mwili wa mtu mwengine yeyote, kikiwa ni kitendo ambacho hakihesabiki kuwa ni kubaka, atakuwa ametenda kosa la udhalilishaji mkubwa wa kingono iwapo atafanya hivyo katika mazingira yanayoendana na moja kati ya hali zifuatazo:

(a) bila ya ridhaa ya mtu huyo mwengine;

(b) kwa ridhaa ya mtu huyo mwengine pale ambapo ridhaa hiyo imepatikana kwa kutumia nguvu, vitisho au kutishia au kumtishia mtu huyo mwengine kumuua au kumuumiza au pale ambapo mtu huyo mwengine yupo kizuizini bila ya halali; au

(c) kwa ridhaa ya huyo mtu mwengine endapo ridhaa hiyo imepatikana wakati mtu huyo mwengine alikuwa hana akili timamu au alikuwa katika hali ya ulevi iliyotokana na kilevi au dawa yoyote, jambo au kitu.

(2) Mtu yeyote ambaye:

(a) ametenda kosa la udhalilishaji mkubwa wa kingono atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na tano lakini kisichozidi miaka thelathini, na atalipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa mtu ambaye ametendewa kosa kwa madhara aliyosababishiwa mtu huyo;

(b) ametenda kosa la udhalilishaji mkubwa wa kingono kwa mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano lakini kisichozidi miaka thelathini, na atalipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa mtu ambaye ametendewa kosa kwa madhara aliyosababishiwa mtu huyo.

Muungano wa watu wa jinsia moja.

**140.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anaingia au anaandaa muungano unaokusudiwa kuwa ndoa au vyenginevyo wa watu wa jinsia moja;

(b) anaesherehekea muungano na mtu mwengine wa jinsia moja unaokusudiwa kuwa ndoa au vyenginevyo; au

(c) anayeishi kama mume na mke na mtu mwengine wa jinsia moja,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Usumbufu wa kingono.

**141.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi, anamshambulia au kwa kutumia nguvu za kijinai, anamsumbua kingono mtu mwengine, au kwa kutumia maneno au vitendo, anasababisha maudhi au usumbufu wa kingono kwa mtu huyo mwengine, atakuwa ametenda kosa la usumbufu wa kingono; au

(b) kwa kukusudia kuchafua heshima ya mtu anatamka neno lolote, anatoa sauti yoyote au ishara, au anaonyesha kitu chochote ikijumuisha kiungo chochote cha kiume au cha kike, akikusudia kwamba neno hilo au sauti isikike, au ishara hiyo au kitu kionekane, na mtu huyo, au anaingilia faragha ya mtu, atakuwa ametenda kosa la usumbufu wa kingono,

na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili, na anaweza kuamriwa kulipa fidia ya kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa mtu aliyetendewa kosa kwa madhara aliyosababishiwa mtu huyo.

(2) Kwa kuondosha shaka, vishawishi vya awali vya kingono visivyokaribishwa kwa maneno au vitendo vinavyotumiwa na mtu mwenye mamlaka, katika sehemu ya kazi au sehemu nyengine yoyote, vitakuwa ni kosa la usumbufu wa kingono.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, kushambulia inaweza kujumuisha tendo lolote, ambalo halihesabiki kuwa ni kubaka.

(4) Mashtaka kwa kosa chini ya kifungu hiki hayataanzishwa au kuendelezwa endapo malalamiko yamefanywa na muathirika wakati wowote zaidi ya siku mia moja na themanini baada ya kutokezea kwa tukio linalounda kosa hilo.

Uzinifu.

**142.**-(1) Mtu mwanamme yeyote ambaye anamuingilia kingono mwanamke ambaye anajua au ana sababu ya kuamini kuwa ni mke wa mtu mwengine, bila ya ridhaa au ruhusa ya mume wake, ambapo kumuingilia huko hakuhesabiki kuwa ni kosa la kubaka, atakuwa ni mkosa.

(2) Mtu mwanamke yeyote ambaye anaruhusu kuingiliwa kingono na mtu mwanamme yeyote, ambaye anajua au ana sababu ya kuamini kuwa ni mume wa mtu mwengine, bila ya ridhaa au ruhusa ya mke wake, atakuwa ni mkosa.

Kufanya maingiliano ya kingono na maharimu.

**143.**-(1) Mtu yeyote ambaye anafanya maingiliano ya kingono na mtu mwengine, na ambapo anajua kuwa mtu huyo anayo aina yoyote ya mahusiano yaliyoorodheshwa katika Jadweli la Sheria hii, atakuwa ni mkosa.

(2) Iwapo mkosaji ni mtu mwanamme, mkosaji huyo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka ishirini na tano.

(3) Iwapo mkosaji ni mtu mwanamke, mkosaji huyo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(4) Iwapo itadaiwa kwenye taarifa au shtaka na ikathibitika kwamba mtu mwanamke ana umri chini ya miaka kumi na nane, mkosaji mwanamme atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(5) Iwapo itadaiwa kwenye taarifa au shtaka na ikathibitika kwamba mtu mwanamme ana umri chini ya miaka kumi na mbili, mkosaji mwanamke atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka ishirini.

(6) Iwapo mtu mwanamme anajaribu kutenda kosa lolote kati ya yaliyotajwa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.

(7) Iwapo mtu mwanamke anajaribu kutenda kosa lolote kati ya yaliyotajwa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu.

(8) Atakapotiwa hatiani, katika Mahakama yoyote, mtu yeyote mwanamme au mwanamke yeyote kwa kosa au kwa kujaribu kutenda kosa hilo chini ya kifungu hiki, dhidi ya mtoto wa kiume au mtoto wa kike mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, Mahakama itakuwa na mamlaka kumnyang'anya mkosaji mamlaka yote kwa mtoto huyo, na ikiwa mkosaji ni mlezi wa mtoto huyo, Mahakama itamuondolea mkosaji huyo mamlaka ya ulezi, na katika mazingira mengine yoyote kama hayo, itamteua mtu yeyote au watu kuwa mlezi au walezi wa mtoto huyo wakati wote akiwa mdogo au kwa kipindi kifupi.

(9) Mahakama Kuu inaweza, wakati wowote, kubadilisha au kutengua amri ya uteuzi wa mtu mwengine yeyote kama mlezi, au katika hali nyengine yeyote.

Idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

**144.** Mashtaka kwa kosa lolote chini ya kifungu cha 142 au 143 hayatafunguliwa bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kuweka wazi utambulisho wa muathirika.

**145.**-(1) Mtu yeyote ambaye, anachapisha au anatangaza jina au jambo lolote ambalo litakalowezesha kujulikana utambulisho wa mtu yeyote aliyetendewa kosa dhidi ya maadili chini ya Sheria hii amedaiwa au amepatikana kuwa ametenda kosa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na atalipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama.

(2) Hakuna chochote katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakachotumika kwa chapisho lolote au tangazo lolote la jina au jambo, ambalo litawezesha kujulikana utambulisho wa muathirika iwapo chapisho au tangazo hilo ni:

(a) kwa, au chini ya amri kwa maandishi ya mkuu wa kituo cha polisi au afisa wa polisi anayefanya upelelezi wa kosa hilo, na anayetenda kwa nia njema kwa ajili ya upelelezi huo;

(b) kwa, au pamoja na idhini ya maandishi ya muathirika; au

(c) ikiwa muathirika amekufa au ni mtoto au hana akili timamu, kwa au pamoja na idhini ya maandishi ya ndugu wa karibu wa muathirika,

idhini hiyo haitatolewa na ndugu wa karibu kwa mtu yeyote bila ya ruhusa ya mkuu wa kituo cha polisi na endapo muathirika ni mtoto, idhini hiyo itatolewa na hakimu wa Mahakama ya Watoto.

(3) Mtu yeyote ambaye anachapisha au anatangaza jambo lolote linalohusiana na shauri lolote mbele ya Mahakama kuhusu kosa lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, bila ya kwanza kupata idhini ya Mahakama hiyo, atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili na atalipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama.

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA NDOA NA MAHUSIANO YA KIFAMILIA

Ndoa ya hadaa.

**146.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na kwa udanganyifu anamfanya mwanamke yeyote au mtoto wa kike ambaye sio mke wake kisheria aamini kwamba ameolewa nae kihalali na anakaa naye kinyumba au anamwingilia kimwili mwanamke au mtoto wa kike huyo akiamini kuwa ni mume wake, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi.

Kufunga ndoa kinyume na Sheria.

**147.**-(1) Mtu yeyote ambaye, ana mume au mke aliye hai, anaingia kwenye ndoa ambayo ni batili kwa sababu ndoa hiyo imefanyika wakati mume wake au mke wake huyo yuhai, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

(2) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakitotumika kwa mtu ambaye ndoa yake na mume huyo au mke huyo imetangazwa na Mahakama yenye mamlaka kuwa ni batili.

(3) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakitotumika kwa mtu ambaye amefunga ndoa wakati mume au mke wake wa awali yuhai, iwapo mume au mke huyo, wakati wa ndoa iliyofuata, hajaonekana kwa kipindi cha miaka saba mfululizo, wala haujasikika uwepo wake kama yupo hai ndani ya kipindi hicho.

(4) Vifungu vidogo vya (1) na (3) vya kifungu hiki, havitatumika kwa mwanamme anayefunga ndoa kwa mujibu wa imani ya dini ya kiislamu.

Sherehe ya ndoa iliyofanyika kihadaa bila ya ndoa halali.

**148.** Mtu yeyote ambaye bila uaminifu au kwa nia ya kuhadaa anafunga ndoa, akijua kwamba hafungi ndoa hiyo kisheria, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

Ukatili kwa watoto.

**149.**-(1) Mtu yeyote ambaye, akiwa na mamlaka ya uhifadhi, uangalizi au utunzaji wa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, anamnyanyasa, anampuuza au anamtelekeza mtu huyo au anawezesha tohara kwa mtu huyo au anawezesha mtu huyo kushambuliwa, kunyanyaswa, kupuuzwa au kutelekezwa katika namna ambayo itapelekea kupata maumivu au madhara ya kiafya, ikijumuisha madhara au hasara ya kupoteza uoni au usikivu, mkono au mguu, au kiungo cha mwili au kuchanganyikiwa kiakili, atakuwa ametenda kosa la ukatili kwa watoto.

(2) Mtu yeyote ambaye, anatenda kosa la ukatili kwa watoto atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na tano au atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi na tano au adhabu zote mbili, na atalipa fidia kwa kiwango kitakachoamuliwa na Mahakama kwa mtu ambaye ametendewa kosa kwa madhara aliyosababishiwa mtu huyo.

Kutelekeza mtoto au mtu mwenye ulemavu.

**150.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mzazi au mlezi au mtu mwengine yeyote mwenye mamlaka kisheria ya utunzaji au usimamizi wa mtoto au wa mtu mwenye ulemavu, na ana uwezo wa kumkimu mtoto huyo au mtu mwenye ulemavu, kwa makusudi na bila ya sababu ya kisheria au ya msingi, anamtelekeza mtoto huyo au mtu huyo mwenye ulemavu, na anamuacha bila ya msaada, atakuwa ni mkosa.

Kupuuza kutoa chakula kwa mtoto au mtu mwenye ulemavu.

**151.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mzazi au mlezi au mtu mwengine mwenye mamlaka kisheria ya utunzaji, au usimamizi wa mtoto yeyote au mtu mwenye ulemavu, na mtoto huyo au mtu huyo mwenye ulemavu hawezi kujikimu yeye mwenyewe, anakataa au anapuuza kumpatia, akiwa na uwezo wa kufanya hivyo, chakula cha kutosha, mavazi, malazi na mambo mengine muhimu kwa mtoto huyo au mtu huyo mwenye ulemavu, ikapelekea kudhuru afya ya mtoto huyo au mtu huyo mwenye ulemavu, atakuwa ni mkosa.

Mwajiri kutompatia mwanafunzi au mwajiriwa wake mahitaji.

**152.** Mtu yeyote ambaye, anawajibika kisheria, akiwa ni mwajiri, kumpatia mwanafunzi anayejifunza kwa vitendo au mwajiriwa wake, kumpatia chakula, mavazi au malazi, kwa makusudi na bila ya sababu ya msingi, anakataa au anapuuza kumpatia vitu hivyo, au bila ya halali na kwa nia mbaya anafanya au anawezesha kupatikana madhara yoyote ya kimwili kwa mwanafunzi au mwajiriwa huyo na kwamba maisha ya mwanafunzi huyo au mwajiriwa huyo yako hatarini au kwamba afya yake imeshapata madhara au inaelekea kupata madhara ya kudumu, atakuwa ni mkosa.

Usafirishaji wa binaadamu.

**153.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anajihusisha na kitendo cha kununua, kuuza au kubadilishana mtu kwa fedha au kwa malipo mengine yoyote;

(b) kwa madhumuni ya kuendeleza, kuwezesha au kushawishi ununuzi au uuzaji au ubadilishanaji nafasi ya kulea mtu (kuasili) kwa fedha au kwa malipo mengine yoyote:

(i) anapanga kwa ajili ya, au anasaidia, mtoto kusafirishwa kwenda nje ya nchi bila ya idhini ya mzazi wake au mlezi wake kisheria;

(ii) anapata hati ya kiapo kutoka kwa mwanamke mja mzito kwa fedha au kwa malipo mengine yoyote, kwa ajili ya kumlea mtoto ambae bado hajazaliwa wa mwanamke huyo;

(iii) anaaajiri wanawake, mtoto wa kike au mwaname na mwanamke kwa ajili ya kuzaa watoto;

(iv) akiwa mtu anayehusika na uandikishaji wa vizazi, kwa kujua anaruhusu udanganyifu wa kumbukumbu yoyote ya kizazi au daftari la usajili;

(v) anajihusisha katika upatikanaji wa watoto kutoka hospitali, makaazi ya hifadhi kwa wanawake, zahanati, skuli za maandalizi, vituo vya matunzo ya watoto, au taasisi nyengine za matunzo ya watoto au vituo vya ustawi kwa fedha au malipo mengine au anawezesha upatikanaji wa mtoto kwa ajili ya kulelewa kutoka katika taasisi yoyote ya aina hiyo au kituo, kwa kumtisha mama au mtu mwengine yeyote, au mtoto kwa ajili ya kulelewa kutoka katika taasisi yoyote au kituo hicho; au

(vi) anajifananisha na mama au anasaidia katika kujifananisha,

atakuwa anatenda kosa la usafirishaji wa binaadamu na atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka ishirini au atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi Shilingi Milioni Ishirini au adhabu zote mbili.

Kuiba mtoto.

**154.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kumyang'anya mzazi, mlezi au mtu mwingine mwenye mamlaka kisheria ya uangalizi au usimamizi wa mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nane, kutoka mikononi mwake:

(a) kwa nguvu au kwa hadaa anamchukua au anamrubuni au anamzuia mtoto huyo; au

(b) anampokea au anamficha mtoto huyo, hali akijua kwamba mtoto huyo amechukuliwa au amerubuniwa kwa namna hiyo au kuzuiwa,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi.

(2) Itakuwa ni utetezi kwa kosa lolote miongoni mwa makosa katika kifungu hiki, kuthibitisha kwamba mshtakiwa alidai kwa nia njema kuwa ana haki ya kuwa nae mtoto huyo, au, iwapo mtoto huyo alizaliwa nje ya ndoa, mshtakiwa alidai ni mama wa mtoto huyo au alidai kuwa ni baba wa mtoto huyo.

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## MAUDHI NA MAKOSA DHIDI YA AFYA NA UTULIVU

Maudhi kwa jamii.

**155.**-(1) Mtu yeyote ambaye anatenda kitendo kisichoruhusiwa na sheria au anaacha kutekeleza wajibu wa kisheria na kwa sababu hiyo anasababisha madhara kwa jamii au hatari au maudhi, au anazuia au anasababisha usumbufu kwa jamii katika kutekeleza haki za jamii, atakuwa ametenda kosa linaloitwa "maudhi kwa jamii" na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Haijalishi kwamba kutenda au kuacha kutenda kunakolalamikiwa ni utulivu kwa idadi kubwa katika jamii kuliko kutenda au kuacha kutenda huko kunavyosumbua, na kwamba kutenda au kuacha kutenda huko kunarahisisha utekelezaji wa haki zao kisheria japo kwa sehemu tu ya jamii hiyo kunaweza kuonesha kwamba si maudhi kwa sehemu yoyote ya jamii.

Nyumba ya kamari.

**156.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) akiwa mmiliki au mkaazi, au mtumiaji wa nyumba, chumba au pahala na anafungua, anatunza au anatumia nyumba hiyo kwa madhumuni ya kuendeleza michezo isiyo halali katika nyumba hiyo; au

(b) akiwa mmiliki au mkaazi, au mtumiaji wa nyumba, chumba au pahala na kwa kujua na kwa makusudi anaruhusu nyumba hiyo kufunguliwa, kutunzwa au kutumiwa na mtu mwengine yeyote kwa ajili ya hayo yaliyotajwa katika aya ya (a);

(c) akiwa anatunza au anaendesha au kwa namna yoyote anasaidia katika uendeshaji wa biashara katika nyumba hiyo, chumba au sehemu inayofunguliwa, inayotunzwa au inayotumiwa kwa madhumuni hayo yaliyotajwa katika aya ya (a),

atahesabika kuwa anaweka nyumba maarufu ya kamari.

(2) Katika kifungu hiki "kamari" inajumuisha ruleti, michezo yote ya korokoro isipokuwa *"backgammon"*, michezo yote ya karata ambayo sio michezo ya kuongeza ujuzi tu, na mchezo wowote ambao fursa za kushinda hazipo kwa wachezaji wote, ikijumuisha mshika fedha au mtu mwengine au watu wengine wanaochezesha mchezo huo, au dhidi ya wanaochezesha kwa kuweka dau, kucheza au kubahatisha.

(3) Mtu yeyote ambaye anaweka nyumba maarufu ya kamari atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu.

(4) Mtu yeyote mbali ya watu waliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ambaye anakutwa katika nyumba maarufu ya kamari atachukuliwa, isipokuwa ikithibitika vyenginevyo, kuwa yupo pale kwa madhumuni ya kucheza kamari, atakuwa ni mkosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano kwa kosa la kwanza, na kwa kila kosa linafuata atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Saba au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili, au adhabu zote mbili.

Mashine za kamari.

**157.** Mtu yeyote ambaye anaingiza nchini au anamiliki mashine yoyote au kifaa chochote kwa madhumuni ya mchezo wa kamari, atakuwa ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Nne au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka minne au adhabu zote mbili.

Nyumba ya kuweka dau.

**158.**-(1) Nyumba, chumba, au pahala panapotumika kwa moja ya makusudio yafuatayo:

(a) kwa makusudio ya kuweka dau ndani yake baina ya watu wanaopumzika pahala hapo; na

(i) mmiliki, mkaazi, au mwangalizi wa pahala hapo, au mtu anayetumia pahala hapo;

(ii) mtu aliyeletwa au aliyeajiriwa na, au anayetenda kwa, au kwa niaba ya mmiliki huyo, mkaazi au mwangalizi au mtu anayetumia pahala hapo; au

(iii) mtu mwenye dhamana ya uangalizi au usimamizi, au katika hali yoyote anaendesha biashara ya pahala hapo; au

(b) kwa makusudio ya fedha yoyote au mali nyengine inayolipwa, au inayopokelewa ndani humo, na au kwa niaba ya mmiliki huyo yeyote, mkaazi, au mtu anayetumia pahala hapo, kama, au kwa malipo:

(i) kwa madhumuni ya kuhakikisha, kuchukua, ahadi, au makubaliano ya wazi wazi au kwa kumaanisha, kulipa au kutoa baadae fedha yoyote au mali nyengine kwa tukio lolote au uwezekano wa au kuhusiana na mashindano ya mbio za farasi, au mashindano ya mbio nyengine, mapigano, kamari, michezo au mazoezi; au

(ii) kwa ajili ya kuweka dhamana ya kumlipa au kulipwa na mtu mwengine fedha yoyote au mali nyengine kutokana na tukio hilo au uwezekano huo,

itaitwa nyumba maarufu ya kuweka dau.

(2) Mtu yeyote ambaye, akiwa mmiliki au mkaazi wa nyumba yoyote, chumba au pahala, kwa kujua na kwa makusudi anaruhusu ifunguliwe, iwekwe au itumike kama nyumba maarufu ya kuweka dau na mtu mwengine, au ana mamlaka ya kutumia au kuendesha, au anasaidia kuendesha biashara, ya nyumba maarufu ya kuweka dau, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka minne au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Nne au adhabu zote mbili.

(3) Hakuna chochote kilichoelezwa katika kifungu hiki kitakachokataza kisheria matumizi ya mashine ya kuhesabia dau lililowekwa kwa klabu inayotambuliwa na Serikali kisheria katika mkutano wowote wa hadhara, na ulioruhusiwa na Kamishna wa Polisi.

(4) Katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, "mashine ya kuhesabia dau" maana yake na inajumuisha chombo, mashine au kifaa, ambacho kikawaida kinajulikana kama mashine ya kuhesabia dau na chombo chengine chochote, mashine au kifaa chenye maumbile yanayofanana na hivyo, au mfumo wowote unaowezesha idadi yoyote ya watu kuweka dau baina yao kwa misingi inayofanana.

Bahati nasibu.

**159.**-(1) Mtu yeyote ambaye anafungua, anaweka au anatumia pahala popote kwa ajili ya kuchezesha bahati nasibu pasipoidhinishwa na Kamishna wa Polisi au afisa wa polisi mwenye cheo si chini ya Mrakibu wa Polisi ambaye amekasimiwa mamlaka na Kamishna wa Polisi kutoa idhini hiyo, atakuwa ni mkosa, na mtu ambaye kwa njia yoyote anakiuka au anashindwa kufuata masharti aliyopewa wakati alipopewa idhini hiyo kama ilivyotajwa hapo juu, atakuwa ni mkosa.

(2) Mtu yeyote anayechapisha au kutangaza, au anawezesha kuchapishwa au kutangazwa, tangazo au taarifa nyengine inayohusiana na bahati nasibu ambayo haijaidhinishwa au inayohusiana na uuzwaji wa tiketi au nafasi au hisa katika tiketi yoyote au nafasi katika bahati nasibu yoyote ambayo haijaidhinishwa, atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tano.

(3) Masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, hayatatumika kwa tangazo lolote au taarifa ambayo inachapishwa au inatangazwa kwa madhumuni tu ya kuipa taarifa jamii matokeo ya bahati nasibu yoyote isiyoidhinishwa.

(4) Katika kifungu hiki "bahati nasibu" inajumuisha mfumo wowote au kifaa kwa ajili ya uuzaji, utoaji zawadi, uondoshaji au usambazaji wa mali yoyote unaotegemea au unaoamuliwa kwa mgao au nafasi, ama kwa kurusha au kutupa kete,

au kwa kuandika tiketi, kadi, maeneo, nambari au picha, au kwa njia ya ringi au mnyama aliyefundishwa au vyenginevyo.

(5) Pale mtu anapotiwa hatiani kwa kutenda kosa chini ya kifungu hiki, Mahakama inaweza, zaidi ya adhabu au badala ya adhabu ambayo inaweza kutolewa, kuamuru kutaifishwa na Serikali kifaa chochote au kitu kilichotumika kuhusiana na bahati nasibu ambayo hatia imepatikana.

Maana ya mtunza jengo.

**160.** Mtu yeyote ambaye anaonekana, anatenda au anajifanya kama mkuu, au kama mtu mwenye dhamana ya uangalizi au uendeshaji wa nyumba hiyo, chumba, mkusanyiko wa vyumba au pahala kama ilivyotajwa kwenye vifungu 157, 158 na 159 atachukuliwa kuwa ni mtunzaji wa vitu hivyo, ama akiwa ni mtunzaji halisi au sio mtunzaji halisi.

Kusafirisha machapisho machafu.

**161.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa madhumuni ya, au kwa njia ya biashara, au kwa madhumuni ya kusambaza au maonesho ya hadharani, anafanya, anazalisha, au anayo katika hifadhi yake moja ya au zaidi ya lolote katika maandishi machafu, michoro, machapisho, picha, jambo lililochapishwa, picha, bango, alama, picha za mnato, picha za sinema au vitu vyengine vyovyote vichafu, au kitu chengine chochote chenye lengo la kuharibu maadili;

(b) kwa madhumuni mengine yoyote yaliyotajwa katika aya ya (a) anaingiza, anawasilisha au anasafirisha, au anasababisha kuingizwa, kuwasilishwa au kusafirishwa, mambo hayo yoyote au vitu vyovyote, au katika hali ya namna yoyote ambayo anaweka chochote katika hivyo kwenye mzunguko;

(c) anafanya au anashiriki katika biashara yoyote, ama hadharani au faragha, kuhusiana na mambo au vitu hivyo, au anajishughulisha katika mambo hayo au vitu hivyo kwa namna yoyote ile, au anasambaza chochote katika hivyo, au anaonesha hadharani chochote katika hivyo, au anafanya biashara ya kukodisha chochote katika hivyo;

(d) anatangaza au anafanya ijulikane kwa njia yoyote ile kwa dhamira ya kusaidia mzunguko wa, au usafirishaji katika, mambo hayo yoyote au vitu hivyo vyovyote, kwamba mtu anayejishughulisha katika moja ya vitendo vyovyote vilivyotajwa katika kifungu hiki, au anatangaza, au anafanya ijulikane vipi, au kutoka kwa nani, mambo

hayo yoyote au vitu hivyo vyovyote vinaweza kupatikana ama moja kwa moja au sio moja kwa moja; au

(e) anaonyesha hadharani onesho lolote lisilofaa au kazi ya kisanii au onesho au kazi ya kisanii inayolenga kuharibu maadili;

(f) katika kituo chochote kinachotoa huduma ya mtandao ambacho kiko wazi kwa jamii, akiwa mmiliki anaruhusu mtu yeyote kuonesha vitu vichafu kutoka kwenye mtandao, au akiwa mtumiaji anaonesha vitu vichafu kutoka kwenye mtandao,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka sita au atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tatu lakini isiyozidi Shilingi Milioni Sita.

(2) Iwapo, kuhusiana na makosa yoyote yaliyoainishwa katika aya za (a), (b), (c), (d) na (f) za kifungu kidogo cha (1), kitu chochote ambacho ni kiini cha makosa hayo kinapotendeka Zanzibar, kutendeka huko kutatosha kumfanya mtu huyo anayetuhumiwa kwa kosa hilo kushtakiwa Zanzibar.

(3) Mahakama inaweza, kwa maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kuamuru uteketezaji wa jambo lolote au kitu chochote kichafu ambacho kifungu hiki kinahusika, ama mtu yeyote anaweza kuwa ameshatiwa hatiani au anaweza kuwa hajatiwa hatiani chini ya masharti ya kifungu hiki kutokana na jambo hilo au kitu hicho kichafu.

Matendo machafu.

**162.** Mtu yeyote ambaye, kwa kuudhi wengine anafanya tendo lolote chafu hadharani, atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini, au adhabu zote mbili.

Watu wavivu na wenye tabia mbaya.

**163.** Mtu yeyote kati ya watu wafuatao ambaye:

(a) kahaba mzoefu anayefanya kitendo cha aibu au kisichofaa mahala popote hadharani;

(b) anazurura au anakaa popote hadharani kuomba au kukusanya sadaka, anasababisha au anawezesha au anashajihisha mtoto yeyote au watoto kufanya hivyo;

(c) anacheza, michezo ya kamari kwa ajili ya kupata fedha au kitu chenye thamani ya fedha, katika mahala popote hadharani;

(d) katika mahala popote hadharani anafanya yeye mwenyewe mambo yanayopelekea kusababisha uvunjifu wa amani;

(e) katika mahala popote hadharani anakutikana amelewa na anafanya fujo au mambo mabaya au hawezi kujihudumia yeye mwenyewe;

(f) bila ya sababu ya msingi, anafanya hadharani tendo lolote lisilofaa;

(g) katika mahala popote hadharani, anashawishi kwa ajili ya mambo yaliyo kinyume na maadili;

(h) anazurura ovyo na anajitahidi kuonesha majeraha au ulemavu ili apate au akusanye sadaka; na

(i) ni muhuni au anafanya jambo katika namna ambayo linapelekea kwenye tendo lisilofaa au miongoni mwa lolote katika haya,

atachukuliwa kuwa ni mtu mvivu na mwenye tabia mbaya, na atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili au atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili.

Wakorofi na wazururaji.

**164.** Yeyote miongoni mwa watu wafuatao ambaye:

(a) anazurura kama mchukuaji au mkusanyaji sadaka, au anajitahidi kuwezesha upatikanaji wa misaada ya hali yoyote au aina yoyote, kwa kisingizio cha uongo au udanganyifu;

(b) ni mtu anayetuhumiwa au anayesifika kwa wizi ambaye hana njia zinazoonekana za kujikimu na hawezi kutoa maelezo mazuri kuhusiana na yeye mwenyewe;

(c) anakutwa ndani, au katika au karibu na jengo au kwenye barabara au barabara kuu au pahala pengine popote karibu na sehemu hizo au mahala popote hadharani katika wakati na katika mazingira yanayopelekea kuthibitisha kwamba mtu huyo yupo hapo kwa makusudio ya kufanya mambo yasiyo halali au mabaya;

(d) anaonekana kuwepo katika eneo lisiloruhusiwa ambalo linaweza kila mara kutangazwa hivyo na mamlaka ya Serikali za Mitaa au mamlaka nyengine yoyote, ama mtu huyo amelala au vyenginevyo, na ambaye anashindwa kutoa sababu za msingi za kuwepo hapo wakati huo,

atahesabiwa kuwa ni mkorofi na mzururaji, na atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu lakini kisichozidi miaka miwili au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili.

Makosa dhidi ya sare za kijeshi.

**165.**-(1) Mtu yeyote ambaye, asiyekuwa anafanya kazi katika jeshi la ulinzi au majeshi mengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Idara Maalum anavaa, bila ya ruhusa ya mamlaka ya kisheria, sare za yoyote kati ya majeshi hayo au Idara Maalum au nguo yoyote yenye muonekano au ina chochote katika vyeo au alama zinazoashiria sare hiyo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Moja.

(2) Hakuna chochote katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitakachomzuia mtu kuvaa sare yoyote au nguo katika mchezo jukwaani unaochezwa katika pahala popote ambapo michezo ya jukwaani kisheria inaweza kuchezwa hadharani, au katika ukumbi wa mziki au michezo ya sarakasi, au katika maigizo ya kijeshi bila ya dhamira mbaya.

(3) Mtu ambaye, bila ya halali anavaa sare ya yoyote kati ya majeshi au Idara Maalum zilizotajwa awali, au nguo yoyote yenye muonekano au ina chochote katika vyeo au alama zinazoashiria sare hiyo, kwa namna ambayo au katika mazingira yanayopelekea kuleta dharau kwa sare hiyo, au anamuajiri mtu mwengine yeyote kuvaa sare hiyo au nguo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini.

(4) Mtu yeyote ambaye, asiyekuwa katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali au asiyekuwa awali alipata ruhusa ya maandishi kutoka kwa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo, anaingiza nchini au anauza au anazo katika hifadhi yake kwa ajili ya kuuza aina yoyote ya sare hiyo au nguo kama ilivyotajwa katika kifungu hiki, au vifungo au beji zinazohusika na sare hizo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

(5) Hakuna chochote katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, kitakachochukuliwa kukataza kuwa nayo sare yoyote ya aina hizo au nguo kwa mtu ambaye, alishatumikia majeshi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Idara Maalum za Serikali.

(6) Endapo mtu ameshatiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki, sare, nguo, kifungo, beji au kitu chengine kinachohusiana na kosa lililokwishatendwa kitataifishwa, isipokuwa kama Mahakama itaamuru vyenginevyo.

Kitendo cha uzembe kinachoweza kueneza maambukizo.

**166.** Mtu yeyote ambaye, bila halali au kwa uzembe anatenda kitendo chochote ambacho, na anajua au ana sababu ya kuamini kinaweza kueneza maambukizo ya maradhi yoyote ya hatari kwa maisha, atakuwa ni mkosa.

Kuchafua maji.

**167.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anaharibu au anachafua maji ya chemchem yoyote ya jamii au hodhi, kiasi cha kuyafanya maji hayo yasifae kwa matumizi ya kawaida yanayokusudiwa, atakuwa ni mkosa.

Kuchafua hewa.

**168.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anachafua hewa ya pahala kiasi cha kuifanya hewa hiyo iwe na madhara kwa afya ya watu kwa ujumla wanaokaa au kufanya kazi katika maeneo jirani na mahali hapo au wanaopita njia, atakuwa ni mkosa.

Biashara mbaya.

**169.** Mtu yeyote ambaye, kwa madhumuni ya biashara au vyenginevyo, anafanya kelele kubwa au anasababisha harufu mbaya au inayochukiza katika pahala na mazingira yanayowakasirisha idadi kubwa ya watu wanaotumia haki zao za kawaida, atakuwa ametenda kosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kutotii amri ya karantini.

**170.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua anapinga amri yoyote iliyotolewa na ikatangazwa na Serikali kwa ajili ya kuweka chombo chochote katika hali ya karantini, au kwa ajili ya kusimamia muingiliano wa vyombo katika hali ya karantini kwenye ufukwe au muingiliano wa chombo na vyombo vyengine katika hali ya karantini, au kwa ajili ya kusimamia muingiliano baina ya maeneo ambayo maradhi ya kuambukiza yameibuka na maeneno mengine, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili.

Adhabu ya maudhi kwa jamii.

**171.** Mtu yeyote ambae anatenda kosa la maudhi kwa jamii katika hali yoyote ambayo adhabu yake haijaainishwa katika Sheria hii, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kuendelea kwa maudhi.

**172.** Mtu yeyote ambaye anarejea au anaendeleza maudhi kwa jamii, akiwa ameshaonywa na mtumishi yeyote wa umma mwenye mamlaka ya kisheria kutoa katazo hilo kutorudia au kuendeleza maudhi hayo, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili.

Kuchanganya chakula na kitu chengine.

**173.** Mtu yeyote ambaye anachanganya chakula au kinywaji na kitu chengine chochote, kiasi cha kukifanya chakula hicho au kinywaji hicho kiwe na madhara kwa kutumika kama chakula au kinywaji, kwa nia ya kuuza kama chakula au kinywaji, hali akijua kwamba kuna uwezekano mkubwa kuwa kitu hicho kitauzwa kama chakula au kinywaji, atakuwa ni mkosa.

Kuuza chakula chenye madhara.

**174.** Mtu yeyote ambaye anauza, anatoa au anatangaza kwa ajili ya kuuza, kama chakula au kinywaji, kitu chochote ambacho kimefanywa au kimekuwa kina madhara, au kiko katika hali isiyofaa kwa chakula au kinywaji, akijua au akiwa na kila sababu za

kuamini kwamba chakula au kinywaji hicho kina madhara kama chakula au kinywaji, atakuwa ni mkosa.

Kuchanganya dawa.

**175.** Mtu yeyote ambaye anachanganya dawa yoyote au mchanganyiko maalum wa dawa katika hali ambayo itapunguza nguvu au kubadilisha matumizi ya dawa hizo au mchanganyiko huo maalum wa dawa, au kuifanya iwe na madhara, kwa kukukusudia kwamba itauzwa au itatumika kwa ajili ya matibabu, kama vile haijachanganywa, atakuwa ni mkosa.

Kuuza dawa zilizochanganywa.

**176.** Mtu yeyote ambaye anachanganya dawa yoyote au mchanganyiko maalum wa dawa katika hali ambayo inapunguza nguvu au inabadilisha matumizi yake, au kuifanya iwe na madhara, anauza dawa hiyo au mchanganyiko huo maalum wa dawa, au anatoa au anatangaza kuuza, au anatoa kutoka katika zahanati yoyote kwa ajili ya matibabu kama vile haijachanganywa, au anawezesha kutumika kwa ajili ya matibabu na mtu yeyote bila kujua kwamba imechanganywa, atakuwa ni mkosa.

## SEHEMU YA KUMI NA SITA
## KUUA, KUUA BILA YA KUKUSUDIA
## NA KUUA MTOTO MCHANGA

Kuua bila ya kukusudia.

**177.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa kutenda bila halali au kuacha kutenda bila halali anasababisha kifo cha mtu mwengine, atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "kuua bila kukusudia".

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kuacha kutenda bila halali" ni kuacha kutenda kiasi cha kufikia uzembe wa kulaumiwa katika kutekeleza wajibu unaokusudia kulinda uhai na afya, ama kutokutenda huko kumefuatana au hakukufuatana na nia ya kusababisha kifo au madhara ya mwili.

Adhabu ya kuua bila ya kukusudia.

**178.** Mtu yeyote ambaye anatenda kosa la kuua bila ya kukusudia atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuua kwa kukusudia.

**179.** Mtu yeyote ambaye akiwa na nia ovu anasababisha kifo cha mtu mwengine kwa kutenda bila ya halali au kwa kuacha kutenda bila ya halali, atakuwa ni mkosa wa kosa la kuua kwa kukusudia.

Adhabu ya kuua kwa kukusudia.

**180.** Mtu yeyote ambaye ametiwa hatiani kwa kosa la kuua kwa kukusudia atapewa adhabu ya kifo.

Nia ovu.

**181.** Nia ovu itachukuliwa kuwa imethibitishwa kwa ushahidi unaothibitisha yoyote au zaidi ya moja ya mazingira yafuatayo:

(a) nia ya kusababisha kifo cha au nia ya kusababisha madhara makubwa kwa mtu yeyote, ama mtu huyo ni mtu hasa aliyeuliwa au mtu mwengine;

(b) kujua kwamba kutenda au kuacha kutenda kunakosababisha kifo kunaweza kusababisha kifo cha au madhara makubwa kwa mtu yeyote, ama mtu huyo ni mtu hasa aliyeuliwa au mtu mwengine, ijapokuwa kujua huko kunafuatana na kutokujali ama kifo au madhara makubwa ya kimwili yanasababishwa au vyenginevyo, au kwa kutaraji kwamba kusingesababisha madhara makubwa ya kimwili au kifo;

(c) nia ya kutenda kosa; au

(d) nia kwa kutenda au kwa kuacha kutenda kwa kuwezesha kutoroka au kukimbia kutoka katika kizuizi kwa mtu yeyote ambaye ameshatenda au amejaribu kutenda kosa.

Kuua kwa kukasirishwa.

**182.** Endapo mtu yeyote ambaye bila ya halali atamuua mtu mwengine kutokana na mazingira ambayo, isipokuwa kutokana na masharti ya kifungu hiki, yangetengeneza kosa la kuua kwa makusudi, anafanya kitendo ambacho kitasababisha kifo akiwa katika joto la hasira lililosababishwa na kukasirishwa ghafla kama kutakavyotafsiriwa baadae ndani ya Sheria hii, na kabla ya kuwepo muda wa hasira zake kupungua, atakuwa ni mkosa wa kuua bila ya kukusudia.

Maana ya kukasirishwa.

**183.**-(1) Neno "kukasirishwa" maana yake ni na linajumuisha, isipokuwa kama itakavyoelezwa baadae katika sheria hii, kitendo chochote bila halali au matusi ya namna ambayo yanaweza kupelekea, wakati yanapotolewa kwa mtu wa kawaida, au mbele ya mtu wa kawaida kwa mtu mwengine ambaye yupo katika uangalizi wake wa karibu, au kwake ana uhusiano wa kindoa, wa kiuzawa, wa kifamilia, au wa kindugu, au katika uhusiano wa muajiri au muajiriwa, kumnyima uwezo wa kujidhibiti yeye mwenyewe na kumshawishi yeye kutenda shambulio la aina ambayo mtu anaeshtakiwa amelitenda kwa mtu ambaye ametenda kitendo cha kukasirisha au ametoa matusi ya kukasirisha.

(2) Pale tendo la kukasirisha limefanywa au matusi ya kukasirisha yametolewa na mtu mmoja kwa mwengine, au mbele ya mtu mwengine kwa mtu ambaye yuko chini ya uangalizi wa karibu wa mtu huyo mwengine, au kwake mtu huyo ambaye yuko chini ya uangalizi wa karibu ana uhusiano wa aina yoyote ule kama ilivyokwishatajwa, mtu aliyetenda tendo la kukasirisha au aliyetoa matusi ya kukasirisha atahesabika kwamba amemkasirisha mtu ambaye yuko chini ya uangalizi wa karibu kwa ajili ya kufanya shambulio.

(3) Kitendo cha halali sio kitu cha kumkasirisha mtu yeyote kufanya shambulio.

(4) Kitendo ambacho mtu atakifanya baada ya kupewa ushawishi na mtu mwengine ili kumshawishi yeye kufanya kitendo na baadae kukifanya ndio kinga kwa kufanya shambulio hakitahesabiwa kuwa kitu cha kukasirisha kwa mtu huyo mwengine kwa ajili ya kufanya shambulio.

(5) Kukamata kusiko halali sio kitu cha kukasirisha kwa ajili ya kufanya shambulio, lakini kunaweza kuwa ushahidi wa kitu cha kukasirisha kwa mtu anayejua kutokuwepo kwa uhalali huo.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "mtu wa kawaida" maana yake ni mtu wa kawaida katika jamii ambayo mtuhumiwa anahusika nayo.

Maana ya kusababisha kifo.

**184.** Mtu atachukuliwa kuwa amesababisha kifo cha mtu mwengine ijapokua kitendo chake sio sababu ya karibu au sio sababu ya pekee ya kifo katika moja ya mazingira yafuatayo:

(a) ikiwa atampatia madhara ya kimwili mtu mwengine na kutokana na madhara hayo mtu huyo mwengine atafanyiwa upasuaji au matibabu ambayo yatasababisha kifo; katika hali hii haijalishi ama matibabu yalikuwa sahihi au yalikosewa, iwapo yalifanywa kwa nia njema na kwa ujuzi wa kawaida na uzoefu; lakini mtu aliyesababisha madhara hayo hatachukuliwa kuwa amesababisha kifo ikiwa matibabu ambayo ndiyo yalikuwa sababu ya karibu hayakufanywa kwa nia njema au yalifanywa bila ujuzi wa kawaida au uzoefu;

(b) ikiwa mtu atampatia madhara ya kimwili mtu mwengine ambayo yasingesababisha kifo kama mtu huyo aliyedhuriwa angepatiwa upasuaji sahihi au matibabu sahihi au angefuata tahadhari zinazofaa kuhusu aina yake ya maisha;

(c) ikiwa kwa kutumia nguvu au vitisho anasababisha kwamba mtu mwengine kufanya kitendo kinachosababisha kifo cha mtu huyo, kitendo hicho kikiwa ni njia ya kuepuka nguvu na vurugu ambalo kutokana na mazingira vingeonekana vya kawaida kwa mtu ambaye kifo chake kimesababishwa;

(d) ikiwa kwa kutenda au kuacha kutenda anaharakisha kifo cha mtu anayesumbuliwa na maradhi yoyote au madhara ambayo mbali na kutenda huko au kuacha kutenda yangemsababishia kifo; au

(e) ikiwa kutenda kwake au kuacha kutenda kusingesababisha kifo isipokuwa kumefuatana na kutenda au kuacha kutenda kwa mtu aliyeuliwa au kutenda au kuacha kutenda kwa watu wengine.

Wakati mtoto anapochukuliwa kuwa mtu.

**185.** Mtoto anakuwa mtu anayeweza kuuliwa wakati anapozaliwa kikamilifu akiwa hai kutoka katika mwili wa mama yake, ama amevuta pumzi au hakuvuta, na ama anaweza kujisukuma mwenyewe au hawezi, na ama uzi wa kitovu umeshakatwa au bado.

Ukomo wa muda wa kifo.

**186.-**(1) Mtu hatachukuliwa kuwa amemuua mtu mwengine ikiwa kifo cha mtu huyo hakijatokea ndani ya mwaka mmoja na siku moja ya sababu ya kifo.

(2) Kipindi hicho kinahesabiwa kikijumuisha siku ambayo kitendo kisicho halali kilichochangia sababu ya kifo kilipotendwa.

(3) Pale sababu ya kifo ni kuacha kufuata au kuacha kutekeleza wajibu, kipindi hicho kinahesabiwa kikijumuisha siku ambayo kitendo kilichoachwa kimesitishwa.

(4) Pale sababu ya kifo ni sehemu ya kitendo kisicho halali, na ni sehemu ya kuacha kufuata au kutekeleza wajibu, kipindi kinahesabiwa kikijumuisha siku ambayo kitendo cha mwisho kisicho halali kilifanywa au siku ambayo kitendo kilichoachwa kimesitishwa, chochote kati ya hivyo kilichokuja mwisho.

Kuua mtoto mchanga.

**187.** Endapo mwanamke au mtoto wa kike, kwa kitendo chochote kwa makusudi au kwa kuacha kutenda kwa makusudi, anasababisha kifo cha mtoto wake akiwa chini ya umri wa miezi kumi na mbili, lakini wakati wa kitendo hicho au kuacha kutenda huko mezania ya akili yake ilikuwa inasumbuliwa kwa sababu hakuwa amepona sawasawa kutoka katika athari ya kumzaa mtoto huyo au kwa sababu ya athari ya kunyonyesha baada ya kumzaa mtoto huyo, pia, bila ya kujali kwamba mazingira yalikuwa kwamba isipokuwa kwa kifungu hiki kosa hilo lingehesabika kuua kwa kukusudia, atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa kuua mtoto mchanga, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

## SEHEMU YA KUMI NA SABA
## WAJIBU KUHUSIANA NA HIFADHI YA MAISHA NA AFYA

Jukumu la mtu anayemsimamia mtu mwengine.

**188.** Mtu atawajibika akiwa ana dhamana ya kusimamia mtu mwengine ambaye huyo anayesimamiwa hana uwezo kwa sababu ya umri, maradhi, upungufu wa akili, kuwepo kizuizini au kwa sababu nyengine yoyote akijiondosha mwenyewe katika usimamizi huo, na ambaye hana uwezo wa kujihudumia mwenyewe kwa mambo muhimu ya maisha, iwapo usimamizi huo ni kwa mujibu wa mkataba, au kwa mujibu wa sheria, au umetokana na sababu ya kitendo chochote, ama kipo kisheria au bila ya sheria, cha mtu huyo mwenye usimamizi huo, kutoa kwa mtu huyo mwengine mambo

muhimu ya maisha; na mtu huyo mwenye dhamana ya usimamizi atachukuliwa kuwa amesababisha matokeo yoyote ambayo yanaathiri vibaya maisha au afya ya mtu huyo mwengine kwa sababu tu ya kutokutenda wajibu huo.

Wajibu wa kiongozi wa familia.

**189.** Mtu atawajibika akiwa kiongozi wa familia, ana dhamana ya uangalizi wa mtoto aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane, akiwa ni mmoja wa watu wa nyumbani kwake, kumpatia mtoto huyo mahitaji ya lazima ya maisha; na mtu huyo mwenye dhamana ya uangalizi atachukuliwa kuwa amesababisha matokeo yoyote ambayo yanaathiri vibaya maisha au afya ya mtoto huyo kwa sababu tu ya kutokutenda wajibu huo, ama mtoto huyo hawezi kujisaidia au anaweza kujisaidia.

Wajibu wa mwajiri.

**190.** Mtu atawajibika akiwa mwajiri ambaye ameingia mkataba wa kutoa mahitaji ya lazima ya chakula, mavazi, au malazi kwa mwajiriwa yeyote au mwanafunzi aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane kumpatia vitu hivyo; na mwajiri huyo atachukuliwa kuwa amesababisha matokeo yoyote ambayo yanaathiri vibaya maisha au afya ya mwajiriwa au mwanafunzi huyo kwa sababu tu ya kutokutenda wajibu huo.

Wajibu wa watu wanaofanya vitendo vya hatari au wenye dhamana ya vitu vya hatari.

**191.**-(1) Mtu atawajibika akiwa, isipokuwa katika hali ya dharura, anachukua madaraka ya kusimamia utabibu wa kupasua au wa kutoa dawa kwa mtu mwengine yeyote, au kufanya kitendo kingine chochote halali ambacho ni au kinaweza kuwa ni hatari kwa maisha ya mwanadamu au afya, kuwa na ujuzi unaofaa na kutumia uangalifu wa kutosha katika kufanya kitendo hicho; na mtu huyo atachukuliwa kama amesababisha matokeo yoyote ambayo yanaathiri vibaya maisha au afya ya mtu huyo kwa sababu tu ya kuacha kuzingatia au kutekeleza wajibu huo.

(2) Mtu atawajibika akiwa ana dhamana ya uangalizi au udhibiti wa kitu chochote kikiwa chenye uhai au kisicho hai, na ama kinatembea au kimetulia, kwa hali ambayo kwamba, pasipokuwa na uangalifu au tahadhari katika matumizi au matunzo yake, uhai, usalama au afya ya mtu yeyote inaweza kuwa katika hatari, kutumia uangalifu wa kutosha na kuchukua tahadhari ya kutosha kuepuka hatari hiyo; na mtu huyo atachukuliwa amesababisha matokeo yoyote ambayo yanaathiri vibaya maisha au afya ya mtu huyo kwa sababu tu ya kuacha kutekeleza wajibu huo.

Adhabu kwa kushindwa kutimiza wajibu.

**192.** Mtu yeyote ambaye anashindwa kutekeleza wajibu wake chini ya masharti ya sehemu hii, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni moja au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA KUMI NA NANE
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KUUA KWA KUKUSUDIA NA KUJIUA

Kujaribu bila halali kusababisha kifo.

**193.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anajaribu bila halali kusababisha kifo cha mwengine; au

(b) kwa makusudi bila halali anasababisha kifo cha mwengine, anafanya kitendo chochote, au anaacha kutenda kitendo chochote ambacho ni wajibu kwake kukitenda, kutenda huko au kuacha kutenda kukawa katika hali ambayo kunaweza kuhatarisha maisha ya mwanadamu,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kusaidia baada ya kutendeka kosa la kuua kwa kukusudia.

**194.** Mtu yeyote ambaye anasaidia baada ya kutendeka kwa kosa la kuua kwa kukusudia, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka saba.

Kutishia kwa maandishi kuua kwa kukusudia.

**195.** Mtu yeyote ambaye, kwa kujua maudhui yaliyopo ndani yake, moja kwa moja au vyenginevyo anasababisha mtu yeyote kupokea maandishi yoyote ya kutishia kumuua mtu yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kula njama ya kuua kwa makusudi.

**196.** Mtu yeyote ambaye, anakula njama na mtu mwengine yeyote kumuua mtu, ama mtu huyo anayetaka kuuliwa yumo ndani ya Zanzibar au popote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kusaidia kujiua.

**197.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anasababisha mtu mwengine ajiuwe; au

(b) anamshauri mtu mwengine ajiuwe na akamshawishi mtu huyo kufanya hivyo; au

(c) anamsaidia mtu mwengine ajiuwe,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kujaribu kujiua.

**198.** Mtu yeyote ambaye anajaribu kujiua mwenyewe atakuwa ni mkosa.

Kuficha kuzaliwa kwa mtoto.

**199.** Mtu yeyote ambaye, pale ambapo mwanamke au mtoto wa kike anazaa mtoto, anajitahidi, kwa njia yoyote ya siri kutupa maiti ya mtoto huyo, kuficha kuzaliwa kwa mtoto, ama mtoto huyo alikufa kabla ya, wakati wa, au baada ya kuzaliwa, atakuwa ni mkosa.

Kuharibu mtoto.

**200.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo hiki, mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kuharibu maisha ya mtoto ambaye anaweza kuzaliwa akiwa hai, kwa kitendo chochote cha makusudi anasababisha mtoto huyo kufariki kabla hajawa na maisha ya kutomtegemea mama yake, atakuwa ni mkosa wa kosa la kuharibu mtoto, na atapewa adhabu akitiwa hatiani ya kifungo cha maisha.

(2) Haitakuwa ni kosa chini ya kifungu hiki ikiwa itathibitika kwamba kitendo kilichosababisha kifo cha mtoto kimefanywa kwa nia njema na daktari aliyepo kwenye hospitali ya Serikali kwa ajili tu ya kulinda maisha ya mama na ukweli kwamba kitendo hicho kilichofanywa kimeungwa mkono na cheti kilichosainiwa na jopo la madaktari wengine angalau wawili katika hospitali ya Serikali au hospitali iliyosajiliwa chini ya Sheria ya (Usimamizi wa) Hospitali Binafsi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, ushahidi kwamba mwanamke au mtoto wa kike alikuwa katika wakati huo ana ujauzito wa kipindi cha wiki ishirini na nane au zaidi, ni ushahidi wa awali unaothibitisha kwamba alikuwa ana ujauzito wa mtoto ambaye angeweza kuzaliwa akiwa hai.

Kuficha mpango wa kutenda kosa.

**201.**-(1) Mtu yeyote anayekusudia kuwezesha au anajua kuwa kuna uwezekano kwamba atawezesha kufanyika kosa lenye adhabu ya kifo, au kifungo cha maisha, kwa makusudi anaficha, kwa kutenda au kuacha kutenda bila halali, kuwepo kwa mpango huo wa kutenda kosa au anatoa maelezo yoyote ambayo anajua kuwa ni ya uongo kuhusu mpango huo, endapo kosa hilo limetendeka, mtu huyo atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba, au kama kosa halikutendeka, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

(2) Mtu yeyote anayekusudia kuwezesha au anajua kuwa kuna uwezekano kwamba atawezesha kufanyika kosa lenye adhabu ya kifungo, kwa makusudi anaficha, kwa kutenda au kuacha kutenda bila halali, kuwepo kwa mpango wa kutenda kosa hilo au anatoa maelezo yoyote ambayo anajua kuwa ni ya uongo kuhusu mpango huo, endapo kosa limetendeka, mtu huyo atapewa adhabu ya kifungo cha mwaka mmoja au, kama kosa halikutendeka, atapewa adhabu ya kifungo cha miezi sita.

## SEHEMU YA KUMI NA TISA
## MAKOSA YA KUHATARISHA MAISHA AU AFYA

Kumzuia mtu kujihami ili kosa litendeke.

**202.** Mtu yeyote ambaye, kwa njia yoyote inayopelekea kuzuia pumzi, kumkosesha mtu hewa au kukaba koo, na kwa nia ya kutenda au kuwezesha kutendeka kosa, au kuwezesha utorokaji wa mtenda kosa baada ya kutenda au kujaribu kutenda kosa, anafanya au anajaribu kufanya kitendo cha kumfanya mtu yeyote asiweze kujihami, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kumpumbaza mtu kwa nia ya kutenda kosa.

**203.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kutenda au kuwezesha kutendeka kosa, au kuwezesha utorokaji wa mtenda kosa baada ya kutenda au kujaribu kutenda kosa, anampa au anajaribu kumpa mtu dawa au kitu chochote cha kupumbaza au kumzidi nguvu, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Vitendo vinavyokusudia kusababisha madhara makubwa ya kimwili au kuzuia ukamataji.

**204.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kumsababishia mtu ulemavu wa kudumu, kumharibu umbo au kumsababishia ulemavu, au kumsababishia madhara makubwa, au anapinga au anazuia ukamataji halali au kuwekwa kizuizini mtu yeyote:

(a) bila halali anajeruhi au anasababisha madhara makubwa kwa mtu yeyote kwa njia zozote zile;

(b) bila halali anajaribu katika hali yoyote kumshambulia mtu kwa kitu chochote cha kurusha au mkuki, upanga, kisu au silaha nyengine ya hatari au ya kushambulia;

(c) bila halali kusababisha kitu cha mripuko kuripuka;

(d) anatuma au anapeleka kwa mtu kitu chochote cha mripuko au kitu chengine cha hatari au madhara;

(e) anasababisha kitu hicho kuchukuliwa au kupokelewa na mtu;

(f) anaweka majimaji ya tindikali au kitu kinachoharibu au cha mripuko pahala popote; au

(g) bila halali anammiminia au anamrushia mtu majimaji hayo au kitu hicho, au vyenginevyo anampaka majimaji hayo au kitu hicho katika mwili wa mtu yeyote,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kumzuia mtu kujiokoa katika chombo.

**205.** Mtu yeyote ambaye bila halali:

(a) anamzuia au anamkinga mtu yeyote ambaye yumo ndani ya chombo, au anakimbia kutoka kwenye chombo ambacho kimo hatarini au kinazama, katika jitihada zake za kuokoa maisha yake; au

(b) anamkinga mtu yeyote katika jitihada zake za kuokoa maisha ya mtu yeyote ambaye yupo katika hatari hiyo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kwa makusudi kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa reli.

**206.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kujeruhi au kuhatarisha usalama wa mtu yeyote anayesafiri kwa njia ya reli yoyote, awe ni mtu maalum au mtu mwengine:

(a) anaweka kitu chochote kwenye reli hiyo;

(b) anashughulika na reli, au kitu chochote kile kilichopo kwenye reli hiyo au karibu na reli, kwa namna ambayo kitadhuru au kitahatarisha matumizi huru na salama ya reli hiyo au usalama wa mtu yeyote huyo;

(c) anapiga au anarusha kitu chochote kwenye, au katika au anasababisha kitu chochote kugusana na mtu yeyote au kitu chochote ndani ya reli hiyo;

(d) anaonesha mwangaza wowote au alama yoyote, au kwa njia yoyote anajihusisha na mwangaza au alama yoyote iliyopo kwenye reli hiyo au karibu na reli hiyo; au

(e) kwa kuacha kutenda kitendo chochote ambacho ana wajibu wa kukitenda, anasababisha usalama wa mtu yeyote huyo kuwa katika hatari,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuhatarisha usalama wa chombo.

**207.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anafanya kitendo cha ghasia dhidi ya mtu aliyekuwemo ndani ya chombo cha baharini au cha angani kikiwa safarini ikiwa kitendo hicho kinapelekea kuhatarisha usalama wa chombo hicho cha baharini au cha angani;

(b) anaharibu chombo cha baharini au cha angani wakati kipo katika matengenezo au anasababisha uharibifu kwa chombo hicho cha baharini au cha angani ambao utakifanya kutokuweza kutembea au kuruka au ambao unaweza kuhatarisha usalama wake wakati wa safari;

(c) anaweka au anasababisha kuwekwa ndani ya chombo cha baharini au cha angani kikiwa katika matengenezo, kwa njia yoyote ile kifaa au kitu ambacho kinaweza kuharibu chombo hicho cha baharini au cha angani, au kinaweza kusababisha uharibifu kwa chombo hicho ambao unapelekea kuhatarisha usalama wake;

(d) anaharibu au analeta madhara kwa vifaa vya kurahisisha usafiri baharini au angani au anaingilia ufanyaji kazi wa vifaa hivyo, endapo kitendo chochote hicho kinaweza kupelekea kuhatarisha usalama wa chombo cha baharini au cha angani wakati wa safari; au

(e) anawasilisha taarifa ambazo anajua kuwa ni za uongo, kwa taarifa hizo anahatarisha usalama wa chombo cha baharini au cha angani wakati wa safari,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(2) Katika kifungu hiki:

(a) chombo cha angani kitahesabiwa kuwa kipo katika safari wakati wowote kutoka kipindi ambacho milango yote ya nje imefungwa kufuatia kuruka hadi wakati ambao mlango wowote miongoni mwa milango hiyo utakapofunguliwa kwa ajili ya kuteremka; katika hali ya kulazimika kutua, chombo cha angani kitachukuliwa kuwa kinaendelea na safari hadi pale mamlaka husika zitakapochukua jukumu la chombo cha angani, na watu na mali zilizomo katika chombo hicho;

(b) chombo cha angani kitachukuliwa kuwa kiko katika matengenezo kutoka pale yanapoanza matayarisho ya kabla ya safari ya chombo hicho kwa wafanyakazi wanaotoa huduma ardhini au wafanyakazi wanaotoa huduma kwa safari maalum hadi saa ishirini na nne baada ya kutua; kipindi cha matengenezo, katika namna yoyote, kitaendelea kwa kipindi chote ambacho chombo cha angani kiko katika safari kama ilivyoelezwa katika aya ya (a) ya kifungu hiki;

(c) kitendo cha fujo kinajumuisha kitisho chochote cha kutumia nguvu.

(3) Mtu yeyote anaweza kushtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya kujali kwamba kosa limefanyika nje ya Zanzibar.

(4) Endapo kosa limefanyika ndani ya chombo au linahusiana na chombo cha angani kilichosajiliwa Zanzibar au kinachomilikiwa na raia wa Tanzania anayeishi Tanzania au kinamilikiwa na shirika lililoanzishwa chini ya sheria yoyote ya Zanzibar, mtu yeyote hatashitakiwa na kuadhibiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki ikiwa mtu huyo ameshashtakiwa na kutiwa hatiani au, kama itakavyokuwa, ameachiwa huru, kwa kosa hilo hilo au kwa kosa linalohusisha mambo hayo hayo, katika Mahakama yoyote au mamlaka nyengine ya kimahakama nje ya Zanzibar.

(5) Mtu yeyote hatoshtakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Madhara makubwa.

**208.** Mtu yeyote ambaye bila halali anasababisha madhara makubwa kwa mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kujaribu kujeruhi kwa kitu kinachoripuka.

**209.** Mtu yeyote ambaye bila halali, na kwa nia ya kusababisha madhara kwa mtu mwengine, anaweka kitu chochote chenye kuripuka mahali popote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kuweka sumu kwa nia mbaya kwa lengo la kudhuru.

**210.** Mtu yeyote ambaye bila halali, na kwa nia ya kumdhuru au kumuudhi mwengine, anasababisha sumu au kitu chochote chenye madhara kupewa, au kuchukuliwa na mtu, na hivyo kuhatarisha maisha yake, au kumsababishia madhara makubwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kujeruhi na matendo yanayofanana na hayo.

**211.** Mtu yeyote ambaye:

(a) bila halali anamjeruhi mwengine; au

(b) bila halali, na kwa nia ya kumjeruhi au kumuudhi mtu mwengine yeyote, anasababisha sumu yoyote au kitu chengine chenye madhara kupewa au kuchukuliwa na mtu,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kushindwa kutoa mahitaji ya muhimu.

**212.** Mtu yeyote ambaye, akiwa na jukumu la kutoa mahitaji ya lazima ya maisha kwa mtu mwengine, bila sababu za msingi anashindwa kufanya hivyo, ambapo maisha ya mtu huyo mwengine yapo katika hatari au yanaweza kuwa katika hatari, au afya yake imeathiriwa au inaweza kuathiriwa moja kwa moja, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Wajibu kwa wanaofanya upasuaji wa kitabibu.

**213.** Mtu yeyote hatokuwa na jukumu la kijinai kwa kufanya kwa nia njema na kwa uangalifu na ujuzi wa kutosha, upasuaji wa kitabibu kwa mtu yeyote kwa manufaa yake, au kwa mtoto ambaye hajazaliwa kwa ajili ya kulinda uhai wa mama, ikiwa utekelezaji wa upasuaji huo ulikuwa unakubalika, kwa kuzingatia hali ya mgonjwa ilivyo kwa wakati huo, na katika mazingira yote ya ugonjwa husika.

Wajibu wa kijinai.

**214.** Mtu yeyote aliyeruhusiwa kutumia nguvu kwa mujibu wa sheria au kwa idhini ya mtu mwenyewe aliyejeruhiwa, atawajibika kijinai kwa nguvu yoyote ya ziada kutokana na hali na kiwango cha kitendo kinachopelekea nguvu ya ziada.

Idhini haitoathiri uwajibikaji wa kijinai.

**215.** Bila kujali chochote kilichomo katika kifungu cha 214, idhini ya mtu kwa ajili ya kusababisha kifo chake mwenyewe au ulemavu wake wa kudumu haitoathiri wajibu wa kijinai wa mtu ambaye amesababisha kifo hicho au ulemavu huo wa kudumu.

## SEHEMU YA ISHIRINI
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SHUGHULI ZA MAKUNDI YA KIJINAI

Makosa yanayohusiana na makundi.

**216.**-(1) Mtu yeyote ambaye anashiriki kikamilifu katika au ni mwanachama wa kundi la kihalifu na ambaye:

(a) kwa makusudi anasaidia na anawezesha shughuli yoyote ya kihalifu iliyotendwa kwa manufaa ya, na kwa maelekezo ya, na kwa kushirikiana na, kundi lolote la kihalifu;

(b) anatishia kutenda, kuleta au kufanya kitendo chochote cha ghasia au kitendo chochote cha kihalifu kwa kundi la wahalifu au kwa msaada wa kundi la kihalifu; au

(c) anatishia watu maalum wowote kwa ujumla, pamoja na kulipiza kisasi kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kwa kulipiza kitendo chochote au kitendo kinachodaiwa kuwa ni cha ghasia,

atakuwa ni mkosa.

(2) Mtu yeyote ambaye:

(a) anatenda kitendo chochote ambacho kinakusudiwa kusababisha, kuleta, kuendeleza au kuchangia kwenye mpango wa shughuli za kundi la kihalifu;

(b) anamshawishi, anamchochea, anamuamrisha, anamsaidia, anamshauri, anamuhamasisha au anamuwezesha mtu yeyote kutenda, kuleta, kutekeleza, au kushiriki katika mpango wa shughuli za kundi la kihalifu; au

(c) anamchochea, anamuamrisha, anamsaidia au anamshauri mtu mwengine kujiunga na kundi la kihalifu,

atakuwa ni mkosa.

Adhabu.

**217.**-(1) Mtu yeyote aliyetiwa hatiani kwa kosa lililotajwa katika:

(a) kifungu cha 216(1) au (2)(a) atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni sita au atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka sita;

(b) kifungu cha 216(2)(b) au (c), atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni tatu au atapewa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu.

(2) Ikiwa kosa lililoainishwa katika kifungu cha 216 limefanyika katika jengo au viwanja vya, au ndani ya mita mia tano za skuli za umma au skuli za binafsi, au taasisi yoyote nyengine ya elimu, wakati huduma za masomo zinaendelea au shughuli za kimasomo zinaendelea au watoto wanatumia huduma hiyo, hali hiyo itazingatiwa kama inaongeza uzito wa mazingira ya kosa.

(3) Ikiwa Mahakama, baada ya kumtia hatiani mshitakiwa kwa kosa lolote, isipokuwa kosa lililoainishwa katika Sehemu hii, itaona kwamba mshtakiwa alikuwa ni mwanachama wa kundi la kihalifu wakati wa kutenda kosa hilo, mtazamo huo utazingatiwa kama unaongeza uzito wa mazingira ya kosa kwa ajili ya kutoa adhabu.

Tafsiri ya mwanachama wa kundi la kihalifu.

**218.** Katika kuzingatia ama mtu ni mwanachama wa kundi la kihalifu kwa madhumuni ya Sehemu hii, Mahakama inaweza kuzingatia mambo yafuatayo, yaani mtu huyo:

(a) anakubali uanachama wa kundi la kihalifu;

(b) anatambuliwa kama mwanachama wa kundi la kihalifu na mzee, mlezi au mtu mwengine yeyote;

(c) anaishi au anakwenda mara kwa mara katika eneo maalum la kundi la kihalifu na anafuata utaratibu wao wa mavazi, matumizi ya ishara zao za mikono, lugha au tatu zao, na anajihusisha na wanachama wanaojulikana wa kundi la kihalifu;

(d) ameshakamatwa zaidi ya mara moja akifuatana na wanachama wanaotambuliwa wa kundi la kihalifu kwa makosa yanayoendana na shughuli za kawaida za kundi la kihalifu;

(e) anatambuliwa kama ni mwanachama wa kundi la kihalifu kwa ushahidi halisi kama vile picha na nyaraka nyenginezo.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
## JINAI KWA KUTOJALI NA KUPUUZA

Tendo la kuharakisha au la kizembe linalosababisha kifo.

**219.** Mtu yeyote ambaye, kwa tendo la kuharakisha au la kizembe, lisilopelekea kosa la kuua bila ya kukusudia, akasababisha kifo cha mtu mwengine, atakuwa ametenda kosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au adhabu zote mbili.

Vitendo vya kuharakisha na vya kizembe.

**220.** Mtu yeyote ambaye, kwa namna ya kuharakisha au kwa uzembe ikapelekea kuhatarisha maisha ya binaadamu au ikawezesha kusababisha madhara kwa mtu mwengine yeyote:

(a) anaendesha chombo cha moto au anaendesha chombo cha maringi mawili barabarani;

(b) anasafiri, au anashiriki katika kusafiri au anafanya kazi katika chombo chochote cha majini;

(c) anafanya kitendo chochote kwa moto au kitu kinachoweza kuwaka, au anaacha kuchukua tahadhari dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na moto au kitu kinachoweza kuwaka kilicho katika hifadhi yake;

(d) anaacha kuchukua tahadhari dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na mnyama aliye katika hifadhi yake;

(e) anaacha kuzungushia uzio au kuchukua hadhari nyengine zinazofaa dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na kisima chochote, hodhi au sehemu iliyochimbwa iliyopo katika hifadhi yake au chini ya udhibiti wake;

(f) anatoa utibabu wa dawa au upasuaji wa mtu ambaye ameahidi kumtibu;

(g) anagawa, anatoa, anauza, anampa au anampatia dawa yoyote au sumu au kitu chochote cha hatari;

(h) anafanya kitendo chochote kuhusiana na au anaacha kuchukua tahadhari inayofaa dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na mashine ambayo yeye peke yake au yeye ni sehemu ya wenye dhamana; au

(i) anafanya kitendo chochote kuhusiana na au anaacha kuchukua tahadhari dhidi ya hatari yoyote inayoweza kutokea kutokana na kitu chochote cha mripuko kilichopo kwenye hifadhi yake,

atakuwa ni mkosa.

Kuondosha matonsisi.

**221.**-(1) Mtu yeyote ambaye, sio daktari mwenye sifa zinazokubalika, anayeondoa matonsisi ya mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

(2) Endapo uondoshaji huo wa matonsisi ya mtu moja kwa moja unasababisha kifo chake, mtu anayeondosha matonsisi atakuwa ni mkosa wa kosa la kuua bila ya kukusudia.

Uondoshaji wa viungo vya binaadamu.

**222.**-(1) Mtu yeyote ambaye ama ni daktari mwenye sifa zinazokubalika au vyenginevyo:

(a) anaondosha kiungo cha binaadamu katika mwili wa mtu ikiwa mtu huyo yupo hai au amekufa, bila ya idhini ya mtu huyo au idhini ya mtu wa karibu wa mtu aliyekufa;

(b) anaondosha kiungo cha binaadamu katika mwili wa mtoto au bila ya idhini ya mzee, mlezi, au mtu wa karibu wa mtoto huyo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini.

(2) Endapo uondoshaji huo wa kiungo cha mtu moja kwa moja umesababisha kifo chake, mtu aliyeondosha kiungo hicho atakuwa ametenda kosa la kuua kwa kukusudia.

Vitendo vyengine vya uzembe vinavyosababisha madhara.

**223.** Mtu yeyote ambaye bila halali anafanya kitendo chochote, au anaacha kutenda kitendo chochote ambacho ana wajibu wa kukifanya kitendo hicho, kisichokuwa ni kitendo au kuacha kutenda kulikoainishwa katika kifungu cha 220, kwa kitendo ambacho au kuacha kutenda ambako kumesababisha madhara kwa mtu yeyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Ushughulikiaji vitu vya sumu kwa uzembe.

**224.** Yeyote anayefanya, kwa kutumia kitu chochote chenye sumu, kitendo chochote katika namna ya kuharakisha au uzembe kiasi cha kuhatarisha maisha ya binadamu, au kinachopelekea kusababisha maumivu au madhara kwa mtu mwengine yeyote, au kwa kujua au kwa uzembe ameacha kuchukua hadhari ya kitu chochote chenye sumu kilicho katika hifadhi yake kama ambavyo ingetosha kulinda dhidi ya uwezekano wa hatari ya maisha ya binaadamu, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano.

Kuhatarisha usalama wa watu wanaosafiri kwa njia ya reli.

**225.** Mtu yeyote ambaye, kwa kitendo kisicho halali au kwa kutokutenda kusiko halali ambako hakukuainishwa katika kifungu cha 206, anasababisha usalama wa mtu yeyote anayesafiri kwa njia ya reli kuwa hatarini, atakuwa ni mkosa.

Kuonesha taa za uongo, alama au boya.

**226.** Mtu yeyote ambaye anaonesha taa za uongo, alama au boya, akikusudia au akijua kuwepo uwezekano kwamba uoneshaji huo utampoteza msafiri yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kusafirisha mtu kwa njia ya maji kwa malipo katika chombo kisichokuwa salama au kilichojaza sana.

**227.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua au kwa uzembe anasafirisha, au anasababisha kusafirishwa kwa malipo, mtu yeyote kwa njia ya majini katika chombo chochote cha majini, wakati chombo hicho kiko katika hali ambayo au kimejaza sana kiasi ya kuwa hakiko salama, atakuwa ni mkosa.

Hatari au kizuwizi kwenye njia ya umma au njia ya usafiri.

**228.** Mtu yeyote ambaye, kwa kufanya kitendo chochote au kwa kuacha kuchukua tahadhari ya kutosha kwa mali yoyote iliyopo katika hifadhi yake, au ipo katika usimamizi wake, anasababisha hatari, kizuizi au madhara kwa mtu yeyote katika barabara ya umma au njia ya usafiri ya umma, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
## MASHAMBULIO

Shambulio la kawaida.

**229.** Mtu yeyote ambaye bila halali anamshambulia mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na iwapo shambulio halikutendwa katika mazingira ambayo adhabu kubwa zaidi inaelezwa katika Sheria hii, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Shambulio linalosababisha madhara ya mwili.

**230.** Mtu yeyote ambaye anafanya shambulio linalosabisha madhara mwilini, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Mashambulio kwa watu wanaolinda vyombo.

**231.** Mtu yeyote ambaye anamshambulia, anampiga au anamjeruhi hakimu yeyote, afisa au mtu mwengine aliyepewa mamlaka kihalali, katika kutimiza wajibu wake au katika kutimiza wajibu unaohusiana na kulinda chombo kilicho hatarini, au chombo au bidhaa au vitu vilivyozama, vilivyokwama au vilivyotupwa ufukweni, au vilivyo chini ya maji, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita lakini kisichozidi miaka saba.

Shambulio lenye adhabu ya kifungo cha miaka mitano.

**232.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anamshambulia mtu mwengine kwa nia ya kutenda kosa, au anakaidi au anazuia kukamatwa kihalali au asiwekwe kizuizini yeye mwenyewe au mtu mwengine yeyote kwa kosa lolote;

(b) anashambulia, anakaidi au kwa makusudi anamzuia afisa yeyote wa polisi wakati wa kutimiza wajibu wake, au mtu yeyote anayemsaidia afisa huyo;

(c) anamshambulia mtu yeyote kufuatia muungano wowote usio halali au njama kwa ajili ya kuinua kiwango cha ujira, au kuhusiana na biashara yoyote, shughuli au uzalishaji au kuhusiana na mtu husika au muajiriwa katika mambo hayo;

(d) anamshambulia, anakaidi au anamzuia mtu yeyote aliyejihusisha katika utekelezaji wa halali wa hatua, au kukamata mali kihalali, kwa nia ya kuiokoa mali hiyo yoyote iliyochukuliwa kihalali katika hatua hizo au kuzuiwa huko; au

(e) anamshambulia mtu yeyote kufuatia kitendo chochote kilichotendwa na mtu huyo katika utekelezaji wa wajibu wowote aliopewa kwa mujibu wa sheria,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU
## MAKOSA DHIDI YA UHURU WA MTU

Tafsiri ya kuteka nyara kutoka Zanzibar.

**233.** Mtu yeyote anayemsafirisha mtu mwengine nje ya mipaka ya Zanzibar bila ya idhini ya mtu huyo, au idhini ya mtu mwengine mwenye mamlaka kisheria kutoa idhini kwa niaba ya mtu huyo, itachukuliwa kuwa amemteka nyara mtu huyo kutoka Zanzibar.

Tafsiri ya kuteka nyara kutoka kwa mlezi halali.

**234.** Mtu yeyote ambaye anamchukua au anamshawishi mtoto, au mtu yeyote mwenye upungufu wa akili, kutoka kwenye uangalizi wa mlezi halali wa mtoto huyo au mtu huyo mwenye upungufu wa akili, bila ya idhini ya mlezi huyo, itachukuliwa kuwa amemteka nyara mtoto huyo au mtu huyo mwenye upungufu wa akili kutoka kwenye ulezi halali.

Adhabu ya kuteka nyara.

**235.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara mtu mwengine kutoka Zanzibar, au kutoka kwenye ulezi halali, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Tafsiri ya kutorosha.

**236.** Mtu yeyote ambaye kwa nguvu anamlazimisha, au kwa njia zozote za udanganyifu anamshawishi, mtu mwengine kwenda kutoka mahala popote, itachukuliwa kuwa amemtorosha mtu huyo.

Kuteka nyara au kutorosha kwa ajili ya kuua kwa kukusudia.

**237.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au anamtorosha mtu yeyote ili mtu huyo auwawe, au atupwe ili kuwekwa katika hatari ya kuuawa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumfungia mtu.

**238.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au kumtorosha mtu yeyote kwa nia ya kusababisha mtu huyo afungiwe kwa siri na kimakosa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kuteka nyara au kutorosha kwa nia ya kumsababishia mtu madhara makubwa au kumfanya mtumwa.

**239.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au kumtorosha mtu yeyote ili mtu huyo aweze kuwekwa, au aweze kutupwa ili awekwe katika hatari ya kupatiwa madhara makubwa, au kuwa mtumwa, au huyo au ili aweze kutupwa katika mazingira ambayo yatamuweka katika shauku mbaya ya mtu yeyote iliyo kinyume na maumbile, au kwa kujua kuwepo kwa uwezekano kwamba, mtu huyo atawekwa au atatupwa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi.

Kuficha mtu aliyetekwa au kutoroshwa kinyume na sheria.

**240.** Mtu yeyote ambaye, akijua kwamba mtu yeyote ametekwa nyara au ametoroshwa, bila halali anamficha au anamfungia mtu huyo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu kwa namna ile ile kama kwamba amemteka nyara au amemtorosha mtu huyo akiwa na nia ile ile au kwa ufahamu ule ule, au kwa madhumuni yale yale, kama kwamba au kwa kitendo ambacho alimficha au alimfungia mtu huyo kizuizini.

Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kumuibia.

**241.** Mtu yeyote ambaye anamteka nyara au anamtorosha mtoto yeyote kwa nia ya kuchukua bila ya uaminifu kitu chochote kinachohamishika kutoka katika mwili wa mtoto huyo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kumteka nyara au kumtorosha mtoto kwa nia ya kudai fedha.

**242.** Mtu yeyote ambaye bila halali:

(a) ama kwa kutumia nguvu au udanganyifu au njia nyengine zozote zisizo halali anamchukua, au anamhadaa au anamshawishi kuondoka, au anamzuia mtoto yeyote kwa nia ya kumnyima mzazi yeyote, mlezi au mtu mwengine mwenye uangalizi halali au dhamana ya mtoto huyo, kuwa naye mtoto huyo; au

(b) kwa nia ya kudai kitu chochote, fedha, au kitu chochote kutoka kwa wazazi wake, mlezi, au mtu mwengine yeyote mwenye uangalizi halali au dhamana ya mtoto huyo,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano.

Kuzuia bila halali.

**243.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anamzuia mtu yeyote kwa lengo la kumkinga mtu huyo asiendelee kwenda upande ambao mtu huyo ana haki ya kwenda, itachukuliwa kuwa amemzuia mtu huyo bila halali.

Kuweka kizuizini bila halali.

**244.** Mtu yeyote ambaye bila halali anamzuia mtu yeyote kwa namna ambayo itakayomzuia mtu huyo kwenda zaidi ya mipaka iliyoainishwa, itachukuliwa kuwa amemueka kizuizini mtu huyo bila halali.

Adhabu ya kuzuia bila halali.

**245.** Mtu yeyote ambaye amemzuia bila halali mtu yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Moja.

Adhabu ya kuweka kizuizini bila halali.

**246.** Mtu yeyote ambaye amemuweka kizuizini bila halali mtu yeyote, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja.

Kumnunua au kumuuza mtu yeyote kama mtumwa.

**247.** Mtu yeyote ambaye, anaingiza nchini, anatoa kutoka nchini, anaondosha, ananunua, anauza, anamtoa mtu yeyote kama mtumwa, au anamkubali, anampokea, au anamzuwia mtu yeyote kama mtumwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Mazoea ya kujihusisha na watumwa.

**248.** Mtu yeyote ambaye ana mazoea ya kuwaingiza nchini, kuwatoa kutoka nchini, kuwaondosha, kuwanunua, kuwauza, kuwasafirisha, au kujihusisha na watumwa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi.

Kumlazimisha mtu kufanya kazi.

**249.** Mtu yeyote ambaye bila halali anamlazimisha mtu yeyote kufanya kazi kinyume na matakwa ya mtu huyo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE
## WIZI

Vitu vinavyoweza kuibiwa.

**250.-**(1) Kitu chochote kisichokuwa na uhai ambacho ni mali ya mtu yeyote, na ambacho kinaweza kuhamishika, kinaweza kuibiwa.

(2) Kitu kisichokuwa na uhai ambacho ni mali ya mtu yeyote, na ambacho kinaweza kufanywa kuwa chenye kuhamishika, kinaweza kuibiwa mara tu kinapokuwa kinahamishika, ingawa kimefanywa kihamishike kwa nia ya kukiiba.

(3) Mnyama yoyote wa kufugwa, awe wa kufugwa kwa asili au wa porini na baadaye akafanywa wa kufugwa, ambaye ni mali ya mtu yeyote, anaweza kuibiwa.

(4) Wanyama wa porini kwa asili, wa aina ambayo si kawaida kuonekana katika mazingira huru ya kimaumbile ndani ya Zanzibar, ambao ni mali ya mtu yeyote, na ambao kikawaida wanawekwa katika hali ya kufungiwa, wanaweza kuibiwa, iwe kiuhalisia wamefungiwa au wametoroka kutoka kifungoni.

(5) Wanyama wa porini kwa asili, wa aina ambayo si kawaida kuonekana kwenye mazingira ya kuwa huru kwa asili Zanzibar, ambao ni mali ya mtu yeyote, na wana uwezo wa kuweza kuibwa wakati ambao wamo kifungoni na wakati wakiwa wanakimbizwa baada ya kotoroka kutoka kifungoni, lakini si katika wakati mwingine wowote.

(6) Mnyama wa porini kwa asili huchukuliwa kuwa yupo katika hali ya kufungiwa anapokuwa yupo katika pango la makaazi, tundu, uzio, sanduku maalum, au uzio mwengine mdogo, au vyenginevyo amewekwa kwamba hawezi kutoroka, na kwamba mmiliki wake anaweza kumchukua wakati apendao.

(7) Wanyama wa porini wakiwa katika hali ya kufurahia uhuru wao wa asili hawawezi kuibiwa lakini miili ya wanyama hao waliokufa inaweza kuibiwa.

(8) Kila kitu kinachozalishwa kutoka kwa mnyama au kinachofanya sehemu ya mwili wa mnyama ambaye anaweza kuibiwa, kinaweza kuibiwa.

Tafsiri ya wizi.

**251.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa udanganyifu na bila ya kuwa na dai la haki, anachukua kitu chochote kinachoweza kuibiwa, au kwa udanganyifu, anabadilisha kwa matumizi ya mtu yeyote tofauti na mmiliki yeyote au mmiliki maalum wa kitu hicho chochote kinachoweza kuibiwa, itachukuliwa amekiiba kitu hicho.

(2) Mtu yeyote ambaye anachukua au anabadilisha kitu chochote kinachoweza kuibiwa, atachukuliwa kufanya hivyo kwa udanganyifu iwapo anafanya hivyo kwa nia yoyote kati ya hizi zifuatazo:

(a) nia ya kumnyang'anya moja kwa moja mmiliki yeyote au maalum wa kitu hicho;

(b) nia ya kutumia kitu hicho kama rehani au dhamana;

(c) nia ya kukichukua kitu hicho kwa sharti la kurejesha ambalo mtu aliyechukua au aliyebadilisha matumizi hawezi kulitekeleza;

(d) nia ya kukitumia kitu hicho kwa namna ambayo hakiwezi kurejeshwa katika hali kilivyokuwa wakati wa kukichukua au wakati wa kukibadilisha matumizi; au

(e) ikiwa ni fedha, nia ya la kuzitumia fedha hizo kwa matakwa ya mtu ambaye anachukuwa au anazibadilisha matumizi, ijapokuwa anaweza kuwa amekusudia baadae kuzirejesha fedha hizo kwa mmiliki,

(3) Neno "mmiliki maalum" linajumuisha mtu yeyote ambaye ana dhamana au ana haki ya rehani, au haki yoyote inayotokana na kuwa nacho kitu hicho husika.

(4) Iwapo kitu kilichoibiwa kimebadilishwa, haijalishi ama kimechukuliwa kwa lengo la kubadilishwa, au ama wakati kinabadilishwa kipo katika mikono ya mtu anayekibadilisha matumizi; na pia haijalishi kwamba mtu ambaye anakibadilisha kitu husika ana hati ya uwakala kwa ajili ya uhaulishaji wa kitu hicho, au vyenginevyo ameruhusiwa kuhaulisha kitu hicho.

(5.) Iwapo kitu kilichobadilishwa kimepotezwa na mmiliki na kikaonekana na mtu ambaye amekibadilisha kitu hicho, ubadilishaji huo hautachukuliwa kuwa ni udanganyifu, iwapo wakati wa ubadilishaji huo mtu aliyechukuwa au aliyekibadilisha kitu hicho hakujua nani mmiliki, na anaamini kwa sababu za msingi kwamba mmiliki hawezi kupatikana.

(6) Mtu hatachukuliwa kwamba amechukuwa kitu isipokuwa kama amekihamisha kitu hicho au amesababisha kitu hicho kuhamishwa.

Kesi maalum.

**252.**-(1) Iwapo dalali au wakala anaweka rehani au anatoa haki ya kuzuiwa kwa mali au nyaraka za kumiliki mali zilizoaminiwa kwake kwa madhumuni ya kuuza au vyenginevyo kwa kiasi chochote cha fedha ambacho si kikubwa kuliko kiwango anachostahiki kutoka kwa mwenye mali wakati wa kuweka rehani hiyo au haki ya kuzuia, pamoja na kiwango cha hati yoyote ya malipo au ahadi ya malipo iliyokubaliwa au iliyotengenezwa na mtu huyo au kwa niaba ya mwenye mali, muamala huo wa bidhaa au nyaraka za umiliki hautachukuliwa kuwa ni wizi.

(2) Iwapo mtumishi, kinyume na amri ya mkuu wake, anachukua kutoka mikononi mwake chakula chochote ili kwamba aweze kupewa mnyama anayemilikiwa au yupo katika mikono ya mkuu wake, uchukuaji huo hautachukuliwa kuwa ni wizi.

Fedha inayozuiliwa kwa maelekezo.

**253.** Iwapo mtu yeyote anapokea, ama yeye peke yake au pamoja na mtu mwengine, fedha yoyote au dhamana yenye thamani au hati ya uwakala kwa ajili ya kuuza, kuweka rehani mali isiyohamishika, kuweka rehani mali inayohamishika au uhaulishaji mwengine wa mali yoyote, ama inayoweza kuibiwa au haiwezi kuibiwa, kwa maelekezo kati ya moja ya hali hizo kwamba fedha hizo au sehemu ya fedha hizo, au fedha nyengine yoyote iliyopokelewa katika kubadilishana na fedha hizo, au sehemu yoyote ya fedha hizo, au mapato au sehemu yoyote ya mapato ya dhamana hiyo, au mapato ya rehani ya mali isiyohamishika, mali inayohamishika, au uhaulishaji mwengine, fedha hizo zitatumika kwa madhumuni yoyote au zitalipwa kwa mtu yeyote aliyeainishwa katika maelekezo, fedha hizo na mapato hayo yatachukuliwa kuwa ni mali ya mtu ambaye kutoka kwake fedha hizo, dhamana, au hati ya uwakala ilipokelewa hadi pale maelekezo hayo yatakapofuatwa.

254. Iwapo mtu yeyote anapokea, ama yeye peke yake au kwa pamoja na mtu mwengine, mali yoyote kutoka kwa mtu mwengine kwa masharti yanayomuidhinisha au yanayomtaka mtu huyo kuuza mali hiyo au vyenginevyo kuhaulisha mali hiyo, na kumtaka mtu huyo alipe au aweke kumbukumbu za mapato ya mali, au sehemu yoyote ya mapato hayo, au kuwasilisha kitu chochote kilichopokelewa kwa kubadilishana kwa mali hiyo, kwa mtu ambaye kutoka kwake mali hiyo ilipokelewa, au mtu mwengine yeyote, kuwa mapato ya mali hiyo, na kitu chochote kinachopokelewa kwa kubadilishana kwa mali hiyo, vitu vyote hivyo vitachukuliwa kuwa ni mali ya mtu ambaye kutoka kwake mali hiyo ilipokelewa, hadi pale mali hizo zitakapohaulishwa kwa mujibu wa masharti ambayo mali hiyo ilipokelewa, isipokuwa kama ni sehemu ya masharti hayo kwamba mapato hayo, kama yapo, yatakuwa ni kitu katika hesabu ya mkopeshwaji na mkopeshaji baina ya mtu aliyepokea mali na mtu ambaye anatakiwa alipwe katika hesabu yao, na kwamba uhusiano baina ya mkopeshwaji na mkopeshaji utakuwepo baina yao kuhusiana na mali hizo.

Fedha zinazopokelewa na wakala kutokana na mauzo.

255. Iwapo mtu yeyote anapokea, ama yeye peke yake au pamoja na mtu mwengine, fedha yoyote kwa niaba ya mtu mwengine, fedha hiyo itahesabiwa kuwa ni mali ya mtu ambaye kwa niaba yake fedha hizo zimepokelewa, isipokuwa kama fedha hizo zimepokelewa kwa masharti kwamba zitafanywa kuwa ni kitu katika hesabu ya mkopeshwaji na mkopeshaji, na kwamba uhusiano baina ya mkopeshwaji na mkopeshaji utakuwepo baina yao kuhusiana na fedha hizo.

Fedha inayopokelewa kwa niaba ya mwengine.

256. Iwapo mtu anachukua au anabadilisha kitu chochote ambacho kinaweza kuibiwa, katika mazingira ambayo vyenginevyo yangeweza kuwa ni wizi, haijalishi kwamba mtu huyo yeye mwenyewe ana umiliki maalum au maslahi maalum katika kitu hicho, au yeye mwenyewe ni mmiliki wa kitu kilichochukuliwa au kilichobadilishwa bila ya kuathiri baadhi ya umiliki maalum au baadhi ya maslahi maalum ya watu wengine yaliyomo katika kitu hicho, au kwamba yeye ni mkodishwaji wa kitu hicho, au kwamba yeye mwenyewe ni mmoja kati ya wawili au zaidi ya wamiliki wa kitu hicho, au kwamba yeye ni Mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni au jumuiya ambao ni wamiliki wake.

Wizi wa watu wenye maslahi katika kitu kilichoibiwa.

257. Mtu yeyote ambaye, akiwa mwanamme na mke wake wanaishi pamoja, anawezesha mmoja kati yao kushughulikia kitu chochote ambacho, kwa kujua kwake, ni mali ya mwengine katika hali ambayo ingeweza kuwa ni wizi kama ingekuwa hawajaoana, itachukuliwa kuwa amekiiba kitu hicho, na anaweza kushtakiwa kwa wizi.

Mume na mke.

258. Mtu yeyote ambaye anaiba kitu chochote ambacho kinachoweza kuibiwa atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "wizi", na atapewa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu, isipokuwa kama kulingana na mazingira ya wizi na uhalisia wa kitu kilichoibiwa, baadhi ya adhabu nyengine inatolewa.

Adhabu ya jumla ya wizi.

Kuiba wasia, kitu kilichotumwa kwa njia ya posta au mnyama.

**259.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni:

(a) waraka wa wasia, ama anayeusia yuko hai au amekufa;

(b) kitu kilichotumwa kwa njia ya posta, au kitu chochote, fedha au dhamana yenye thamani iliyomo kwenye kitu kilichotumwa kwa njia ya posta; au

(c) farasi, farasi jike, farasi dume aliyehasiwa, punda, nyumbu, mbuni, ng'ombe dume, ng'ombe jike, ng'ombe maksai, kondoo dume, kondoo jike, kondoo jike mzee, mbuzi, nguruwe, au mnyama mwengine yeyote wa jamii hiyo,

mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Kuiba kutoka maungoni au kuiba bidhaa zinazosafiri-shwa.

**260.** Ikiwa wizi utafanyika kati ya moja ya mazingira yafuatayo, yaani:

(a) iwapo kitu kimeibiwa kutoka kwenye mwili wa mtu mwengine;

(b) iwapo kitu kimeibiwa katika nyumba ya makaazi, na thamani yake inazidi Shilingi Elfu Kumi au mkosaji wakati wa kabla au baada ya kuiba anatumia au anatishia kutumia nguvu kwa mtu aliyemo ndani ya nyumba hiyo ya makaazi;

(c) iwapo kitu kimeibiwa kutoka katika aina yoyote ya chombo cha majini au chombo cha nchi kavu au sehemu ya kuhifadhi inayotumika kwa ajili ya kusafirisha au kutunza bidhaa zinazopita kutoka sehemu moja kwenda nyengine;

(d) iwapo kitu kilichoibiwa kimeambatanishwa au ni sehemu ya njia ya reli au barabara;

(e) iwapo kitu kimeibiwa kutoka katika chombo cha baharini, ambacho kiko hatarini au kinachozama au kilichokwama;

(f) ikiwa kitu kimeibiwa kutoka katika ofisi ya umma ambapo kimehifadhiwa au kimewekwa;

(g) ikiwa mkosaji, ili kutenda kosa, anafungua chumba chochote kilichofungwa, boksi, au kontena, kwa kutumia ufunguo au kifaa chengine;

(h) ikiwa kitu kilichoibiwa ni mazao ya kilimo ama ghafi au yote au sehemu ya mazao hayo yaliyotengenezwa au yaliyosarifiwa au

mifugo au mazao ya mifugo kutoka Serikalini au kwenye shamba la Serikali,

mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kuibia Serikali.

**261.**-(1) Iwapo kitu kilichoibiwa ni mali ya Serikali au shirika lake la umma, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Shirika lake la umma, au kampuni ambayo hisa zake zote au sehemu ya hisa hizo zinamilikiwa na Serikali na thamani ya mali hiyo inazidi Shilingi Elfu Kumi lakini haizidi Shilingi Elfu Hamsini, mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka minne.

(2) Endapo thamani ya mali inayohusika inazidi Shilingi Elfu Hamsini, mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano, na ziada ya adhabu hiyo, Mahakama itamuamuru mkosaji amlipe mmiliki wa mali fidia sawa na thamani ya mali hiyo iliyoibiwa ikiwa mali hiyo haiwezi kupatikana au kurejeshwa.

Wizi wa makarani na watumishi.

**262.** Iwapo mkosaji ni karani au mtumishi, na kitu kilichoibiwa ni mali ya mwajiri wake, au kiliingia katika mikono ya mkosaji kwa sababu ya mwajiri wake, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidia miaka saba.

Wizi wa wakurugenzi au maafisa wa makampuni.

**263.** Iwapo mkosaji ni mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni, na kitu kilichoibiwa ni mali ya shirika hilo au kampuni hiyo, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Wizi wa mawakala.

**264.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni kimoja kati ya vitu vifuatavyo, yaani:

(a) mali ambayo imepokelewa na mkosaji mwenye hati ya uwakala kwa ajili ya uhaulishaji wa mali hiyo;

(b) mali ambayo mkosaji amepewa kwa njia ya kuaminiwa ama yeye peke yake au pamoja na mtu mwengine kwa ajili ya kuiweka katika ulinzi salama au kuitumia, kulipa au kuiwasilisha kwa madhumuni yeyote au kwa mtu yeyote mali hiyo au sehemu yoyote ya mali hiyo au mapato yoyote yanayotokana na mali hiyo;

(c) mali ambayo imepokelewa na mkosaji, ama yeye peke yake au pamoja na mtu mwengine kwa ajili ya au kwa sababu ya mtu mwengine yeyote;

(d) mapato yote au sehemu ya mapato ya dhamana yoyote yenye thamani ambayo yamepokelewa na mkosaji kwa maelekezo

kwamba mapato hayo yatumike kwa madhumuni yoyote au yalipwe kwa mtu yeyote aliyeainishwa katika maelekezo;

(e) mapato yote au sehemu ya mapato yanayotokana na uhaulishaji wowote wa mali yoyote ambayo imepokelewa na mkosaji kupitia hati ya uwakala kwa ajili ya uhaulishaji huo, hati hiyo ya uwakala iliyopokelewa na mkosaji kwa maelekezo kwamba mapato hayo yatumike kwa madhumuni yoyote au yalipwe kwa mtu yeyote aliyeainishwa katika maelekezo,

mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Wizi wa wapangaji au wageni.

**265.** Iwapo kitu kilichoibiwa ni chombo kilichowekwa mahala pa kudumu au kitu kinachohamishika kimekodishwa kwa mkosaji akitumie kwenye nyumba au nyumba ya kulala wageni, na thamani yake inazidi Shilingi Laki Moja, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kuiba baada ya kutiwa hatiani awali.

**266.** Iwapo mkosaji, kabla ya kufanya wizi, alikuwa ameshatiwa hatiani kwa wizi chini ya kifungu cha 258, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Wizi wa karafuu.

**267.** Ikiwa karafuu ni mali ya Serikali au mashirika yake zimeibiwa, mkosaji atapewa adhabu zifuatazo:

(a) kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka kumi;

(b) akiwa katika chuo cha mafunzo atapanda na atailea mikarafuu mia moja.

Wizi wa mazao.

**268.**-(1) Iwapo mali iliyoibiwa ni mazao ya kilimo yasiyokua mali ya Serikali au mashirika yake au mali ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano na kwa pamoja na adhabu hiyo atatakiwa kulipa mara mbili ya thamani ya soko ya mazao yaliyoibiwa na mapato yatagaiwa sawa sawa baina ya mmiliki na Serikali.

(2) Endapo mkosaji anashindwa kulipa faini iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi chengine cha miezi sita.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "mazao ya kilimo" maana yake ni mazao yanayopatikana kutoka katika aina yoyote ya kilimo na yanajumuisha, mpunga, mtama, uwele, mahindi, choroko, majimbi, ndizi, mbatata, mbogamboga, nazi, maharage, mbaazi, njegere, embe, ndimu, limau, machungwa, shelisheli, asali, nta au jamii ya

yoyote katika vitu hivyo na kanga, bata, na ndege wa jamii hiyo na inajumuisha ghafi au yote au sehemu ya yoyote kati ya mazao hayo yaliyosarifiwa.

Kutaifisha jengo ambalo mbao na miti ya wizi imetumika katika ujenzi.

**269.**-(1) Endapo mtu ametiwa hatiani kwa kosa la wizi wa mbao na miti inayomilikiwa na Serikali na pale ambapo mbao au miti hiyo imekutwa imetumika katika jengo lolote, Mahakama pamoja na kutoa adhabu yoyote, itaamuru kutaifishwa jengo hilo na Serikali.

(2) Endapo mbao zozote au miti iliyoibiwa imekutwa imetumika katika ujenzi wa jengo lolote, jukumu la kutoa maelezo ya kuridhisha kivipi amezipata mbao hizo, au miti hiyo litakuwa kwa mmiliki wa jengo hilo.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO
## MAKOSA YANAYOFANANA NA WIZI

Kuficha madaftari ya kumbukumbu.

**270.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, anaficha au anachukua kutoka katika sehemu yake ya uhifadhi daftari lolote ambalo limeidhinishwa au limetakiwa kisheria kuwekwa kwa ajili ya kuthibitisha au kuweka kumbukumbu ya umiliki wa mali yoyote, au kuweka kumbukumbu za vizazi, ubatizo, ndoa, vifo au mazishi au nakala ya sehemu yoyote ya daftari lolote hilo ambalo linahitajika kisheria kupelekwa katika ofisi yoyote ya umma, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi.

Kuficha wasia.

**271.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, anaficha waraka wowote wa wasia, ama mtoa wasia yuko hai au amefariki, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Kuficha nyaraka.

**272.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, anaficha waraka wote au sehemu ya waraka wowote ambao ni ushahidi wa umiliki wa ardhi yoyote au maslahi katika ardhi, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kuua mnyama kwa nia ya kumuiba.

**273.** Mtu yeyote ambaye anamuua mnyama yoyote anayeweza kuibiwa kwa nia ya kuiba ngozi au mzoga, au sehemu yoyote ya ngozi au mzoga, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ile ile kama kwamba amemuiba mnyama.

Kuhamisha kwa nia ya kuiba.

**274.** Mtu yeyote ambaye anafanya kitu chochote kihamishike kwa nia ya kukiiba, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ile ile kama kwamba ameiba kitu baada ya kuwa kinahamishika.

Kuhaulisha kwa udanganyifu bidhaa zilizowekwa rehani.

**275.**-(1) Mtu yeyote ambaye, akiwa mmiliki wa bidhaa zilizowekwa rehani, ataondoa au anahaulisha bidhaa hizo bila ya ridhaa ya aliyewekewa rehani, na kwa nia ya udanganyifu, atakuwa ni mkosa.

(2) Katika kifungu hiki neno "bidhaa iliyowekwa rehani" linajumuisha bidhaa zozote na vitu vinavyohamishika vya aina yoyote, na wanyama wowote, na mtoto yoyote wa wanyama wowote, na mazao yoyote yanayozalishwa kutoka ardhini, ama bado yanakuwa au yameshavunwa, ambayo yanahusika kwa wakati huo kuwa, kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote au waraka wowote ulioandikwa, deni halali au haki ya mtu kuzuia bidhaa hizo kwa njia ya dhamana kwa ajili ya deni lolote au wajibu wowote.

Udanganyifu unaohusiana na madini katika migodi.

**276.** Mtu yeyote ambaye anachukua, anaficha, au vyenginevyo anahaulisha mawe yenye thamani au metali au madini ndani au karibu na mgodi, kwa nia ya kumdanganya mtu yeyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Kuchukua umeme kwa udanganyifu.

**277.** Mtu yeyote ambaye kwa udanganyifu anatoa au anabadilisha mwelekeo kwa matumizi yake mwenyewe au kwa matumizi ya mtu mwengine yeyote, mtambo wowote, nguvu ya mwangaza au nguvu ya umeme iliyopatikana kutoka kwenye mashine yoyote, zana au kitu ambacho ni mali ya mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Kuchukua au kubadilisha kusikokuwa wizi.

**278.** Mtu yeyote ambaye bila halali na bila ya kuwa na dai la haki, lakini sio kwa kiasi hicho kuwa ni mkosa wa wizi, anachukua au anabadilisha kwa matumizi yake binafsi au kwa matumizi ya mtu mwengine yeyote, boti yoyote au mnyama wa kupanda au chombo cha moto chochote au baskeli ya aina yoyote inayosukumwa vyovyote, au chombo chochote cha majini, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA SITA
## UNYANG'ANYI NA KUPORA KWA NGUVU

Tafsiri na adhabu ya unyang'anyi.

**279.**-(1) Mtu yeyote ambaye anaiba kitu chochote, na, wakati wa kuiba, au kabla ya kuiba au mara baada ya kuiba kitu hicho, anatumia au anatishia kutumia nguvu halisi kwa mtu yeyote au mali yoyote ili akipate au akizuwie kitu hicho kilichoibiwa au kuzuia au kuondosha pingamizi katika kukiiba kitu hicho au kukizuia kitu hicho, atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "unyang'anyi".

(2) Mtu yeyote anayetenda kosa la unyang'anyi atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka ishirini na tano.

Unyang'anyi wa kutumia silaha.

**280.** Mtu yeyote ambaye anaiba kitu chochote, na, wakati wa kuiba, au kabla ya kuiba au mara baada ya kuiba kitu hicho, ametumia silaha yoyote ya hatari au yenye kudhuru au chombo, au amefuatana na mtu mmoja au zaidi ya mtu mmoja,

au iwapo, wakati wa unyang'anyi au baada ya unyang'anyi, anajeruhi, anapiga, anashambulia au anatumia nguvu nyengine zozote za mwili wake kwa mtu yeyote, atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "unyang'anyi wa kutumia silaha" na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Adhabu ya kujaribu kufanya unyang'anyi na kujaribu kufanya unyang'anyi wa kutumia silaha.

**281.**-(1) Mtu yeyote ambaye ametiwa hatiani kwa kujaribu kunyang'anya atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

(2) Mtu yeyote ambaye ametiwa hatiani kwa kujaribu kunyang'anya kwa kutumia silaha atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Shambulio kwa nia ya kuiba.

**282.** Mtu yeyote ambaye anamshambulia mtu kwa nia ya kuiba kitu chochote atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kudai mali kwa vitisho vya maandishi.

**283.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kuchukua kwa nguvu au kupata chochote kutoka kwa mtu yeyote, na kwa kujua yaliyomo katika maandishi, anasababisha mtu kupokea maandishi yoyote yakidai kitu chochote kutoka kwa mtu bila ya sababu ya msingi au ya kuaminika, na yamekusanya vitisho vya madhara yoyote au hasara ya aina yoyote itakayosababishwa kwa mtu, ama na mkosaji au na mtu mwengine yeyote, iwapo dai hilo halijatekelezwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kujaribu kuchukua kwa vitisho.

**284.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kuchukua au kupata kitu chochote kutoka kwa mtu yeyote:

(a) anamtuhumu au anatishia kumtuhumu mtu yeyote kutenda kosa, au kwa kutoa au kufanya ombi lolote au kitisho kwa mtu kama ni ushawishi wa kutenda au kuruhusu kutendeka kwa kosa;

(b) anamtishia mtu huyo atatuhumiwa na mtu mwengine yeyote kwa kosa, au kwa kitendo hicho chochote;

(c) kwa kujua yaliyomo katika maandishi, anasababisha mtu yeyote kupokea maandishi yoyote yaliyokusanya tuhuma hiyo yoyoye au vitisho kama vilivyoelezwa,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitano.

(2) Ikiwa tuhuma au kitisho cha tuhuma ni:

(a) kosa ambalo adhabu ya kifo au kifungo cha maisha inaweza kutolewa;

(b) makosa yoyote dhidi ya maadili au kujaribu kufanya kosa lolote kati ya makosa hayo;

(c) shambulio kwa nia ya kumuingilia kingono mtu yeyote kinyume na maumbile, au bila halali na kwa shambulio la aibu dhidi ya mtu mwanamme; au

(d) ombi au kitisho kilichotolewa au kufanywa kwa mtu kama ni kishawishi cha kutenda kosa au ruhusa ya kutendeka kosa lolote kati ya makossa yaliyoelezwa atakuwa ni mkosa,

mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

(3) Katika mazingira mengine yoyote mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

(4) Haijalishi kama mtu anayetuhumiwa au anayetishiwa kutuhumiwa ametenda au hajatenda kosa au kitendo ambacho anatuhumiwa nacho au anatishiwa kutuhumiwa nacho.

Kuwezesha utekelezaji wa nyaraka kwa vitisho.

**285.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, na kwa njia yoyote isiyo halali ya kutumia nguvu, au kwa kumzuia mtu wa mwengine, au kwa njia ya kitisho chochote cha kutumia nguvu au kuzuia kutumika kwa nguvu hizo katika mwili wa mtu mwengine, au kwa njia ya kutuhumu au kutishia kumtuhumu mtu kutenda kosa, au kwa kutoa au kufanya ombi lolote au kitisho kwa mtu kama ni kishawishi cha kutenda au kuruhusu kutendeka kwa kosa lolote, anamlazimisha au anamshawishi mtu yeyote:

(a) kutekeleza, kufanya, kukubali, kuridhia, kubadilisha au kuharibu dhamana yote au sehemu yoyote ya dhamana yoyote yenye thamani; au

(b) kuandika jina lolote au kutia alama au kubandika muhuri wowote kwenye karatasi au ngozi yoyote ya kuandikia, ili kwamba iweze baadae kufanywa au kugeuzwa au kutumiwa au kushughulikiwa kama ni dhamana yenye thamani,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Kudai mali kwa kutishia kwa nia ya kuiba.

**286.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kuiba kitu chochote chenye thamani, anadai kitu hicho kutoka kwa mtu kwa vitisho au nguvu, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitano.

Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu.

**287.** Mtu yeyote ambaye bila ya uaminifu anatumia vibaya au anabadilisha kwa matumizi yake binafsi mali yoyote inayohamishika, atakapotiwa hatiani atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kiwili au atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni mbili, au adhabu zote mbili.

Matumizi mabaya ya mali bila ya uaminifu ya mtu aliyekufa.

**288.** Mtu yeyote ambaye, bila ya uaminifu anatumia au anabadilisha kwa matumizi yake binafsi mali, akijua kwamba mali hiyo ilikuwa mikononi mwa mtu aliyekufa wakati wa kifo cha mtu huyo, na tangu wakati huo haijawa mikononi mwa mtu anayestahiki kisheria kuwa nayo mali hiyo, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu na kama mkosaji wakati wa kifo cha mtu huyo alikuwa ni mwajiriwa wa mtu huyo kama karani au mtumishi kifungo kinaweza kuongezeka hadi miaka saba.

Kuvunja uaminifu kijinai.

**289.** Mtu yeyote ambaye, akiwa katika hali yoyote ameaminiwa kwa mali, au kwa uangalizi wa mali, bila ya uaminifu anatumia vibaya au anabadilisha kwa matumizi yake binafsi mali hiyo, au bila uaminifu anatumia au anahaulisha mali hiyo kwa kuvunja maelekezo yoyote ya sheria inayoelekeza utaratibu ambao amana hiyo itekelezwe, au kwa mkataba wowote halali, kwa wazi wazi au kwa kumaanisha, ambao yeye ameingia unagusa utekelezaji wa amana hiyo, au kwa makusudi unamlazimisha mtu mwengine yeyote kufanya hivyo, ametenda "uvunjaji wa uaminifu kijinai" na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu, au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA SABA
## UVUNJAJI WA NYUMBA USIKU, UVUNJAJI WA NYUMBA MCHANA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

Tafsiri ya kuvunja na kuingia.

**290.**-(1) Mtu yeyote ambaye anavunja sehemu yoyote, ama nje au ndani ya jengo, au anafungua kwa kutoa komeo, anavuta, anasukuma, anainua, au kwa njia nyengine yoyote ile, mlango wowote, dirisha, shata, kilango cha dari, au kitu chengine, kilichokusudiwa kufunga au kuziba uwazi katika jengo lolote, au uwazi unaotoa njia ya kutoka sehemu moja ya jengo kwenda sehemu nyengine ya jengo, itachukuliwa kuwa amevunja jengo hilo.

(2) Mtu atachukuliwa ameingia katika jengo mara tu ambapo sehemu yoyote ya mwili wake au sehemu yoyote ya kifaa chochote anachokitumia kipo ndani ya jengo hilo.

(3) Mtu yeyote ambaye ameingia ndani ya jengo kwa njia za kitisho chochote au hadaa iliyotumika kwa lengo hilo, au kwa kushirikiana kwa hila na mtu yeyote aliyemo ndani ya jengo hilo, au anaingia kwa kupitia kwenye tundu lolote la jengo lililoachwa wazi kwa madhumuni yoyote, lakini halikusudiwi kutumika kikawaida kama njia ya kuingilia, atachukuliwa kuwa amevunja na ameingia katika jengo hilo.

Uvunjaji nyumba mchana na uvunjaji nyumba usiku.

**291.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anavunja na anaingia katika jengo lolote, hema au chombo chochote kinachotumika kama makaazi ya binaadamu kwa nia ya kutenda kosa ndani humo; au

(b) akiwa ameshaingia ndani ya jengo lolote, hema au chombo chochote kinachotumika kama makaazi ya binaadamu kwa nia ya kutenda kosa ndani humo, au akiwa ameshatenda kosa ndani ya jengo, hema, au chombo anavunja kutoka nje,

atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "uvunjaji nyumba mchana"; na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

(2) Ikiwa kosa limetendeka wakati wa usiku, litaitwa "uvunjaji nyumba usiku" na mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano.

Kuingia katika nyumba ya makaazi kwa nia ya kutenda kosa.

**292.**-(1) Mtu yeyote ambaye anaingia au yumo ndani ya jengo lolote, hema, au chombo kinachotumika kama makaazi ya binaadamu kwa nia ya kutenda kosa ndani humo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

(2) Ikiwa kosa limetendeka usiku mkosaji atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na mbili.

Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia kwa nia ya kutenda kosa.

**293.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anavunja na anaingia katika jengo la skuli, duka, ghala, stoo, ofisi, nyumba ya kuhifadhia fedha, gereji, nyumba ya matumizi maalum, klabu, kiwanda au karakana, au jengo linalomilikiwa na Serikali, idara ya Serikali, au linalomilikiwa na manispaa au mamlaka nyengine ya umma, au jengo ambalo limeshikana na nyumba ya kuishi na

linakaliwa pamoja na nyumba hiyo, lakini sio sehemu ya nyumba hiyo, au jengo linalotumika kama sehemu ya ibada na anatenda kosa ndani yake; au

(b) anavunja kwa kutoka nje ya jengo hilo akiwa ameshatenda kosa ndani yake,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na mbili.

Kuvunja jengo kwa ajili ya kuingia na kutenda kosa.

**294**. Mtu yeyote ambaye anavunja na anaingia katika jengo la skuli, duka, ghala, stoo, ofisi, nyumba ya kuhifadhia fedha, gereji, nyumba ya matumizi maalum, klabu, kiwanda au karakana, au jengo linalomilikiwa na Serikali, idara ya Serikali, au linalomilikiwa na manispaa au mamlaka nyengine ya umma, au jengo ambalo limeshikana na nyumba ya kuishi na linakaliwa pamoja na nyumba hiyo, lakini sio sehemu ya nyumba hiyo, au jengo linalotumika kama sehemu ya ibada kwa nia ya kutenda kosa ndani yake, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Watu kukutwa na silaha kwa nia ya kutenda kosa.

**295.**-(1) Mtu yeyote anayekutwa katika mojawapo ya mazingira yafuatayo:

(a) akiwa na silaha ya hatari au ya madhara au kifaa, na akiwa na silaha hiyo kwa nia ya kuvunja au kuingia katika nyumba ya makaazi na kutenda kosa ndani humo;

(b) akiwa na silaha kama ilivyoelezwa wakati wa usiku, na akiwa na silaha hiyo kwa nia ya kuvunja au kuingia katika jengo lolote lile, na akatenda kosa ndani humo;

(c) akiwa na kifaa chochote cha kuvunjia nyumba wakati wa usiku, bila ya sababu ya msingi, jukumu la kuthibitisha sababu hiyo ya msingi liko juu yake;

(d) akiwa na kifaa chochote hicho wakati wa mchana kwa nia ya kutenda kosa;

(e) akiwa ameficha sura yake au amejitia rangi nyeusi au vyenginevyo amejigeuza umbo, kwa nia ya kutenda kosa;

(f) akiwa ndani ya jengo lolote lile wakati wa usiku kwa nia ya kutenda kosa ndani humo;

(g) akiwa ndani ya jengo lolote lile wakati wa mchana kwa nia ya kutenda kosa ndani yake, na amechukua tahadhari asijulikane kama yupo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(2) Ikiwa mkosa alishatiwa hatiani awali kwa kosa linalohusiana na mali, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Kuingia kijinai.

**296.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anaingia ndani au katika mali iliyo kwenye mikono ya mtu mwengine kwa nia ya kutenda kosa au kutisha, kutukana au kumuudhi mtu anayemiliki kitu hicho;

(b) akiwa ameingia ndani au katika mali hiyo kihalali, bila halali anaendelea kubakia ndani humo kwa nia ya kutisha, kutukana au kumuudhi mtu huyo yeyote au kwa nia ya kutenda kosa; au

(c) bila halali anaingia mahala wakati sherehe, ngoma au shughuli nyengine inakaribia kuanza au inaendelea bila kulipa ada ya kiingilio ambayo inapaswa kulipwa au ambaye anatangatanga au bila halali anaendelea kubakia ndani ya yadi ishirini ya eneo hilo lolote,

atakuwa ni mkosa wa kosa linaloitwa "kuingia kijinai" na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Hamsini Elfu au adhabu zote mbili.

(2) Ikiwa mali ambayo kosa limetendeka ni nyumba, hema au chombo kinachotumika kama makaazi ya binaadamu au jengo lolote linalotumika kama sehemu ya ibada au kama sehemu ya kuhifadhia mali, mkosa atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kutaifisha.

**297.** Ikiwa mtu ametiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii Mahakama inaweza kutoa amri kwamba silaha yoyote ya hatari au ya kudhuru au kifaa kilichotumika katika kosa hilo lolote kitataifishwa na Serikali.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA NANE
## UDANGANYIFU

Tafsiri ya udanganyifu.

**298.** Uwasilishaji wowote unaofanywa kwa maneno, maandishi, au kwa kitendo, wa jambo lolote, ama lililopita au lililopo, uwasilishaji ambao kiukweli ni uongo, na mtu ambae anaefanya uwasilishaji huo anajua kuwa ni uongo au haamini kuwa ni ukweli, ni udanyanyifu.

Kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu.

**299.** Mtu yeyote ambaye kwa njia ya udanganyifu, na kwa nia ya kudanganya, anajipatia kutoka kwa mtu mwengine kitu chochote kinachoweza kuibiwa au anashawishi mtu mwengine yeyote kupeleka kwa mtu yeyote kitu chochote kinachoweza kuibiwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

Kujipatia utekelezaji wa dhamana kwa njia ya udanganyifu.

**300.** Mtu yeyote ambaye kwa njia yoyote ya udanganyifu, na kwa nia ya kudanganya, anamshawishi mtu yeyote kutekeleza, kutengeneza, kukubali, kuridhia, kubadilisha, au kuharibu dhamana yote yenye thamani au sehemu yoyote ya dhamana yoyote yenye thamani au kuandika jina au kutia alama au kubandika muhuri kwenye karatasi au ngozi yoyote ya kuandikia, ili kwamba iweze baadae kufanywa au kugeuzwa au kutumiwa au kushughulikiwa kama ni dhamana yenye thamani, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

Kuhadaa.

**301.** Mtu yeyote ambaye kwa njia yoyote ya hila ya udanganyifu au ujanja anajipatia kutoka kwa mtu mwengine yeyote kitu chochote kinachoweza kuibiwa au anamshawishi mtu mwengine yeyote kupeleka kwa mtu yeyote kitu chochote kinachoweza kuibiwa au kulipa au kupeleka kwa mtu yeyote fedha yoyote au bidhaa au kiwango chochote kikubwa cha fedha au kiwango kikubwa cha bidhaa kuliko kile ambacho angelipa au angepeleka isipokuwa kwa hila hiyo au ujanja huo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka mitano.

Kujipatia mkopo kwa njia ya udanganyifu.

**302.** Mtu yeyote ambaye:

(a) katika kupata deni lolote au dhima, anajipatia mkopo kwa njia nyengine zozote za hadaa au kwa njia nyengine yoyote ya udanganyifu;

(b) kwa nia ya kudanganya wakopeshaji wake au yeyote kati yao anafanya au anasababisha kufanywa zawadi yoyote, kupelekwa, au kuhamishwa au malipo yoyote ya mali yake; au

(c) kwa nia ya kudanganya wakopeshaji wake au yeyote kati yao, anaficha, anauza, au anaondosha sehemu yoyote ya mali yake baada au ndani ya miezi miwili kabla ya tarehe ya kutekelezwa hukumu au amri ya malipo ya fedha iliyotolewa dhidi yake,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kula njama ya kudanganya.

**303.** Mtu yeyote anayekula njama na mwengine, kwa hadaa au njia yeyote ya udanganyifu kuathiri bei ya soko ya kitu chochote kinachouzwa hadharani, au kudanganya umma au mtu yeyote, awe mtu maalum au mtu mwengine, au kupora mali yoyote kutoka kwa mtu, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Udanganyifu katika kuuza au kuweka rehani mali.

**304.** Mtu yeyote ambaye, akiwa ni muuzaji au muweka rehani wa mali yoyote au akiwa ni wakili au wakala wa muuzaji huyo yeyote au muweka rehani, kwa nia ya kumshawishi mnunuzi au muwekewa rehani kukubali hati ya umiliki iliyotolewa kwake yeye, na kwa nia ya kudanganya:

(a) anaficha kutoka kwa mnunuzi au muwekewa rehani hati muhimu kwa umiliki, au kikwazo chochote;

(b) anadanganya uhusiano wowote wa kindugu ambao hati ya umiliki inategemea au inaweza kutegemea; au

(c) anatoa maelezo yoyote ya uongo juu ya hati ya umiliki iliyotolewa au anaficha ukweli wowote ambao ni muhimu kwa hati hiyo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.

Kujifanya kupiga ramli.

**305.** Mtu yeyote ambaye, kwa ajili ya kipato au malipo, anajifanya kutumia au anatumia aina yoyote ya uchawi, wanga, kupiga ramli, au kiinimacho, au anafanya utabiri, au anajifanya kutokana na ujuzi au elimu katika sayansi yoyote ya uchawi kugundua wapi na kwa namna gani kitu chochote kinachodhaniwa kimeibiwa au kimepotea kinaweza kupatikana, atakuwa ni mkosa.

Kujipatia usajili kwa udanganyifu.

**306.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anajipatia au anajaribu kujipatia kwa ajili yake binafsi au mtu mwengine yeyote usajili, leseni au cheti chini ya sheria yoyote kwa njia yoyote ya udanganyifu, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Tamko la uongo ili kupata hati ya kusafiria.

**307.** Mtu yeyote ambaye anatoa maelezo ambayo anajua kuwa sio ya ukweli kwa ajili ya kupata hati ya kusafiria, ama kwa ajili yake mwenyewe au kwa ajili ya mtu mwengine yeyote, atakuwa ni mkosa.

Kujifanya Afisa wa umma.

**308.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anajifananisha na mtu mwengine aliyeajiriwa katika utumishi wa umma katika tukio ambalo mtumishi wa umma anahitajika kufanya jambo lolote au kuhudhuria sehemu yoyote kwa sababu ya ajira yake; au

(b) kwa kudanganya anajifanya, yeye mwenyewe kuwa ni mtu aliyeajiriwa katika utumishi wa umma, na anachukua jukumu la kufanya kitu chochote au kuhudhuria katika sehemu yoyote kwa madhumuni ya kufanya kitendo chochote kwa kupitia ajira hiyo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitano.

## SEHEMU YA ISHIRINI NA TISA
## KUPOKEA MALI ILIYOIBIWA AU ILIYOPATIKANA ISIVYO HALALI NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

Kupokea mali iliyoibiwa au iliyopatinaka isivyo halali.

**309.**-(1) Mtu yeyote ambaye anapokea au anahifadhi kitu chochote, fedha, dhamana yenye thamani au mali nyengine ile, akijua au akiwa na sababu ya kuamini kwamba mali hiyo imeibiwa, imenyang'anywa bila halali, kinyume na sheria imechukuliwa, imepatikana, imebadilishwa au imehaulishwa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

(2) Mtu yeyote ambaye anasaidia katika kuficha au kuhaulisha mali akijua au akiwa na sababu ya kuamini mali hiyo kuwa imeibiwa, imepatika au imehaulishwa kwa njia yoyote ile kwa kitendo kinachopelekea kosa, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, haijalishi ikiwa kwa kitendo hicho mali hiyo iliibiwa, ilipatikana au ilihaulishwa kilifanyika ndani au nje ya Zanzibar au pahala ambapo hapajulikani, ikiwa kitendo hicho kama kingefanyika Zanzibar kingepelekea kosa.

Watu wanaotuhumiwa kuwa na au kusafirisha mali ya wizi.

**310.** Mtu yeyote ambaye amewekwa kizuizini kutokana utekelezaji wa mamlaka ya afisa wa polisi ya kuzuia na kupekuwa vyombo na watu katika mazingira fulani yaliyotajwa katika Sheria ya Mwenendo wa Jinai na analetwa mtu huyo mbele ya

Mahakama kushtakiwa kwa kukutwa au kusafirisha katika njia yoyote ile kitu chochote ambacho kinaweza kudhaniniwa kuwa kimeibiwa au kimepatikana bila halali, na ambaye hatatoa maelezo ya kuiridhisha Mahakama jinsi alivyokipata kitu hicho, atakuwa ni mkosa.

Kupatikana na mali ya wizi.

**311.**-(1) Mtu yeyote ambaye anakutwa na afisa wa polisi akiwa na au akiwa na udhibiti wa mali ambayo inaweza, kwa kuzingatia mazingira yote, kimsingi kudhaniwa kuwa ni mali iliyoibiwa au vyenginevyo imepatikana bila halali, anaweza kushtakiwa kwa kukutwa na au kusafirisha au kuwa na udhibiti wa, kama itakavyokuwa, mali ambayo inadhaniwa kuwa imeibiwa au vyenginevyo imepatikana bila halali, na akishindwa kuiridhisha Mahakama kwamba hakuiba au vyenginevyo kaipata bila halali mali hiyo, atakuwa ni mkosa wa kosa la kukutwa na mali ya wizi, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi au atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi au vyote kwa pamoja.

(2) Pamoja na adhabu iliyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama itaamuru kutaifishwa na Serikali mali ambayo inahusiana na utendaji wa kosa hilo, au kama mali hiyo haitaweza kutaifishwa au haitaweza kupatikanwa, thamani ya mali hiyo kama itakavyotathminiwa na Mahakama.

(3) Isipokuwa kama itaamriwa vyenginevyo na Mahakama kuhusiana na mali iliyotaifishwa kwa Serikali, madai ya mtu mwengine yoyote dhidi ya Serikali kwa mali hiyo hayatopokelewa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kupatikana bila halali" maana yake ni kupatikana katika mazingira ambayo ni kinyume na sharti lolote la Sheria.

Kuficha bidhaa.

**312.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anafanya biashara ya kuuza bidhaa za aina yoyote ama kwa jumla au rejareja na ana bidhaa hizo katika ghala, anakataa kuuza bidhaa zote au kiwango chochote cha bidhaa hizo kwa mtu anayetaka kununua bidhaa hizo; au

(b) vyenginevyo hafanyi biashara ya kuuza kwa jumla au rejareja ana bidhaa hizo katika ghala au ana bidhaa za aina yoyote katika kiwango ambacho chini ya mazingira husika kiko juu zaidi ya mahitaji ya nyumbani ya mtu wa kawaida,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka saba au atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Saba au adhabu zote mbili.

(2) Pamoja na adhabu iliyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama itaamuru bidhaa zote zilizohusika katika shtaka hilo zitaifishwe.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki:

(a) "mtu yeyote ambaye anafanya biashara ya kuuza bidhaa za aina yoyote" maana yake na inajumuisha wakala yeyote au muajiriwa wa mtu huyo;

(b) mtu atachukuliwa kuwa anafanya biashara ya kuuza bidhaa za aina yoyote iwapo:

(i) wakati wowote katika kipindi kinachohusika na shtaka la kosa ambalo anatuhumiwa kulitenda ameuza au ametoa kwa ajili ya kuuza bidhaa hizo;

(ii) wakati wowote ndani ya kipindi kilichotajwa katika aya ya (i) hapo juu amejionesha yeye mwenyewe kuwa ni mtu anayefanya biashara ya kuuza bidhaa hizo; au

(iii) akiwa mtu aliyeruhusiwa kufanya biashara ya jumla au ya rejareja, wakati wa kosa ana mikononi mwake kiwango chochote cha bidhaa hizo katika mazingira ambayo, kwa maoni ya Mahakama, inaweza kuhusishwa kuwa bidhaa hizo zilikusudiwa na yeye kuuzwa katika biashara yake.

(4) Mtu atachukuliwa kuwa ana bidhaa ya aina yoyote katika ghala au mikononi mwake:

(a) ikiwa ana kiwango chochote cha bidhaa hizo katika jengo lililo chini ya udhibiti au usimamizi wake;

(b) ikiwa yeye ni mmiliki wa kiwango chochote cha bidhaa hizo au ana haki zote za kuhaulisha kwa njia ya kuuza kiwango chochote cha bidhaa hizo.

(5) Mtu atachukuliwa kuwa amekataa kuuza bidhaa zozote wakati anapotoa bidhaa kwa ajili ya kuuza katika bei au kwa masharti ambayo, kwa maoni ya Mahakama, kwa kuzingatia mazingira yote husika, sio muafaka.

Kukutwa na mali iliyoibiwa nje ya Zanzibar.

**313.** Mtu yeyote ambaye, bila sababu ya kisheria, ana mikononi mwake mali yoyote akijua au akiwa na kila sababu ya kuamini kwamba mali hiyo imeibiwa, imepatikana au imehaulishwa katika njia yoyote ile nje ya Zanzibar kwa kitendo ambacho, kama kingefanyika Zanzibar, kingekuwa ni kosa, atakuwa ni mkosa kwa kiwango kile kile na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

## SEHEMU YA THELATHINI
## UDANGANYIFU WA WADHAMINI NA WATU WALIO KATIKA NAFASI ZA DHAMANA NA HESABU ZA UONGO

Wadhamini kuharibu au kubadilisha mali za muamana kwa udanganyifu.

**314.**-(1) Mtu yeyote ambaye, akiwa mdhamini wa mali yoyote, anaharibu mali kwa nia ya udanganyifu, au kwa nia ya udanganyifu, anabadilisha mali katika matumizi yasiyoruhusiwa na amana husika, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki neno "mdhamini" inajumuisha watu wafuatao:

(a) wadhamini kutokana na amana ya waziwazi iliyoundwa kwa mkataba, wasia au hati ya maandishi ama kwa madhumuni ya umma au binafsi au msaada;

(b) wadhamini walioteuliwa na au chini ya mamlaka ya sheria yoyote kwa madhumuni hayo;

(c) mrithi au mwakilishi binafsi wa mdhamini yeyote kama ilivyoelezwa na mtu mwengine yeyote ambaye kwa mtu huyo amana yoyote hiyo itakwenda au itamfikia;

(d) wasimamizi wa mirathi inajumuisha wasimamizi wanaochukua usimamizi kimakosa na wasimamizi wa mirathi walioteuliwa na Mahakama;

(e) wasimamizi walioteuliwa chini ya mamlaka ya Sheria ya Afya ya Akili;

(f) wasimamizi rasmi, waliopewa dhamana, wafilisi au maafisa wengine wanaofanana na hao, kwa jina lolote wanaloitwa, wanafanya chini ya mamlaka ya sheria yoyote inayohusu ufilisi au makampuni ya hisa za pamoja.

Ubadhirifu na udanganyifu wa Wakurugenzi na Maafisa wa Mashirika.

**315.** Mtu yeyote ambaye:

(a) akiwa mkurugenzi au afisa wa shirika au kampuni, anapokea au anamiliki yeye mwenyewe kama mkurugenzi au afisa mali ya shirika au kampuni kinyume na malipo halali ya deni au madai, na, kwa nia ya udanganyifu, anaacha kuingiza kwa ukamilifu na ukweli katika vitabu na hesabu za shirika au kampuni, au anashindwa kusababisha au kuelekeza uingizwaji huo kufanywa katika vitabu hivyo au hesabu hizo;

(b) akiwa mkurugenzi, afisa, au mwanachama wa shirika au kampuni, anafanya moja kati ya vitendo vifuatavyo, kwa nia ya kudanganya, yaani:

(i) anaharibu, anabadili, anachana, au anaghushi kitabu chochote, nyaraka, dhamana yenye thamani au hesabu, ambayo ni mali ya shirika au kampuni, au uingizaji wowote katika kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu au anashiriki katika kitendo hicho chochote;

(ii) anafanya, au anashiriki kuacha kufanya, jambo lolote muhimu kutoka katika kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu; au

(iii) anaacha, au anashiriki kuacha, jambo lolote muhimu kutoka kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

Maelezo ya uongo ya maafisa wa kampuni.

**316.** Mtu yeyote ambaye, akiwa muanzishaji, mkurugenzi, afisa au mkaguzi wa hesabu wa shirika au kampuni, ama lililopo au linalokusudiwa kuanzishwa, anatengeneza, anasambaza au anachapisha, au anashiriki katika kutengeneza, kusambaza au kuchapisha, maelezo ya maandishi au hesabu ambayo, katika maelezo yoyote muhimu, anajua ni ya uwongo, kwa nia ya kutekeleza moja ya madhumuni yafuatayo:

(a) kumdanganya au kumhadaa mwanachama, mwanahisa, au mkopeshaji wa shirika au kampuni, ama mtu mahsusi au yeyote;

(b) kumshawishi mtu, awe mtu mahsusi au yeyote, kuwa mwanachama wa, au kuweka amana au kukopesha mali yoyote kwa, shirika au kampuni, au aingie kwenye dhamana yoyote kwa maslahi ya shirika au kampuni,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Hesabu za uongo.

**317.** Mtu yeyote ambaye, akiwa karani au mtumishi, au akiwa ameajiriwa au anafanya kazi kama karani au mtumishi, anafanya moja ya vitendo vifuatavyo kwa nia ya kudanganya, yaani:

(a) anaharibu, anabadili, anachana au anaghushi kitabu chochote, nyaraka, dhamana yenye thamani au hesabu ambayo inamilikiwa au iko katika mikono ya mwajiri wake, au uingizaji wowote katika

kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu, au anashiriki katika kitendo hicho chochote;

(b) anafanya, au anashiriki katika kufanya uingizaji wowote wa uongo katika kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu; au

(c) anaacha au anashiriki katika kuacha maelezo yoyote muhimu kutoka kwenye kitabu hicho chochote, nyaraka au hesabu,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Hesabu za uongo kwa Afisa wa umma.

**318.** Mtu yeyote ambaye, akiwa afisa mwenye dhamana ya kupokea, kuhifadhi au usimamizi wa sehemu yoyote ya mapato ya umma au mali, kwa kujua anatoa taarifa yoyote ya uongo au anafanya marejesho ya fedha yoyote au mali aliyoipokea au aliyoaminiwa kuitunza, au bakaa yoyote ya fedha au mali iliyo mikononi mwake au ipo chini ya usimamizi wake, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

## SEHEMU YA THELATHINI NA MOJA
## MAKOSA YANAYOSABABISHA UHARIBIFU WA MALI

Uchomaji wa mali kwa makusudi.

**319.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila halali anachoma moto katika:

(a) Jengo lolote au boma lolote, ama limekamilika au bado halijakamilika;

(b) chombo chochote kile kiwe kimekamilika au bado hakijakamilika; au

(c) mgodi, au maeneo ya kazi, matengenezo au zana za machimbo ya mgodi,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kujaribu kuchoma mali.

**320.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anajaribu bila halali kuchoma moto kitu chochote hicho kama kilivyotajwa katika kifungu cha 319; au

(b) kwa makusudi na bila halali anachoma moto kitu chochote ambacho kipo pahala ambapo kitu chochote kilichotajwa katika kifungu cha 319 kinaweza kushika moto kutokana na kitu hicho,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne.

Kuchoma moto mazao na mimea.

**321.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila halali anachoma moto katika:

(a) mazao ya kilimo, ama yawe katika mti, yamechumwa au yamekatwa;

(b) mazao ya nyasi za kulisha wanyama, au majani yaliyolimwa, ama yawe ya kimaumbile au ya asili kutokana na udongo au vyenginevyo, na ama yawe katika mti au yamekatwa; au

(c) miti yoyote, miche, au magugu, ama ya asili au vyenginevyo, inayolimwa; au

(d) mrundikano wowote wa mazao ya mbogamboga, au wa madini, au mafuta ya matunda,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne.

Kujaribu kuchoma moto mazao.

**322.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anajaribu bila halali kuchoma moto kitu chochote kama kilivyotajwa katika kifungu cha 321; au

(b) kwa makusudi na bila halali anachoma moto kitu chochote ambacho kipo pahala ambapo kitu chochote kilichotajwa katika kifungu cha 321 kinaweza kushika moto kutokana na kitu hicho,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kupeleka chombo mrama.

**323.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi na bila halali anapeleka mrama au anaharibu chombo chochote, ama kimekamilika au hakijakamilika;

(b) kwa makusudi na bila halali anafanya kitendo chochote ambacho kinapelekea hasara ya mara moja au uharibifu wa chombo kilichopo hatarini; au

(c) kwa nia ya kukipeleka chombo katika hatari, anaingilia mwangaza wowote, mnara, boya, alama, au ishara zinazotumika kwa madhumuni ya uongozaji wa safari, au anaonesha taa za uongo au ishara za uongo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne.

Kujaribu kupeleka mrama chombo.

**324.** Mtu yeyote ambaye anajaribu bila halali kupeleka mrama chombo au kuharibu chombo ama kimekamilika au bado hakijakamilika, au anajaribu bila halali kufanya kitendo chochote kinachopelekea hasara ya mara moja au uharibifu wa chombo kilichopo hatarini, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kujeruhi wanyama.

**325.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila halali anaua, anamtia ulemavu au anamjeruhi mnyama yoyote anayeweza kuibiwa, atakuwa ni mkosa.

Adhabu ya kuharibu mali kwa makusudi.

**326.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila halali anaharibu au anatia hasara mali yoyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu, kama hakuna adhabu nyengine iliyotolewa, ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(2) Ikiwa mali husika ni nyumba ya makaazi au chombo, na madhara yamesababishwa na mripuko wa kitu chochote kinachoripuka, na kama:

(a) mtu yeyote yumo ndani ya nyumba hiyo ya makaazi au chombo hicho; au

(b) uharibifu huo au hasara hiyo kiuhalisia imehatarisha maisha ya mtu yeyote,

mtu huyo ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(3) Ikiwa mali husika:

(a) ni ukingo au ukuta wa mto, mfereji, msingi wa kupita maji, hodhi, au maji ya nchi kavu (mto, ziwa, bwawa), au ujenzi unaohusiana na bandari, hodhi, au maji ya nchi kavu, na madhara yanasababisha hatari halisi au mafuriko au hasara kwa ardhi yoyote au jengo;

(b) ni njia ya reli au daraja, msingi, au msingi wa maji ambao unajengwa juu ya barabara kuu, njia ya reli, au mfereji au juu ya vitu hivyo reli, barabara kuu, au mfereji unapita, na mali inaharibiwa; au

(c) ikiwa ni njia ya reli au daraja hilo lolote, msingi, au msingi wa maji, umeharibiwa, na uharibifu unafanywa kwa nia ya kuifanya njia hiyo ya reli, daraja, msingi, au msingi wa maji, au njia hiyo kuu, au mfereji unaopita juu yake au chini yake au sehemu yoyote ya juu yake au chini yake, ni ya hatari na isipitike, na vitu hivyo au sehemu ya vitu hivyo kuwa ni hatari au visipitike,

mtu huyo atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

(4) Iwapo mali husika, ni waraka wa wasia, ama mtoa wasia huo yuko hai au amefariki, au daftari la kumbukumbu ambalo limeidhinishwa au limetakiwa kisheria liwekwe kwa ajili ya kuthibitisha au kuweka kumbukumbu ya hati ya umiliki mali yoyote, au kuweka kumbukumbu za vizazi, ubatizo, ndoa, vifo au mazishi, au nakala ya sehemu yoyote ya daftari hilo lolote ambalo limetakiwa kisheria kupelekwa kwa afisa yeyote wa umma, mtu huyo ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

(5) Iwapo mali husika, ni chombo kilicho hatarini au kilichozama, au kilichokwama, au kitu chochote ni sehemu ya chombo hicho, mtu huyo atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(6) Iwapo mali husika, ni sehemu yoyote ya njia ya reli au barabara, au kazi yoyote inayohusiana na njia ya reli au barabara, mtu huyo atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne.

(7) Iwapo mali husika:

(a) ni chombo, ama kimekamilika au hakijakamilika, kimeharibiwa;

(b) ni chombo, ama kimekamilika au hakijakamilika, kimepata hasara, na hasara hiyo imefanywa kwa nia ya kukiharibu au kukifanya kisitumike;

(c) ni taa, mnara, boya, alama au ishara inayotumika kwa ajili ya uongozaji wa safari, au kwa ajili ya kuwaongoza watu wanaojihusisha na usafiri;

(d) ni ukingo au ukuta wa mto, mfereji, msingi wa maji, hodhi, au maji ya nchi kavu, au ujenzi ambao unahusiana na bandari, mfereji, msingi wa maji, hodhi, au maji ya nchi kavu, ambavyo vinatumika kwa madhumuni ya kupakia au kushusha bidhaa;

(e) ni njia ya reli, au ni daraja, msingi, au msingi wa maji ambao unajengwa juu ya barabara kuu, njia ya reli au mfereji, au ambapo juu yake barabara kuu, njia ya reli au mfereji unapita, imepata hasara, na hasara hiyo kwa nia ya kuifanya njia ya reli, daraja, msingi, au msingi wa maji, au barabara kuu au njia ya reli au mfereji unaopita juu yake au chini yake au sehemu yoyote ya hivyo, ya hatari au visipitike;

(f) ni kitu chochote kilichopo katika hatua za kutengenezwa, au mashine ya kilimo au ya kiwanda au zana ya kiwanda, au mashine au kifaa kinachotumika au kinachokusudiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa hatua yoyote inayohusiana na matayarisho ya uzalishaji wa kilimo au mifugo, kimeharibiwa;

(g) ni kitu chochote hicho, mashine, zana, au kifaa, kama ilivyotajwa awali, kimepata hasara, na hasara hiyo imefanywa kwa nia ya kukiharibu kitu hicho husika na kukifanya kisitumike;

(h) ni bomba au njia ya machimbo ya madini, na uharibifu umefanyika kwa nia ya kutia hasara machimbo ya madini au kuzuia ufanyaji kazi wake;

(i) ni mashine, kifaa, chombo, jengo, ukuta, daraja au barabara, inayohusiana au inayotumika pamoja na machimbo, ama kitu husika kimekamilika au hakijakamilika;

(j) ni kamba, mnyororo au ngoweko iliyotengenezwa kwa kitu chochote, ambayo inatumika katika machimbo, au katika namna yoyote au kazi yoyote inayohusiana au inayotumika kwenye machimbo, imeharibiwa;

(k) ni kamba hiyo yoyote, mnyororo, au ngoweko, kama ilivyoelezwa awali, imepata hasara, na hasara imefanywa kwa nia ya kuharibu kitu husika au kukifanya kisitumike; au

(l) ni kisima, au kisima cha bomba, au bwawa, ukingo, ukuta, au mlango wa kuzuia maji ya bwawa la kinu cha umeme, au bwawa,

mtu huyo atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kischozidi miaka saba.

(8) Iwapo mali husika ni nyaraka ambayo imehifadhiwa au imewekwa katika ofisi ya umma, au ambayo ni ushahidi wa hati ya kumiliki ardhi yoyote au maslahi katika ardhi, mtu huyo ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

(9) Iwapo mali husika inatumika au inakusudiwa itumike kwa madhumuni ya utoaji wa huduma muhimu, mtu huyo ni mkosa na:

(a) iwapo kosa hilo linawezekana kusababisha hatari kwa maisha ya binaadamu au uharibifu, kutia hasara, kuzuwia, au kuingilia huduma yoyote muhimu au utoaji wa huduma hiyo, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka ishirini; na

(b) iwapo kosa limetendeka katika mazingira ambayo hayasababishi hatari ya maisha ya binaadamu, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na tano.

Kujaribu kuharibu mali kwa miripuko.

**327.** Mtu yeyote ambaye, bila halali na kwa nia ya kuharibu au kutia hasara mali yoyote anaweka kitu chochote cha mripuko mahala popote pale, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne.

Kusambaza maradhi ya kuambukiza kwa wanyama.

**328.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila ya halali anasababisha, au anahusika katika kusababisha, au anajaribu kusababisha, maradhi yoyote ya kuambukiza yasambazwe kwa wanyama wanaoweza kuibiwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kuondosha alama za mipaka kwa nia ya kudanganya.

**329.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi na bila ya halali, na kwa nia ya udanganyifu anaondosha au anaharibu kitu chochote au alama ambayo imewekwa kisheria au imetengenezwa kama ishara ya mpaka wa ardhi yoyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kuharibu kwa makusudi alama za upimaji na alama za mipaka.

**330.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi anaondosha, anaharibu au anaathiri alama yoyote ya upimaji au alama za mpaka zilizotengenezwa au zilizowekwa na au chini ya maelekezo ya idara yoyote ya Serikali wakati wa au kwa ajili ya upimaji wa Serikali;

(b) ikiwa na wajibu wa kutunza vizuri alama yoyote ya mpaka iliyotengenezwa au iliyowekwa kama ilivyoelezwa awali, anapuuza au anakataa kutunza alama hiyo;

(c) kwa makusudi anaondosha, anaharibu au anaathiri alama yoyote ya upimaji iliyowekwa na au chini ya mamlaka ya mpimaji yeyote aliyeruhusiwa au alama yoyote iliyowekwa na muombaji aliyekusudiwa kukodishwa, kupewa kibali au haki chini ya sheria yoyote inayohusiana na machimbo au madini; au

(d) kwa makusudi anaondosha, anaharibu au anaathiri alama yoyote iliyowekwa na muombaji aliyekusudiwa kukodishwa, kupewa kibali au haki chini ya sheria yoyote inayohusiana na machimbo au madini,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Hamsini Elfu, na inaweza kuamriwa zaidi ya mahakama kulipa gharama ya

matengenezo au kuiweka tena alama hiyo ya upimaji au alama hiyo ya mipaka na gharama za upimaji mpya unaohitajika kutokana na kitendo au uzembe wa mtu huyo.

Adhabu kwa kuharibu ujenzi wa reli au barabara.

**331.** Mtu yeyote ambaye:

(a) kwa makusudi anaharibu, anaathiri, au anazuia ujenzi wowote, njia, barabara, jengo, mlango, geti, mashine za kukusanyia ada ya barabara, uzio, mizani ya barabarani, mashine, kiguzo cha kingo za barabara, kifaa cha uchukuzi, toroli, gari ya mzigo, kifaa, kifaa kinachotumika katika ujenzi wa reli;

(b) anang'oa, anaondoa, anabadilisha, au anaharibu, au kwa njia yoyote anaingilia, nguzo zozote, pegi, bendera, vigingi, mistari, alama, au kitu chochote kilichochimbiwa ardhini au kilichowekwa juu ya ardhi, miti, mawe au majengo, au kitu chengine chochote kinachotumika katika ujenzi wa reli;

(c) anafanya maudhi yoyote au kuingia kijinai ndani ya ardhi yoyote, majengo au maeneo yanayotumika kwa ajili ya ujenzi wa reli; au

(d) kwa makusudi anamshambulia, anamzuia au anamkinga afisa mwenye dhamana wa reli yoyote au wasaidizi wake au wafanyakazi wake katika utekelezaji wa kazi yoyote iliyofanywa au itakayofanywa inayohusiana na ujenzi au ukarabati wa reli hiyo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Laki Mbili na Elfu Hamsini.

Vitisho vya kuchoma au kuharibu.

**332.** Mtu yeyote ambaye, akijua maudhui yaliyomo, anapeleka, anawasilisha, anatoa ama moja kwa moja au vyenginevyo anasababisha kupokelewa barua yoyote au maandishi yanayotishia kuchoma au kuharibu nyumba yoyote, ghala, au jengo lolote, au rundo au chungu ya nafaka, majani ya malisho, au majani, au mazao mengine ya kilimo, ama yapo ndani au katika jengo lolote au vyenginevyo, au chombo chochote, au yanayotishia kuua, kutia ulemavu, au kujeruhi mnyama yoyote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

## SEHEMU YA THELATHINI NA MBILI
## KUGHUSHI, UTENGENEZAJI WA SARAFU, UTENGENEZAJI FEDHA BANDIA NA MAKOSA YANAYOFANANA NA HAYO

Tafsiri ya kughushi.

**333.** Kughushi ni kutengeneza waraka wa uongo kwa nia ya kuhadaa au kudanganya.

Nyaraka.

**334.** Neno "waraka" katika Sehemu hii linajumuisha amri ya malipo ya fedha kupitia taasisi za kifedha au amri ya malipo ya fedha kupitia posta lakini haijumuishi alama ya biashara au alama nyengine yoyote inayotumika kuhusiana na bidhaa za biashara ingawa alama hizo zinaweza kuandikwa au kuchapishwa.

Kutengeneza waraka wa uongo.

**335.** Mtu anatengeneza waraka wa uongo, ikiwa mtu huyo:

(a) anatengeneza waraka unaokusudiwa kuwa ni kitu fulani, lakini kiuhalisia sio kitu hicho;

(b) anabadilisha waraka bila ya mamlaka katika namna ambayo iwapo ubadilishaji huo ungekuwa umeidhinishwa ungebadilisha madhumuni ya waraka huo;

(c) anaingiza katika waraka bila ya mamlaka wakati waraka huo unaandikwa jambo ambalo iwapo jambo hilo lingekuwa limeidhinishwa lingebadilisha madhumuni ya waraka huo; au

(d) anasaini waraka:

(i) kwa jina la mtu bila ya ruhusa yake, ama jina hilo ni sawa na jina la mtu anayesaini au jina hilo sio sawa na jina la mtu anayesaini;

(ii) kwa jina la mtu yeyote wa kubuniwa ambaye inadaiwa kuwa yupo, ama mtu huyo wa kubuniwa inadaiwa kuwa ana jina sawa na mtu anayesaini au mtu huyo wa kubuniwa haidaiwi kuwa ana jina sawa na mtu anayesaini;

(iii) kwa jina linalowasilishwa kama jina la mtu mwengine asiyekuwa yule mwenye kusaini waraka huo, na ambalo linakusudiwa kuwa jina hilo limewekwa kimakosa kwa ajili ya jina la mtu huyo anayesaini; au

(iv) kwa jina la mtu ambaye anafananishwa na mtu anayesaini waraka, kwa kuzingatia kwamba matokeo ya waraka huo yanategemea utambulisho baina ya mtu anayesaini waraka na mtu anayejifanya kuwa ni yeye.

Nia ya kudanganya.

**336.** Nia ya kudanganya inadhaniwa kuwepo iwapo inaonekana kwamba wakati ambao waraka wa uongo umetengenezwa kulikuwa na mtu maalum anayejulikana au asiyejulikana ambaye anaweza kudanganywa kwa waraka huo, na dhana hii haitopingwa kwa ushahidi kwamba mkosaji amechukua au amekusudia kuchukua hatua za kumzuia mtu huyo asidanganywe kiuhalisia wala kwa ukweli kwamba alikuwa na haki au alifikiri kuwa ana haki ya kitu hicho kukipata kwa waraka wa uongo.

Adhabu ya jumla ya kughushi.

**337.** Mtu yeyote ambaye anaghushi waraka wowote atakuwa ni mkosa, kwa kosa ambalo, isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo, ni kosa, au isipokuwa kwa mazingira yanayoambatana na kughushi huko au aina ya kitu kilichoghushiwa adhabu nyengine imewekwa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kughushi kunakoadhibiwa kwa kifungo cha maisha.

**338.** Mtu yeyote ambaye anaghushi wasia wowote, waraka wa hati ya umiliki wa ardhi, kumbukumbu ya Mahakama, hati ya uwakala, noti ya benki, noti ya sarafu, hundi, ahadi ya malipo, au hati nyengine ya kuamuru malipo ya fedha, hati ya bima, hundi au hati yoyote ya malipo ya fedha kwa mtu ambaye anafanya kazi za kibenki, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha na Mahakama inaweza ikatoa amri ya ziada kwamba waraka huo wowote utaifishwe na Serikali.

Kughushi hati ya Mahakama au waraka rasmi.

**339.** Mtu yeyote ambaye anaghushi hati yoyote ya Mahakama au waraka rasmi wowote atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kughushi na makosa mengine yanayohusiana na stempu.

**340.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anaghushi stempu yoyote iwe ya kugandamiza au ya kubandika inayotumiwa kwa ajili ya mapato au hesabu na idara yoyote ya Serikali;

(b) bila ya sababu ya msingi, uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu ya mtu huyo, anafanya au kwa kujua anamiliki mashine au kifaa chochote kinachoweza kutumika kwa kutengeneza stempu hiyo yoyote;

(c) kwa njia ya kudanganya anakata, anachana kwa namna yoyote, au anaondosha kutoka kwenye kitu chochote stempu iliyotumiwa kwa ajili ya mapato au hesabu na Serikali, kwa nia ya kwamba matumizi mengine yatafanywa kwa kutumia stempu hiyo au sehemu ya stempu hiyo;

(d) kwa njia ya kudanganya anabadilisha stempu hiyo yoyote kama ilivyoelezwa, kwa nia ya kwamba matumizi mengine yatafanywa kwa kutumia stempu hiyo;

(e) kwa njia ya kudanganya anabandika au anaweka katika kitu chochote au katika stempu hiyo yoyote kama ilivyoelezwa stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo ama kwa udanganyifu au vyenginevyo imekatwa, imechanwa, au kwa njia yoyote imeondolewa kutoka katika kitu chengine chochote au kutoka katika stempu nyengine yoyote;

(f) kwa njia ya udanganyifu anafuta au vyenginevyo anaondosha kiukweli au kimuonekano kutoka kwenye kitu chochote kilichowekwa stempu jina lolote, kiwango, tarehe au, jambo jengine au kitu chochote kile kilichoandikwa juu yake kwa nia ya kwamba matumizi mengine yatafanywa ya stempu juu ya kitu hicho; au

(g) kwa kujua na bila sababu ya msingi, uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu ya mtu huyo, ana katika umiliki wake stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo kwa njia ya udanganyifu imekatwa, imechanwa, au vyenginevyo imeondolewa katika kitu chochote, au stempu yoyote ambayo kwa njia ya udanganyifu ilibadilishwa, au kitu chochote kilichowekwa stempu ambacho kutoka katika kitu hicho, jina lolote, kiwango, tarehe au jambo jengine au kitu kwa njia ya udanganyifu kimefutwa au vyenginevyo kwa uhalisia au kwa muonekano kimeondoshwa,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kutengeneza au kumiliki karatasi au zana za kughushi.

**341.** Mtu yeyote ambaye bila ya mamlaka ya kisheria au sababu ya msingi uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu ya mtu huyo:

(a) anatengeneza, anatumia, au kwa kujua ana katika hifadhi yake au umiliki wake karatasi yoyote inayokusudiwa kufanana na kupitishwa kama karatasi maalum kama ilivyoelezwa huko na inatumika kwa ajili ya kutengeneza sarafu au noti ya kibenki;

(b) anatengeneza, anatumia, au kwa kujua ana katika hifadhi yake au umiliki wake, muundo wowote, umbo, au kifaa cha kutengenezea karatasi hiyo, au kwa kutengeneza kwenye au juu ya karatasi hiyo maneno yoyote, namba, herufi, alama, mistari au vifaa maalum vinavyotumika kwenye au juu ya karatasi hiyo yoyote;

(c) anachora au kwa njia nyengine yoyote anafanya kwenye sahani yoyote, ubao, jiwe, au kitu chengine, maneno yoyote, namba, herufi, alama, mistari au vifaa, uchapishaji wa vitu hivyo unafanana wote au sehemu yake, maneno, namba, herufi, alama, mistari au vifaa maalum vinavyotumika kwenye au juu ya noti za kibenki, au kwenye au juu ya waraka wowote unaotoa haki au unathibitisha umiliki wa mtu yeyote katika hisa yoyote au maslahi katika hisa za umma zozote, malipo ya mwaka, fedha, au deni la Serikali, au katika hisa zozote, malipo ya mwaka, fedha au deni la shirika lolote, kampuni au jumuiya, iliyopo ndani au nje ya Zanzibar;

(d) anatumia au kwa kujua ana katika hifadhi au milki yake, sahani yoyote, ubao, jiwe, au kitu chengine, ambacho maneno hayo yoyote, namba, herufi, alama, mistari au vifaa, vimechorwa au kwa njia nyengine yoyote vimefanywa kama ilivyoelezwa kabla; au

(e) anatumia au kwa kujua ana katika hifadhi yake au umiliki wake karatasi yoyote ambayo maneno hayo yoyote namba, herufi, alama, mistari au vifaa vimechapishwa au katika njia nyengine yoyote vimefanywa kama ilivyoelezwa kabla,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kuwasilisha nyaraka za uongo.

**342.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua na kwa njia ya udanganyifu anawasilisha waraka wa uongo atakuwa ni mkosa wa kosa lile lile na atapewa adhabu ile ile kama kwamba ameghushi kitu kinachohusika.

Kuwasilisha nyaraka zilizofutwa au zilizomaliza muda.

**343.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua anawasilisha waraka kama vile upo na una nguvu za kisheria, waraka ambao kwa mamlaka ya kisheria imeshaamriwa kubatilishwa, kufutwa au kusitishwa, au matumizi ya waraka huo yamesitishwa kutokana na kumalizika muda, au kwa kifo, au kwa kutokezea tukio jengine lolote, atakuwa ni mkosa wa kosa lile lile na atapewa adhabu ile ile, kama kwamba alighushi kitu kinachohusika.

Kuwezesha utekelezaji wa waraka kwa njia ya udanganyifu.

**344.** Mtu yeyote ambaye, kwa njia yoyote ya uwasilishaji wa maelezo ya uongo au udanganyifu kuhusu asili, maudhui au matumizi ya waraka, anamfanya mtu mwengine atiye saini au atekeleze waraka huo, atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ile ile, kama kwamba alighushi waraka huo.

Kufuta mistari katika hundi.

**345.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya:

(a) anafuta, anaongeza au anabadilisha mistari kwenye hundi; au

(b) kwa kujua anawasilisha hundi iliyochorwa mistari, mistari ambayo imefutwa imeongezwa au imebadilishwa,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kutengeneza nyaraka bila mamlaka.

**346.** Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya au kuhadaa:

(a) bila mamlaka ya kisheria au sababu ya msingi, anatengeneza, anasaini au anatekeleza kwa niaba ya au kwa jina la au kwa madhumuni ya mtu mwengine, ama kwa kuleta au vyenginevyo, waraka wowote au maandishi; au

(b) kwa kujua anawasilisha waraka wowote au maandishi yaliyofanywa, yaliyosainiwa, au yaliyotekelezwa na mtu mwengine kama ilivyoelezwa katika aya ya (a),

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kudai mali kwa nyaraka za wasia zilizoghushiwa.

**347.** Mtu yeyote ambaye anawezesha kupewa au kulipwa yeye mwenyewe au mtu mwengine mali yoyote au fedha kwa njia ya wasia au barua ya usimamizi wa mirathi iliyotolewa kutokana hati ya wasia iliyoghushiwa, akijua kuwa hati hiyo ya wasia imeghushiwa, au kutokana na hati ya usimamizi wa mirathi iliyopatikana kwa ushahidi wa uongo, akijua hati hiyo imepatikana kwa ushahidi wa uongo, atakuwa ni mkosa wa kosa lile lile na atapewa adhabu ile ile, kama kwamba alighushi waraka huo au kitu kwa njia ya waraka huo au kitu hicho aliwezesha kupewa au kulipwa.

Kununua noti zilizoghushiwa.

**348.** Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka halali au sababu ya msingi, uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu ya mtu huyo, ananunua au anapokea kutoka kwa mtu yeyote, au ana katika umiliki wake, noti ya benki iliyoghushiwa au sarafu, ama imejazwa au haijajazwa, akijua kuwa imeghushiwa, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kughushi hati za fedha zinazolipwa chini ya mamlaka ya umma.

**349.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mtumishi wa umma, kwa kujua na kwa nia ya kudanganya anatengeneza au anampa mtu yeyote kwa ajili ya malipo ya fedha zozote zinazolipwa na mamlaka ya umma, kwa kiasi kikubwa au kidogo zaidi kuliko kile ambacho mtu huyo ambaye kwa ajili yake hati husika imetengenezwa anastahiki, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kughushi daftari la kumbukumbu.

**350.** Mtu yeyote ambaye, ana usimamizi halisi wa daftari au kumbukumbu yoyote iliyowekwa na mamlaka halali, kwa kujua, anaruhusu uingizaji wowote ambao katika jambo lolote muhimu anajua kuwa ni la uongo, kuingizwa katika daftari au kumbukumbu, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Kupeleka cheti cha uongo cha ndoa kwa mrajis.

**351.** Mtu yeyote ambaye anasaini au anapeleka kwa mtu aliyeidhinishwa kisheria kusajili ndoa, cheti cha ndoa, au nyaraka zozote zinazodhaniwa kuwa ni cheti cha ndoa, ambacho katika taarifa yoyote muhimu anajua kuwa ni uongo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka saba.

Maelezo ya uongo kwa ajili ya daftari la uandikishaji wa vizazi, vifo au ndoa.

**352.** Mtu yeyote ambaye kwa kujua na kwa nia ya kuwezesha kuingizwa katika daftari la vizazi, vifo, au ndoa anatoa maelezo yoyote ya uongo yanayogusa jambo lolote linalotakiwa kisheria kusajiliwa katika daftari hilo lolote, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kutaifisha.

**353.** Iwapo mtu yeyote ametiwa hatiani kwa kosa chini ya Sehemu hii, Mahakama itaamrisha kutaifishwa na Serikali, noti ya kibenki iliyoghushiwa, au sarafu au stempu yoyote, umbo, chombo, kifaa, mashine, mashine ya kugandamiza au chuma kilichotumika katika kutenda kosa hilo lolote.

## SEHEMU YA THELATHINI NA TATU
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SARAFU NA NOTI

Tafsiri.

**354.** Katika Sehemu hii:

"sarafu" inajumuisha sarafu yoyote iliyotengenezwa kwa madhumuni ya matumizi ndani ya Tanzania, au sarafu yoyote halali inayotumika Tanzania au katika sehemu yoyote ya nchi za Jumuiya ya Madola; na sarafu yoyote ya nchi ya kigeni au Taifa, na sarafu ambayo ilikuwa katika wakati wowote ni fedha halali ndani ya Tanzania au katika nchi nyengine yoyote na ambayo inabadilishika kuwa ni sarafu halali inayotumika ndani ya Tanzania.

"sarafu bandia" maana yake ni sarafu isiyokuwa halisi lakini inafanana au kimuonekano imekusudiwa ifanane au itumike kama ni sarafu sahihi; na inajumuisha sarafu halisi iliyotayarishwa au iliyobadilishwa ili itumike kama sarafu yenye thamani kubwa zaidi.

Kughushi sarafu.

**355.** Mtu yeyote ambaye anatengeneza au anajaribu kutengeneza sarafu bandia yoyote atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Matayarisho ya kutengeneza sarafu bandia.

**356.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anachovya dhahabu au anachovya fedha kipande chochote cha chuma cha kiwango kinachofaa au umbo liwe ni sarafu, kwa nia ya kwamba iwe ni sarafu bandia;

(b) anatengeneza kipande chochote cha chuma cha kiwango kinachofaa au umbo kuwezesha kutengenezwa kutokana na chuma hicho sarafu yoyote bandia, kwa nia ya kwamba sarafu hiyo bandia itatengenezwa kutokana na chuma hicho; au

(c) bila mamlaka halali au sababu ya msingi, uthibitisho ambao wa sababu hiyo utakuwa juu yake:

(i) ananunua, anauza, anapokea, analipa, au anahaulisha sarafu yoyote bandia kwa thamani ndogo kuliko thamani halisi au kimuonekano inakusudiwa kuwa thamani halisi, au anakubali kufanya kitu hicho chochote;

(ii) analeta au anapokea katika Zanzibar sarafu yoyote ya bandia, akijua kuwa ni ya bandia;

(iii) anafanya au anatengeneza, au anaanza au anatayarisha kufanya au kutengeneza, au ana katika milki yake, au anahaulisha muhuri wowote au umbo ambalo linaweza kubadilishwa kufanya lifanane na pande zote mbili au upande mmoja wa sarafu, au sehemu yoyote ya upande wowote wa sarafu hiyo; akijua kwamba kitu hicho ni stempu au umbo au kitu hicho kilibadilishwa kwa ajili hiyo;

(iv) anafanya au anatengeneza, au anaanza au anatayarisha kufanya au kutengeneza, au ana katika milki yake, au anahaulisha chombo chochote, kifaa au mashine ambayo inaweza kubadilishwa na inakusudiwa kutumika kwa ajili ya kutia alama sarafu katika mviringo wa sarafu pamoja na alama za maumbo kimuonekano zifanane na zile za kwenye mviringo wa sarafu yoyote, akijua kwamba kitu hicho kimebadilishwa na kimekusudiwa hivyo;

(v) anafanya au anatengeneza, au anaanza au anatayarisha kufanya au kutengeneza, au ana katika milki yake, au anahaulisha mashine ya kugandamiza kwa ajili ya kutengeneza sarafu, au chombo chochote, kifaa au mashine ambayo inaweza kutumika kwa kukata maumbo ya duara ya dhahabu, fedha au

chuma chengine, akijua mashine hiyo ya kugandamiza, chombo, kifaa, au mashine kuwa imetumika au inakusudiwa kutumika kwa kutengeneza sarafu bandia,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo cha maisha.

Kupunguza sarafu.

**357.** Mtu yeyote ambaye anajihusisha na sarafu yoyote kwa namna ambayo inapunguza uzito wake kwa nia ya kwamba wakati anafanya hivyo inaweza kutumika kama sarafu, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kumiliki vipande vya sarafu zilizokatwa.

**358.** Mtu yeyote ambaye bila halali ana katika milki yake au anahaulisha vipande vyovyote, au vipande vya dhahabu au vya fedha, au vinoo vyovyote vya dhahabu au vya fedha, vumbi, majimaji, au hali nyengine yoyote, vilivyopatikana kwa kujihusisha na sarafu ya dhahabu au fedha kwa namna ambayo inapunguza uzito wake, akijua vitu hivyo vimepatikana kwa njia hiyo, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kutoa sarafu bandia.

**359.** Mtu yeyote ambaye anatoa sarafu yoyote bandia, akijua kuwa ni sarafu bandia, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Kurudia kutoa sarafu bandia.

**360.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anatoa sarafu yoyote bandia akijua kuwa ni sarafu bandia na wakati wa utoaji huo ana katika milki yake sarafu nyengine yoyote bandia;

(b) anatoa sarafu yoyote bandia akijua kuwa ni sarafu bandia, na ama katika siku hiyo hiyo au katika siku yoyote ndani ya siku kumi zinazofuata, anatoa sarafu nyengine yoyote bandia, akijua kuwa ni sarafu bandia; au

(c) ana katika milki yake sarafu tatu au zaidi za bandia, akijua kuwa sarafu hizo ni za bandia kwa nia ya kutoa yoyote kati ya hizo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

Kuwasilisha chuma au sarafu isiyotumika kama sarafu kwa wakati huo.

**361.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kudanganya, anawasilisha kama na kwa ajili ya sarafu medali yoyote au kipande cha chuma atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Mtu yeyote ambaye, kwa njia ya kudanganya, anawasilisha kama na kwa ajili ya sarafu halali inayotumika wakati huo katika Zanzibar kwa mujibu wa sheria au vyenginevyo, sarafu yoyote ambayo si halali wakati huo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kuingiza ndani ya nchi au kusafirisha nje ya nchi sarafu bandia.

**362.** Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka halali au sababu ya msingi, uthibitisho ambao wa sababu hiyo utakuwa juu yake, anaingiza ndani ya nchi au anasafirisha nje ya nchi au anaingiza kwenye chombo cha majini au cha nchi kavu cha aina yoyote, kwa madhumuni ya kuingizwa au kusafirishwa kutoka Zanzibar, sarafu yoyote bandia kwa hali yoyote, akijua kuwa ni sarafu bandia, atakuwa ni mkosa.

Kutaifisha.

**363.** Iwapo mtu yeyote ametiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sehemu hii, Mahakama itaamuru kutaifishwa na Serikali noti yoyote ya kibenki iliyoghushiwa au noti ya sarafu au sarafu yoyote ya bandia, au stempu yoyote, umbo, chombo, kifaa, mashine, mashine ya kugandamiza au sarafu yoyote, kinoo cha dhahabu au chuma kinachotumika katika kutenda kosa hilo.

Kubadilisha noti ya kibenki na kuyayusha sarafu.

**364.** Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka halali:

(a) kwa makusudi anabadilisha, anachana, anakata au vyenginevyo ananyofoa noti yoyote ya kibenki au noti ya sarafu ambayo ni fedha halali; au

(b) anayayusha, anavunja, anabadilisha kwa kupiga muhuri katika sarafu hiyo jina lolote, neno au alama, au anatumia vyenginevyo tofauti na inavyohitajika wakati huo, sarafu yoyote kwa wakati huo,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Mbili kwa kila noti au sarafu.

Utoaji wa noti usio halali.

**365.** Mtu yeyote ambaye anatoa au ni sehemu ya utoaji:

(a) noti yoyote inayokusudiwa kuwa ni noti ya sarafu ya Tanzania au ya nchi nyengine yoyote; au

(b) noti yoyote ya kibenki inayokusudiwa kuwa ni sarafu ndani ya Tanzania; vyenginevyo isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

## SEHEMU YA THELATHINI NA NNE
## STEMPU BANDIA

Kumiliki muhuri wa moto kwa madhumuni ya kutengeneza stempu.

**366.** Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka halali au sababu za msingi, uthibitisho ambao wa sababu hiyo utakuwa juu yake:

(a) anatengeneza au anabadilisha, au anaanza au anatayarisha kutengeneza au kubadilisha, au anatumia, au kwa kujua ipo katika milki yake, au anahaulisha muhuri wowote wa moto, sahani, au kifaa kinachoweza kutengeneza mfanano wa kitu kwamba kimetengenezwa na muhuri wowote wa moto, sahani au kifaa kilichotumika kwa madhumuni ya kutengeneza stempu yoyote, ama ya kugandamiza au ya kugandisha, ambayo inatumika kwa madhumuni ya mapato ya idara ya Posta na Simu Zanzibar, au katika sehemu yoyote ya Tanzania Bara au katika nchi yoyote ya kigeni, au inayoweza kuzalishwa katika karatasi yoyote, neno lolote, nambari, herufi, alama au mistari inayofanana na maneno yoyote, nambari, herufi, alama au mistari inayotumika katika karatasi yoyote maalum iliyotolewa na mamlaka husika kwa madhumuni hayo yoyote;

(b) kwa kujua ana katika milki yake au anahaulisha karatasi yoyote au kitu chengine ambacho kina mgandamizo wa muhuri wa moto huo wowote, sahani au kifaa, au karatasi yoyote ambayo ina maneno hayo yoyote, nambari, herufi, alama au mistari kama ilivyoelezwa;

(c) kwa udanganyifu, na kwa nia kwamba matumizi yanaweza kufanywa ya stempu hiyo yoyote kama ilivyoelezwa, au sehemu yake yoyote, anaondosha stempu hiyo kutoka katika kitu chochote kwa njia yoyote ile;

(d) kwa udanganyifu, na kwa nia kwamba matumizi yanaweza kufanywa ya sehemu yoyote ya stempu hiyo, ananyofoa stempu hiyo;

(e) kwa udanganyifu anabandika au anaweka juu ya kitu chochote au juu ya stempu yoyote hiyo, stempu yoyote au sehemu ya stempu ambayo imeondoshwa kwa njia yoyote kutoka kwenye kitu chengine chochote, au imekatwa au kutoka kwenye stempu nyengine yoyote;

(f) kwa udanganyifu, na kwa nia kwamba matumizi yanaweza kufanywa ya stempu hiyo yoyote ambayo tayari imeshagandamizwa juu yake au imeshabandikwa katika kitu chochote, anafuta au vyenginevyo

anaondosha ama kwa uhalisia au kwa muonekano, kutoka kwenye kitu hicho kitu chochote kile kilichoandikwa juu yake;

(g) kwa kujua ana katika milki yake au anahaulisha kitu chochote kilichopatikana au kilichotayarishwa kwa kitendo chochote hicho kisicho halali kama ilivyoelezwa; au

(h) kwa udanganyifu au kwa nia ya kusababisha hasara kwa Serikali, anatumia kwa madhumuni yoyote stempu yoyote iliyotolewa na Serikali kwa madhumuni ya mapato ambayo anajua kuwa ilishawahi kutumiwa kabla,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba; na muhuri wowote wa moto, sahani, kifaa, karatasi au kitu chengine kama ilivyoelezwa ambacho kinakutikana katika milki yake kitataifishwa na Serikali.

Karatasi na muhuri wa moto kwa ajili ya kutengeneza stempu za posta.

**367.**-(1) Mtu yeyote ambaye, bila mamlaka halali au sababu za msingi, uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu yake:

(a) anatengeneza, au anaanza au anatayarisha kutengeneza, au anatumia kwa madhumuni yoyote ya kiposta, au ana katika milki yake au anahaulisha kitu chochote chenye kufanana au kinachowakilisha stempu yoyote iliyotumika katika karatasi au kitu chengine chochote, kwa kuonesha kiasi chochote cha gharama za posta kwa Zanzibar;

(b) anatengeneza au anabadilisha, au anaanza au anatayarisha kutengeneza au kubadilisha, au anatumia au ana katika milki yake au anahaulisha muhuri wowote wa moto, sahani, kifaa, au kitu chengine chochote kwa ajili ya kutengeneza mfanano huo wowote au kiwakilishi hicho chochote,

atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tatu.

(2) Stempu zozote na vitu vyengine vyovyote kama ilivyoelezwa, ambavyo vitapatikana katika milki yake, vitataifishwa na Serikali.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki stempu inayokusudiwa kuonesha kiasi cha gharama za posta za nchi yoyote itachukuliwa kuwa ni stempu iliyotumika kwa madhumuni ya kiposta katika nchi hiyo mpaka itakapooneshwa vyenginevyo.

## SEHEMU YA THELATHINI NA TANO
## MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KOMPYUTA

Matumizi.

**368.** Masharti ya Sehemu hii na masharti mengine yanayohusiana na Sehemu hii yatatumika kwa kitendo kinachofanywa au kinachoachwa kufanywa:

(a) katika mamlaka ya Mahakama ya Zanzibar;

(b) katika meli au ndege iliyosajiliwa Zanzibar;

(c) kwa raia wa Tanzania ambaye ni mkaazi wa Zanzibar nje ya mamlaka ya nchi yoyote; au

(d) kwa Mtanzania ambaye ni mkaazi wa Zanzibar nje ya mamlaka ya Mahakama za Zanzibar, iwapo kitendo chake kingekuwa ni kosa chini ya sheria ya nchi ambapo kosa hilo limetendeka.

Makosa dhidi ya mali ya ubunifu.

**369.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anabadilisha taarifa, programu, au nyaraka zinazosaidia zinazowekwa au zilizopo ndani au nje ya kompyuta, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta, anatenda kosa.

(2) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anaharibu taarifa, programu, au nyaraka zinazosaidia zinazowekwa au zilizopo ndani au nje ya kompyuta, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta, anatenda kosa.

(3) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anaweka bayana au anachukua taarifa, programu, au nyaraka zinazosaidia ambazo ni siri za kibiashara au ni siri kwa mujibu wa sheria zinazowekwa au zilizopo ndani au nje ya kompyuta, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta, anatenda kosa.

(4) Katika kifungu hiki isipokuwa kama inaelezwa vyenginevyo:

(a) ikiwa kosa ni dhidi ya mali ya ubunifu, basi mtu huyo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(b) ikiwa kosa linatendwa kwa madhumuni ya kutengeneza au kutekeleza mpango wowote au ujanja kwa kudanganya au kupata mali yoyote, basi mtu huyo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Makosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta.

**370.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anabadilisha vifaa au vitu vinavyotumika au vinavyokusudiwa kutumika katika kompyuta, mfumo wa komyuta, au mtandao wa kompyuta, atakuwa ni mkosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(2) Ikiwa kosa linatendwa kwa madhumuni ya kutengeneza au kutekeleza mpango wowote au ujanja kwa kudanganya au kupata mali yoyote, basi mtu huyo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi.

Kuharibu vifaa vya kompyuta.

**371.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anaharibu, anachukua, anaathiri, au anatia hasara vifaa au vitu vinavyotumika au vinavyokusudiwa kutumika katika kompyuta, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta; au mtu yeyote kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini anaharibu, anaathiri, au anatia hasara kompyuta yoyote, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta, anatenda kosa dhidi ya vifaa au vitu vya kompyuta, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu lakini kisichozidi miaka kumi.

(2) Ikiwa hasara kwa vifaa au vitu hivyo vya kompyuta au kwa kompyuta hiyo, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kumpyuta ni Shilingi Milioni Moja au zaidi, au ikiwa kuna kukatika au kuharibika kwa shughuli za Serikali au mawasiliano ya umma, usafirishaji, au usambazaji wa maji, gesi, au huduma nyengine ya jamii, basi mtu huyo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano lakini kisichozidi miaka kumi na tano.

Kuingilia taarifa.

**372.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa makusudi au bila ya hadhari, bila ya sababu ya msingi au sababu inayokubalika, anafanya moja ya vitendo vifuatavyo:

(a) anaharibu au anabadilisha taarifa;

(b) anazifanya taarifa kuwa hazina maana, haziwezi kutumika au kuwa sio za uhalisia;

(c) anazuwia, anasitisha au anaingilia matumizi halali ya taarifa;

(d) anamzuia, anamsitisha, au anamuingilia mtu anayetumia kihalali taarifa; au

(e) anakataa upatikanaji wa taarifa kwa mtu anayestahiki kupata taarifa hizo,

atakuwa anatenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano, au adhabu zote mbili.

(2) Kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitatumika ama kitendo cha mtu huyo kina athari ya muda mfupi au ya kudumu.

Kuingilia mfumo wa kompyuta.

**373.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi au bila ya hadhari, bila sababu ya msingi au sababu inayokubalika:

(a) anazuia au anaingilia ufanyaji kazi wa mfumo wa kompyuta; au

(b) anamzuia au anamuingilia mtu ambaye anatumia kihalali au anaendesha mfumo wa kompyuta,

atakuwa anatenda kosa linaloadhibiwa kwa kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi Milioni Tano au adhabu zote mbili.

(2) Katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, neno "kuzuia" katika uhusiano wa mfumo wa kompyuta, linajumuisha lakini halitaishia kwenye:

(a) kukata umeme kwenye mfumo wa kompyuta;

(b) kusababisha uingiliaji wa umemesumaku katika mfumo wa kompyuta;

(c) kuchafua mfumo wa kompyuta kwa njia yoyote; na

(d) kuingiza, kufuta au kubadilisha taarifa za kompyuta.

Kuingilia kati taarifa kinyume na sheria.

**374.** Mtu yeyote ambaye, kwa makusudi bila sababu ya msingi au sababu inayokubalika, anaingilia kati kwa njia za kiufundi:

(a) mawasiliano yoyote yasiyo ya umma, au katika mfumo wa kompyuta; au

(b) utoaji wa kiumemesumaku kutoka katika mfumo wa kompyuta ambao unabeba taarifa za kompyuta,

anatenda kosa linaloadhibiwa, kwa kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano, au faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano, au adhabu zote mbili.

Vifaa visivyo halali.

**375.** Mtu yeyote anatenda kosa ikiwa mtu huyo:

(a) kwa makusudi na bila ya hadhari, bila sababu ya msingi au sababu inayokubalika anazalisha, anauza, analeta kwa matumizi, anaingiza nchini, anapeleka nje ya nchi, anasambaza au vyenginevyo anafanya vipatikane:

(i) kifaa, kinachojumuisha programu ya kompyuta, ambayo imetengenezwa au inaweza kutumika kwa ajili ya kutenda kosa;

(ii) neno la siri la kompyuta, kodi ya kuingilia kwenye kompyuta au taarifa zinazofanana na hizo ambazo mfumo mzima au sehemu ya mfumo wa kompyuta unaweza kufikiwa, kwa nia ya kwamba itumiwe na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutenda kosa dhidi ya sheria yoyote;

(b) ana kitu kilichotajwa katika aya ndogo ya (i) au (ii) katika milki yake kwa nia ya kwamba kitumiwe na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutenda kosa dhidi ya sheria yoyote,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano.

Kosa dhidi ya watumiaji wa kompyuta.

**376.**-(1) Mtu yeyote ambaye kwa makusudi, kwa kujua, na bila ya idhini:

(a) anatumia au anasababisha kutumia kompyuta yoyote, mfumo wa kompyuta, au mtandao wa kompyuta; au

(b) anamkatalia au anasababisha kukataliwa kwa huduma za mfumo wa kompyuta kwa mtumiaji aliyeruhusiwa wa huduma hizo za mfumo wa kompyuta, ambao, mfumo wote au sehemu ya mfumo huo, unamilikiwa na, chini ya mkataba na, au unaendeshwa na, au kwa niaba ya, au pamoja na mtu mwengine,

atakuwa ni mkosa dhidi ya watumizi wa kompyuta, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Tano.

(2) Ikiwa kosa linatendwa kwa madhumuni ya kutengeneza au kutekeleza mpango wowote au ujanja kwa kudanganya au kupata mali yoyote, basi mtu huyo atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi, au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi.

Udanganyifu na kitendo kinachohusiana na kompyuta za Serikali.

**377.** Mtu yeyote ambaye:

(a) akiwa anajua ametumia kompyuta bila ya idhini au amepindukia idhini ya matumizi aliyoruhusiwa, na kwa njia ya kitendo hicho amepata taarifa ambayo imeamuliwa na Serikali kwa mujibu wa amri ya kiutawala au sheria inayohitaji kulindwa dhidi ya kuwekwa bayana

kusiko ruhusika kwa sababu za ulinzi wa taifa au kwa mahusiano ya kimataifa, au taarifa zozote zilizozuiliwa, kwa sababu ya kuamini kwamba taarifa hizo zilizopatikana hivyo zingeweza kutumiwa kuiathiri Zanzibar, au kwa manufaa ya nchi yoyote ya kigeni kwa makusudi anawasiliana, anatoa, anasafirisha, au anasababisha kuwasilishwa, kutolewa, kusafirishwa, au anajaribu kuwasilisha, kutoa, kusafirisha au anajaribu kusababisha kuwasilishwa, kutolewa, au kusafirishwa taarifa hizo kwa mtu yeyote ambaye hastahiki kupokea taarifa hizo, au kwa makusudi anazuia taarifa hizo na anashindwa kuzitoa taarifa hizo kwa afisa au muajiriwa wa Serikali anayestahiki kupokea taarifa hizo;

(b) kwa makusudi anatumia kompyuta bila ya idhini au anapindukia idhini ya matumizi, na kutokana na kufanya hivyo anapata:

(i) taarifa zilizomo katika kumbukumbu za kifedha za taasisi ya fedha;

(ii) taarifa kutoka idara yoyote au wakala wa Serikali;

(iii) taarifa kutoka katika kompyuta yoyote iliyohifadhiwa ikiwa kitendo kimehusisha mawasiliano baina ya mataifa au ya kigeni;

(iv) kwa makusudi, bila ya idhini kutumia kompyuta yoyote iliyozuiwa ya idara au wakala wa Serikali, anatumia kompyuta hiyo ya idara hiyo au wakala ambayo ni kwa matumizi pekee ya Serikali;

(v) kwa kujua na kwa nia ya kudanganya, anatumia kompyuta iliyohifadhiwa bila ya idhini, au anapindukia matumizi yaliyoruhusiwa, na kwa njia ya kitendo hicho anawezesha udanganyifu uliokusudiwa na anapata kitu chochote chenye thamani,

atakuwa ni mkosa na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na tano au atatozwa faini isiyozidi shilingi milioni kumi na tano.

Tafsiri ya maneno ndani ya Sehemu hii.

**378.** Katika Sehemu hii:

"kompyuta" maana yake ni kifaa cha umeme, sumaku, muangaza, kemikaliumeme, au kifaa chengine kuchakata taarifa kwa haraka kinachofanya kazi za kimantiki, kihesabu, au kuhifadhi, na inajumuisha huduma yoyote ya kuhifadhi taarifa au huduma ya mawasiliano inayohusiana moja kwa moja

au inayofanyakazi kwa pamoja na kifaa hicho, lakini haijumuishi mashine ya uchapaji au mashine ya kupanga maandishi kwa ajili ya uchapaji, kikokotoa cha mkononi, au kifaa chengine kinachofanana nacho;

"mtandao wa kompyuta" maana yake ni kundi la mifumo ya kompyuta na vifaa vyengine vya kompyuta ambavyo vinaunganishwa pamoja kupitia njia za mawasiliano kwa ajili ya kuwezesha mawasiliano na utumiaji wa pamoja wa taarifa miongoni mwa watumiaji walio wengi;

"taarifa za kompyuta" maana yake ni taarifa zinazotengenezwa au kuhifadhiwa na kompyuta, na taarifa hizo zinaweza kuwa katika utaratibu wa maandishi, picha, sauti, programu za softiweya, au aina nyengine za taarifa;

"mfumo wa kompyuta" maana yake ni mfumo wa kompyuta zilizounganishwa ambazo zinatumia kwa pamoja mfumo mkuu wa kuhifadhi na vifaa mbali mbali vya nje kama printa, skana au ruta;

"madhara" maana yake ni kikwazo chochote kuhusu usahihi au upatikanaji wa taarifa, programu, mfumo au maelezo;

"kupindukia mpaka wa matumizi yaliyoruhusiwa" maana yake ni kutumia kompyuta kwa mujibu wa idhini na kutumia idhini hiyo kwa ajili ya kupata au kubadilisha taarifa katika kompyuta ambapo mtumiaji hana haki ya kuzipata au kuzibadilisha;

"taasisi ya fedha" maana yake ni taasisi ya fedha kama ilivyotafsiriwa chini ya sheria inayosimamia taasisi za fedha;

"kumbukumbu za fedha" maana yake ni taarifa inayopatikana kutoka kwenye kumbukumbu yoyote inayotunzwa na taasisi ya fedha kuhusu uhusiano wa mteja na taasisi ya fedha;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama hali itakavyokuwa;

"hasara" maana yake ni gharama yoyote ya kawaida ya muathirika yeyote, inajumuisha gharama ya kushughulikia kosa, kufanya tathmini ya hasara, na kurejesha tena uhifadhi wa taarifa, programu, mfumo au maelezo katika hali yake kabla ya kufanyika kosa, na mapato yoyote yaliyopotea, gharama zilizoingiwa, au hasara nyengine zozote zilizoingiwa kwa sababu ya kusitishwa kwa huduma;

"mtu" maana yake ni mtu yeyote, kampuni, shirika, taasisi ya elimu, taasisi ya fedha, taasisi ya Serikali, au taasisi ya kisheria au taasisi nyengine; na

"kompyuta inayolindwa" maana yake ni kompyuta:

(a) kwa matumizi pekee ya taasisi ya fedha au Serikali;

(b) ambayo inatumika katika biashara au mawasiliano ya mataifa au ya kigeni, inajumuisha kompyuta iliyopo nje ya Zanzibar ambayo inatumika katika namna ambayo inaathiri biashara au mawasiliano ya Serikali ya mataifa au ya kigeni.

## SEHEMU YA THELATHINI NA SITA
## KUGHUSHI ALAMA ZA BIASHARA

Tafsiri ya alama ya biashara.

**379.** Alama ya biashara ni:

(a) alama inayotumiwa kihalali na mtu yeyote kuonesha kitu chochote kuwa ni kifaa au kitu cha kutengeneza, ustadi, uzalishaji au bidhaa ya mtu huyo au kuwa ni kitu cha namna ya kipekee au cha namna mahsusi ambacho kinatengenezwa au kinauzwa na mtu huyo;

(b) alama yoyote au ishara ambayo kwa mujibu wa sheria yoyote inayotumika kwa wakati huo inayohusiana na alama zilizoandikishwa, inatakiwa kuwekwa au kubandikwa kwenye chombo au kitu chochote wakati wa kuwepo au kuendelea kuwepo kwa haki miliki yoyote au haki nyengine ya pekee ambayo imepatikana chini ya masharti ya sheria hiyo.

Kughushi alama za biashara.

**380.**-(1) Mtu yeyote ambaye anafanya moja kati ya mambo yafuatayo kwa nia ya kudanganya au kumuwezesha mwengine kumdanganya mtu mwengine:

(a) anaghushi au anaiga alama zozote za biashara;

(b) anatumia alama zozote za biashara, au alama yoyote ya biashara iliyoghushiwa au iliyoigizwa katika kitu chochote au kifaa chochote ambacho si bidhaa ya mtu ambaye alama yake ya biashara katika kitu au kifaa hicho imeghushiwa au imeigizwa;

(c) anatumia alama zozote za biashara, au alama yoyote ya biashara iliyoghushiwa au iliyoigizwa katika kitu chochote au kifaa chochote ambacho si chenye maelezo mahsusi au ya kipekee ya bidhaa

inayooneshwa au inayokusudiwa kuoneshwa na alama hiyo ya biashara au alama hiyo ya biashara iliyoghushiwa au iliyoingizwa;

(d) anatumia alama zozote za biashara, au alama yoyote ya biashara iliyoghushiwa au iliyoigizwa katika kitu chochote kinachokusudiwa kwa madhumuni ya biashara au uzalishaji, au katika, juu au pamoja na kitu au kifaa chochote kinachokusudiwa kuuzwa, au kinachouzwa au kinachotangazwa au kuwekwa wazi kwa ajili ya kuuzwa;

(e) anafungia au anaweka kifaa au kitu chochote ndani, juu, chini au pamoja na kitu chochote ambacho alama yoyote ya biashara imetumiwa kwa njia ya uongo, au ambapo alama yoyote ya biashara iliyoghushiwa au iliyoigizwa imetumika;

(f) anatumia au anaambatanisha kitu chochote au kifaa chochote katika kasha, kifuniko, kiringi, tiketi, alama au kitu chengine chochote ambacho alama yoyote ya biashara imetumika kwa uongo, au ambapo alama yoyote ya biashara ya uongo au ya kuigizwa imetumika; au

(g) anafungia, anaweka au anaambatanisha kitu chochote au kifaa chochote ndani ya, juu ya, chini ya, pamoja na, au katika kitu chochote ambacho juu yake kina alama ya biashara ya mtu mwengine yeyote,

atakuwa ni mkosa.

(2) Mtu ambaye anayetenda kosa lolote hilo kama lilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu au kifaa hicho kitataifishwa na Serikali:

(a) vitu au vifaa ambavyo alama hiyo yoyote ya biashara au alama ya biashara iliyoghushiwa inatumika au inasababishwa au inawezeshwa kutumika;

(b) kifaa kwa ajili ya kutumia alama yoyote iliyo ya biashara au alama ya biashara iliyoghushiwa katika milki yake au katika mamlaka yake;

(c) vifaa, vitu na vitu hivyo vilivyotajwa katika aya ndogo za (d), (e) na (g) vya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na vitu vinavyofanana na hivyo vinavyofanywa vitumike katika namna kama hiyo vilivyopo katika milki yake au mamlaka yake.

## SEHEMU YA THELATHINI NA SABA
## KUJIFANYA MTU MWENGINE

Kujifanya mtu mwengine kwa ujumla.

**381.**-(1) Mtu yeyote ambaye, kwa nia ya kumdanganya mtu mwengine, kwa njia ya uongo anajifanya kuwa ni mtu mwengine, aliyehai au aliyekufa, atakuwa ni mkosa.

(2) Iwapo kujifanya huko ni kwamba mkosaji ni mtu anayestahiki kwa wasia au kwa utekelezaji wa sheria mali yoyote maalum na anatenda kosa la kujipatia mali hiyo au mali hiyo kuwa katika milki yake, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kwa udanganyifu anatoa maelezo ya kukiri dhima.

**382.** Mtu yeyote ambaye, bila ya mamlaka halali au sababu ya msingi, uthibitisho wa sababu hiyo utakuwa juu yake, anatoa, kwa jina la mtu mwengine yeyote, mbele ya Mahakama yoyote au mbele ya mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kuchukua maelezo ya kukiri dhima hiyo, maelezo ya kukiri dhima ya aina yoyote, au maelezo ya kukiri hati au hati nyengine ya kisheria, atakuwa ni mkosa.

Kujifanya mtu aliyeandikwa katika cheti.

**383.** Mtu yeyote ambaye anatoa waraka wowote ambao umetolewa na mamlaka halali kwa mtu mwengine, na ambapo mtu huyo mwengine anathibitishwa kuwa ni mtu mwenye sifa zozote zinazotambuliwa na sheria kwa madhumuni yoyote, au kuwa ni mtu mwenye dhamana ya ofisi yoyote, au ana haki ya kuitumikia taaluma yoyote, biashara au shughuli, au anastahiki haki yoyote, fursa au kutumia cheo chochote au hadhi, na kwa uongo akajifanya kuwa ni mtu aliyetajwa katika waraka huo, atakuwa ni mkosa wa kosa la aina ile ile na atapewa adhabu ile ile kama ameghushi waraka huo.

Kuazimisha, waraka au cheti kwa kujifanya mtu mwengine.

**384.** Mtu yeyote ambaye, akiwa mtu ambaye kwake yeye waraka wowote umetolewa na mamlaka halali ambapo anathibitishwa kuwa ni mtu mwenye sifa zozote zinazotambulika na sheria kwa madhumuni yoyote, au kuwa ni mtu mwenye dhamana ya ofisi yoyote, au shughuli au kuwa na haki ya kuitumikia taaluma yoyote, biashara au shughuli, au anastahiki kuwa na haki yoyote au fursa, au kutumia cheo chochote au hadhi, anauza, anatoa, anaazimisha waraka kwa mtu mwengine kwa nia ya kwamba huyo mtu mwengine aweze kujifanya kuwa ni mtu aliyetajwa ndani ya waraka huo, atakuwa ni mkosa.

Kujifanya mtu aliyetajwa kwenye uthibitisho wa tabia.

**385.** Mtu yeyote ambaye, kwa madhumuni ya kutaka kupata kazi yoyote, anatoa waraka wowote wenye asili ya kuthibitisha tabia ya mtu uliotolewa kwa mtu mwengine, atakuwa ni mkosa, na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Kuazimisha uthibitisho kwa ajili ya kujifanya mtu mwengine.

**386.** Mtu yeyote ambaye, akiwa ni mtu ambaye kwake yeye waraka wowote ule kama ulivyotajwa katika kifungu cha 385 umetolewa, anatoa, anauza au anaazimisha waraka huo kwa mtu mwengine kwa nia kwamba, mtu huyo mwengine aweze kuutoa waraka huo kwa madhumuni ya kujipatia ajira yoyote, atakuwa ni mkosa.

## SEHEMU YA THELATHINI NA NANE
## KUJARIBU

Tafsiri ya kujaribu.

**387.**-(1) Iwapo mtu, amekusudia kutenda kosa, anaanza kuweka nia yake hiyo katika utekelezaji kwa njia ya kutimiza utekelezaji wake, na anaonesha nia yake kwa kitendo fulani cha wazi, lakini hajakamilisha nia yake kwa kiasi ambacho kuwa ametenda kosa, atachukuliwa kuwa amejaribu kutenda kosa hilo.

(2) Haijalishi, isipokuwa kuhusiana na adhabu, ama mkosaji amefanya mambo yote ambayo ni muhimu kwa upande wake kwa ajili ya kukamilisha kutenda kosa, ama utekelezaji kamili wa nia yake umezuiliwa na mazingira yaliyo nje ya uwezo wake, au alijizuia yeye mwenyewe asiendelee kutekeleza nia yake.

(3) Haijalishi kwamba kwa sababu ya mazingira ambayo mkosaji hayajui haitawezekana kiuhalisia kutenda kosa.

Kujaribu kutenda makosa.

**388.** Mtu yeyote ambaye anajaribu kutenda kosa lisilokuwa katika makosa yaliyotajwa katika kifungu cha 389, atakuwa ni mkosa, ikiwa hakuna adhabu nyengine iliyotolewa, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi cha miaka miwili.

Adhabu kwa kujaribu kutenda baadhi ya makosa.

**389.** Mtu yeyote ambaye anajaribu kutenda kosa la aina ambayo kwamba mtu anayetiwa hatiani kwa kosa hilo anapewa adhabu ya kifo au kifungo kwa kipindi cha miaka kumi na nne au zaidi pamoja na au bila ya adhabu nyengine, atakuwa ni mkosa, ikiwa hakuna adhabu nyengine iliyotolewa, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba.

Kushawishi au kuchochea wengine kutenda kosa ndani ya Zanzibar au kwengine.

**390.**-(1) Mtu yeyote ambaye anashawishi au anachochea au anajaribu kumuwezesha mtu mwengine kufanya kitendo chochote au kuacha kufanya, ama ndani ya Zanzibar au mahala kwengine, ambacho kwa maumbile kwamba, ikiwa kitendo hicho kingefanywa au kingeachwa kufanywa, kosa lingekuwa limetendeka chini ya sheria za Zanzibar au sheria zinazotumika pahala pengine ambapo kufanya au kuacha kufanya huko kunapendekezwa, ama na yeye mwenyewe au na huyo mtu mwengine,atakuwa ni mkosa wa kosa la aina ile ile na atapewa adhabu ile ile kama kwamba yeye mwenyewe amejaribu kufanya kitendo hicho au ameacha kufanya kitendo hicho ndani ya Zanzibar.

(2) Ikiwa kutenda au kuacha kutenda kunapendekezwa kufanywa au kutekelezwa pahala nje ya Zanzibar, adhabu haitozidi ile ambayo angepewa chini ya sheria zinazotumika pahala ambapo kutendwa au kuacha kutendwa kunapendekezwa kufanywa au kutekelezwa, ikiwa yeye mwenyewe alijaribu kutenda kitendo kinachopendekezwa au kuacha kutenda kunakopendekezwa.

(3) Ikiwa kutenda au kuacha kutenda kunapendekezwa kufanywa au kutekelezwa pahala ambapo sio ndani ya Zanzibar, mashtaka hayatofunguliwa isipokuwa kwa ombi la Serikali ya nchi yenye mamlaka ndani ya pahala ambapo kutenda au kuacha kutenda kulipendekezwa kufanywa au kutekelezwa.

Kupuuza kuzuia kosa.

**391.** Mtu yeyote ambaye, akijua kwamba mtu yeyote anapanga kutenda au anatenda kosa, anashindwa kutumia njia zote muafaka za kuzuia kutendwa au kukamilishwa utendaji wa kosa hilo, atakuwa ni mkosa.

## SEHEMU YA THELATHINI NA TISA
## KULA NJAMA

Kula njama ya kutenda kosa.

**392.**-(1) Mtu yeyote ambaye anakula njama na mwengine kutenda kosa, au kutenda kitendo chochote katika sehemu yoyote ya dunia ambacho kama kingetendwa Zanzibar kingekuwa ni kosa lenye adhabu, na ambalo ni kosa chini ya sheria zinazotumika katika pahala ambapo kinapendekezwa kutendwa, atakuwa ni mkosa.

(2) Ikiwa kosa lililoliwa njama chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki lina adhabu ya kifungo kisichozidi miaka miwili, mtu anayekula njama atapewa adhabu ya kifungo cha miaka miwili.

(3) Ikiwa kosa lililoliwa njama chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki lina adhabu ya kifungo kinachozidi miaka miwili, mtu anayekula njama atapewa adhabu ya kifungo cha miaka saba.

Njama nyenginezo.

**393.** Mtu yeyote anayekula njama na mwengine kufanya moja kati ya makusudio yafuatayo:

(a) kuzuia au kupinga utekelezaji wa sheria yoyote au amri;

(b) kuathiri biashara yake, taaluma au kazi;

(c) kusababisha madhara yoyote kwa mtu au heshima ya mtu, au kupunguza thamani ya mali ya mtu;

(d) kuzuia au kupinga uhaulishaji huru na halali wa mali yoyote kwa mmiliki wa mali hiyo kwa ajili ya thamani yake halali;

(e) kumdhuru mtu katika biashara yake au taaluma;

(f) kuzuia au kupinga, kwa njia ya kitendo chochote au vitendo ambavyo ikiwa vinafanywa na mtu binafsi vingekuwa kosa kwa upande wake, utumiaji huru halali wa mtu yeyote kutekeleza kusudio lolote lisilo halali; au

(g) kutekeleza kusudio lolote halali kwa njia ambazo sio halali,

atakuwa ni mkosa.

## SEHEMU YA AROBAINI
## WASHIRIKI WA UHALIFU BAADA YA KUTENDEKA KOSA

Tafsiri ya kushiriki uhalifu baada ya kutendeka kosa.

**394.**-(1) Mtu yeyote ambaye anampokea au anamsaidia mtu mwengine ambaye, kwa kujua, ni mkosa, ili amuwezeshe mtu huyo kukimbia adhabu, atahesabiwa kuwa ni mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka.

(2) Mke hatokuwa mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutokea ambalo mume wake ni mkosa kwa kumpokea au kumsaidia ili amuwezeshe kukimbia adhabu; au kwa kumpokea au kumsaidia, mbele ya mume wake na kwa amri ya mume wake, mtu mwengine ambaye ni mkosa ambapo katika utendaji wa kosa hilo mume wake alishiriki, ili amuwezeshe mtu huyo mwengine kukimbia adhabu; wala mume hatokuwa mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka ambapo mke wake ni mkosa kwa kumpokea au kumsaidia mke wake ili amuwezeshe kukimbia adhabu.

Adhabu ya mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka.

**395.** Mtu yeyote ambaye anakuwa mshiriki wa uhalifu baada ya kosa kutendeka, atakuwa ni mkosa, na ikiwa hakuna adhabu nyengine iliyotolewa, atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu.

Adhabu ya kumshawishi au kumchochea mtu mwengine kutenda kosa.

**396.** Mtu yeyote ambaye anamshawishi au anamchochea mtu mwengine kutenda kosa atakuwa ni mkosa bila kujali kwamba ushawishi huo au uchochezi huo haukuwa na athari.

Kufuta na masharti ya mpito.

**397.**-(1) Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya 2004 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililopo katika Mahakama yoyote kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii litashughulikiwa na litatolewa maamuzi chini ya Sheria iliyofutwa kama kwamba hakuna ufutaji uliofanywa chini ya Sheria hii.

## JADWELI

## ORODHA YA MAHUSIANO YANAYOKATAZWA

**[Kifungu cha 143(1)]**

(i) mama

(ii) baba

(iii) mtoto wa kike wa mama

(iv) mtoto wa kiume wa baba

(v) mtoto wa kike

(vi) mtoto wa kiume

(vii) mama wa baba

(viii) baba wa baba

(ix) mama wa mama

(x) baba wa mama

(xi) mtoto wa kiume wa mtoto wa kike

(xii) mtoto wa kiume wa mtoto wa kiume

(xiii) mtoto wa kike wa mtoto wa kike

(xiv) mtoto wa kiume wa mtoto wa kike

(xv) dada

(xvi) kaka

(xvii) mama wa mke

(xviii) baba wa mume

(xix) mtoto wa kike wa mke

(xx) mtoto wa kiume wa mume

(xxi) dada wa baba

(xxii) kaka wa baba

(xxiii) dada wa mama

(xxiv) kaka wa mama

(xxv) mtoto wa kike wa kaka

(xxvi) mtoto wa kiume wa kaka

(xxvii) mtoto wa kike wa dada

(xxviii) mtoto wa kiume wa dada

(xxix) mke wa mtoto wa kiume

(xxx) mume wa mtoto wa kike

(xxxi) mke wa baba

(xxxii) mume wa mama

(xxxiii) dada wa kunyonya ziwa moja

(xxxiv) kaka wa kunyonya ziwa moja

(xxxv) mama mlezi

(xxxvi) baba mlezi.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 12 Februari, 2018.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***